Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 14 JULAI, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji na Hesabu za Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa Mwaka 2003/2004 (*The Annual Performance Report and Accounts of the Engineers Registration Board for the Year 2003/2004)*

Taarifa ya Kazi na Hesabu za Bodi ya Usajili wa Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31 Desemba, 2003, 2003 *(The Report on the Activities of the Architects and Quantity Surveyors Registration Board for the Year ended 31st December, 2003)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI**:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. ALI SAID SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni yake Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 254

### Pikipiki za Makatibu Tarafa

**MHE. LUCAS L. SELELII (K. n. y. MHE. STEPHEN M. KAHUMBI)** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imewapatia usafiri wa kuaminika Makatibu Tarafa wote nchini na kwa kuwa bado Serikali haijatoa maelekezo kuhusu umiliki wa pikipiki hizi: -

(a) Je, usafiri uliotolewa ni mkopo kwa Makatibu Tarafa na kama ni hivyo uamuzi huo utatolewa lini?

(b) Kwa kuwa pikipiki hizo zina namba za Serikali; je, anayezigharamia matengenezo na mafuta ni Makatibu Tarafa au ni *DAS?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi; Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Bajeti ya Mwaka 2001/2002 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kununua pikipiki kwa Makatibu Tarafa wote nchini. Jumla ya pikipiki 512 zilinunuliwa kutoka Japan na kugawiwa kwa Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Pikipiki moja ambayo haikuwa kwenye makisio ya awali kwa ajili ya Tarafa ya Kwamtoro Wilayani Kondoa ilinunuliwa na Serikali na kufanya Tarafa zote nchini kuwa na usafiri wa uhakika kwa ajili ya Makatibu Tarafa.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali haijatoa maelekezo kuhusu umiliki wake. Pikipiki hizo zimenunuliwa na Serikali, hivyo ni mali ya Serikali. Hata hivyo, uzoefu uliopatikana huko nyuma umeonyesha kuwa, matumizi ya vyombo vya usafiri vya Serikali siyo mazuri na Serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa katika kuhudumia vyombo hivyo.

Kutokana na uzoefu huo, Serikali ilitoa waraka maalum unaoelekeza utaratibu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri watumishi wake. Kwa kuzingatia waraka huo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikwishaielekeza Mikoa yote kuwasilisha taarifa za Makatibu Tarafa wanaohitaji kukopeshwa pikipiki hizo ili taratibu za kuwakopesha ziendelee kufanyika. Hadi sasa taarifa za Mikoa 15 zimekwishapokelewa na kuwasilishwa Hazina ukiwemo Mkoa wa Tabora. Mikoa ambayo haijawasilisha taarifa zake ni Mwanza, Manyara, Mbeya, Mtwara, Dodoma na Shinyanga.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi Katibu Tawala wa Mkoa ndiye Afisa Mhasibu wa Mkoa *(Warrant Holder)*. Katibu Tawala wa Wilaya siyo Afisa Mhasibu kulingana na taratibu na kanuni za fedha za Serikali, hivyo basi, anayepaswa kugharamia vyombo vyote vya usafiri vilivyo chini ya Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya mafuta na matengenezo ni Katibu Tawala wa Mkoa.

Hata hivyo, kutokana na ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge mlioutoa ndani ya Bunge hili ili kuwezesha fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Serikali ilikubali kuanzisha utaratibu huo kwa ajili ya ofisi hizo pamoja na Makatibu Tarafa. Kufuatia uamuzi huo, Katibu Tawala wa Wilaya sasa ni *Sub-Warrant Holder*. Hata hivyo, Afisa huyo bado analazimika kutoa maelezo ya matumizi ya fedha hizo kwa Katibu Tawala wa Mkoa ambaye ndiye Afisa Mhasibu wa Mkoa. Aidha, kuanzia Bajeti ya Mwaka 2002/2003 Mikoa ilielekezwa kutenga fedha kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa pikipiki za Makatibu Tarafa pamoja na mafuta, jambo ambalo limekwishaanza kutekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na pia ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ni ya umakini sana. Nina maswali mawili tu ya nyongeza: -

(a) Kwa kuwa nchi yetu ni kubwa, zipo baadhi ya Tarafa ambazo ni kubwa sana na zinalingana kama Wilaya na zipo baadhi ya Tarafa ambazo zinapita kwenye maeneo ya hatari. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba sasa ni wakati mzuri kwa Tarafa kama hizo ambazo ni kubwa Makatibu Tarafa wake wakapewa magari badala ya kupewa pikipiki?

(b) Kwa kuwa Tarafa hizo kubwa mgawanyo wake wa mafuta unalingana na Tarafa ambazo ni ndogo. Je, Waziri haoni kwamba ni wakati mzuri vile vile kwa Makatibu Tarafa hao kupewa mgao mkubwa wa mafuta ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi kuliko kupewa mafuta sawa na wengine ambao wana Tarafa ndogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Tarafa ambazo ni kubwa na baadhi ya barabara zake zinapita kwenye maeneo yenye wanyama wakali, Serikali inatambua jambo hilo na

tuliwahi kusema hapa kwamba linaangaliwa tuone namna tunavyoweza kusaidia Tarafa za aina hiyo ili kuondokana na uwezekano wa hatari ambayo inaweza ikatokea wanapokuwa na pikipiki katika maeneo yao. Kwa hiyo, tumeishalizingatia, tunasubiri tu tuone uamuzi utakuwaje na uwezo wa kifedha utakuwaje.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli kabisa kwamba kutokana na ukubwa huo, namna bora ilikuwa ni kugawa mafuta kulingana na uwiano wa kazi zenyewe zinavyotokana na ukubwa wa maeneo. Lakini kwa kuwa jambo hili tumeliweka mikononi mwa Mikoa, tunaomba Mikoa inapopanga Bajeti zake kwa ajili ya mafuta na fedha za matengenezo, basi lizingatiwe ili huku Serikalini liweze kupata baraka kwa kadri itakavyowezekana.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeishashusha madaraka ya matumizi ya fedha mpaka kwenye Wilaya kwa Makatibu Tawala, kuhusu suala la mafuta ya Makatibu Tarafa na matumizi mengine ya Makatibu Tarafa, ni kwa nini Serikali isigawe moja kwa moja kwamba sasa kila Katibu Tarafa kulingana na eneo kama alivyofanya anastahili kupata kiasi hiki cha fedha na kwamba fedha hizo zikapelekwa moja kwa moja wakazipata kwenye mishahara yao badala ya kupitia kwa Makatibu Tawala ambao nao wana uwezo wa kukubali au kukataa kumpa mafuta Katibu Tarafa huyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mfaki ni zuri na ninajua ndiyo Waheshimiwa Wabunge wengi wangependa ifanyike hivyo, lakini taratibu haziruhusu kwa sasa. Ni dhahiri kabisa unahitaji *Accounting Officer* au *Sub-Warrant Officer* ambaye ndiyo anawajibika kutoa mgao huo kwa kadri itakavyowezekana, lakini ni wazo ambalo tukilipeleka pengine kwenye vyombo vinavyohusika wanaweza wakalitazama kama uwezekano upo, lakini kwa sasa utaratibu ndiyo huo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongezee vile vile kwamba, suala hili la mafuta bado kwa kweli halijafanyiwa kazi ya kutosha. Katika baadhi ya Mikoa wastani wa matumizi ya mafuta kwa wiki kwa Katibu Tarafa mmoja ni kama lita 21, lakini haiwezi ikatumika kama ndiyo wastani kwa nchi nzima.

Kwa hiyo, bado tunalifanyia uchambuzi tuone namna tunavyoweza kufanya vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa.

Na. 255

**Ujenzi wa Hospitali/Kituo cha Afya**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza: -

Kwa kuwa Mji wa Tunduma umepewa hadhi ya kuitwa Mji Mdogo na kwa kuwa kulingana na Sensa ya Mwaka 2002 Mji huu una wakazi zaidi ya 35,000 na kwa kuwa uwingi huo wa watu hauwezi kuhudumiwa na Zahanati: -

Je, Serikali ina mpango gani wowote wa kujenga Hospitali au Kituo cha Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa; Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi ina idadi ya watu wapatao 515,270 na ina jumla ya Zahanati za Serikali na Mashirika ya Dini 42, Vituo vya Afya vitatu (3) na Hospitali ya Wilaya moja (1). Kulingana na sensa ya mwaka 2002, Mji Mdogo wa Tunduma una watu 34,461 na hivyo kuhitaji Kituo cha Afya badala ya Zahanati. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imekuwa ikitenga fedha za upanuzi wa Zahanati ya Tunduma ili kuifanya iwe na hadhi ya Kituo cha Afya. Katika Mwaka wa Fedha 2004/2005 jumla ya fedha Sh.27,128,214/= zilitengwa kwa ajili ya kujenga Wodi ya Wazazi kwa gharama ya Sh.13,.424,964/= na Wodi ya Watoto kwa gharama ya Sh.13,703,250/=.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huo huo wa fedha, Serikali ilitenga jumla ya Sh.27,904,470/= kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Wanaume ambayo itagharimu Sh.13,525,320/=. Ujenzi wa Nyumba ya Kuhifadhia Maiti *(Mortuary)* ambayo itagharimu Sh.7,800,000/= na ujenzi wa uzio utakaogharimu Sh.7,200,000/=. Hivi sasa ujenzi huu bado unaendelea. Vile vile, Serikali imekuwa ikiipatia Zahanati ya Tunduma *kit* ya dawa ya hadhi ya Kituo cha Afya badala ya Zahanati. Ni dhahiri kuwa muda si mrefu Mji Mdogo wa Tunduma utakuwa na Kituo cha Afya badala ya Zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ili kutoa huduma zote za msingi katika Kituo hiki cha Afya bado ujenzi wa majengo mbalimbali yenye gharama ya Sh.112,550,000/= yanahitajika. Majengo haya ni pamoja na Jengo la Upasuaji *(Operating Theatre),* Wodi mbili za Upasuaji *(Surgical Wards),* Wadi ya Magonjwa ya Mlipuko *(Isolation Wards)*, nyumba sita za Wafanyakazi na ununuzi wa Jokofu la Kuhifadhia Maiti.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwa juhudi zake anazofanya ili kuwapatia maendeleo Wananchi wa Jimbo lake ikiwa ni pamoja na kuwezesha kupatikana kwa Kituo hiki cha Afya cha Tunduma. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninaipongeza Serikali kwa jitihada hiyo na ninawapongeza Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Viongozi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri alivyosema, inaonekana kuwa kwa fedha zilizotengwa inaweza ikachukua muda mrefu sana kumaliza kituo hicho na sasa hivi wagonjwa wanazidi kuwa wengi pamoja na wengine kutoka nchi ya jirani ya Zambia wanakuja pale. Je, wanaweza wakaongeza fedha ili kuwe na *speed* kali ya kumaliza mapema/haraka iwezekanavyo mwishoni mwa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hivyo tulivyofanya ndiyo tumeongeza *speed* kweli kweli. Uwezo wa Serikali ulipofika ndiyo hapo.

Lakini naomba Mheshimiwa Simpasa kwa kuwa ninafahamu umahiri wake, tushauriane vizuri na Halmashauri, tuandae andiko maalum, tujaribu kutafuta wahisani wengine ambao najua watakuwa tayari kusaidia kama Ubalozi wa Japan na sehemu nyingine ambazo najua wako tayari kufanya kazi kama hizo ili Serikali iendelee kutoa huduma hiyo katika maeneo mengine kwa kuwa mahitaji ni makubwa sana.

Na. 256

**Ubinafsishaji wa Shamba la Malonje**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza: -

Kwa kuwa ubinafsishaji wa mashamba ya mifugo umekaribia kukamilika nchi nzima chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo: -

(a) Je, kwa nini Shamba la Malonje halijabinafsishwa kwa kuligawa shamba hilo kwa maeneo madogo madogo ya hekta 50 kila moja ili wafugaji wadogo waanze kulitumia eneo hilo?

(b) Je, shamba la Kalambo limepata wawekezaji wangapi wa ndani na wangapi wa nje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ubinafsishaji wa shamba la Malonje lenye hekta 15,000 haujakamilika. Mkakati wa Serikali kuhusu ubinafsishaji wa shamba hili umelenga kuligawa katika maeneo ya hekta 50 kila moja na kuyamilikisha kwa Watanzania Wazalendo wenye nia na uwezo wa kuyaendeleza kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Kazi hii haijafanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Fedha zinahitajika kwa ajili ya kupima upya eneo lote, kutenga maeneo ya hekta 50 kila moja na kulipa madeni mbalimbali yaliyorithiwa kutoka kwa Kampuni ya Uzalishaji wa Maziwa

*(DAFCO)* na yale yaliyojikusanya baada ya *DAFCO* kufa. Vile vile, fedha zinahitajika kulipa mafao ya watumishi 18 ambao ajira yao itakoma.

Wizara yangu inatarajia kuikamilisha kazi hii kupitia Serikali ya Mkoa wa Rukwa katika mwaka 2005/2006 baada ya kupata fedha. Nawaomba Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wajitokeze kumiliki maeneo hayo mara baada ya kupimwa na kutangazwa.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kuhusu umilikishaji wa Ranchi za Taifa *(NARCO)* ni kuyagawa mashamba hayo katika ranchi ndogo ndogo ambazo zitamilikishwa kwa Wawekezaji Watanzania na kubakiza eneo la hekta 20,000 za mfano kwa kila ranchi ambazo zitaendelezwa na *NARCO*.

Mheshimiwa Spika, ranchi ya Kalambo ilipimwa na kupata jumla ya ranchi ndogo ndogo 13 zenye ukubwa wa hekta 2,100 hadi 3,100 kila moja. Matangazo ya kutafuta wawekezaji yalitolewa katika magazeti mwezi Mei 2004 na jumla ya wawekezaji 40 walijitokeza. Wawekezaji 13 kulingana na *size* za mashamba yaliyopimwa walifanikiwa ikiwa ni pamoja na vikundi vitatu vya wafugaji kutoka vijiji jirani vya Mbuluma, Lolesha na Sintali, Vikundi vya Ushirika na Makampuni sita na Watu Binafsi wanne. Wawekezaji wote hawa ni Wazalendo na hakuna anayetoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Wananchi wote waliomilikishwa ranchi ndogo ndogo hizo kuzingatia taratibu za kuyaendeleza maeneo hayo kulingana na mikataba waliyoingia. Shamba la Malonje ni kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Wananchi wa eneo hilo la Malonje pamoja na Kata nzima ya Molo wamekuwa na kiu sana ya kutaka kazi hii ikamilike haraka iwezekanavyo na baada ya mimi mwenyewe kama Mbunge wa eneo hilo kuhamasisha waanze kuchangia fedha, hadi sasa wameishafikisha Sh.7,000,000/=. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kuiomba Serikali katika mpango wa MKUKUTA na Serikali yenyewe isaidie jitihada za Wananchi ili waweze kuchukua shamba hilo mapema iwezekanavyo? *(Makofi)*

(b) Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, *Captain* George Mkuchika, ameishaiomba Serikali ili ione uwezekano wa kuharakisha mpango huu ili Wananchi waanze kutumia eneo hilo haraka iwezekanavyo na kwamba Serikali inaombwa itoe mapendekezo jinsi ya kuweza kufanya shamba hilo likatumika vizuri haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza ni kwamba, mwaka huu ndiyo fedha zimetengwa kwa ajili ya upimaji. Hatuwezi kuharakisha kabla ya kupima na kuweka eneo katika hali inayokubalika kisheria. Pia, tumetenga fedha kwa ajili ya kulipa wafanyakazi. Kuna wafanyakazi 18 na ilitakiwa walipwe ili wawekezaji watakaopewa maeneo hayo wasiwe na mgogoro tena wa kikazi na wafanyakazi waliopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Mkuchika kutuandikia, jambo hilo linaeleweka kwa sababu sisi ndiyo tulikuwa wa kwanza kuwaandikia ili utaratibu utakapokamilika tu wao wawahamasishe Wananchi wa Wilaya inayozunguka ya Sumbawanga ili waweze kufaidika na mpango huu.

Na. 257

**Haki ya Walemavu Kusomeshwa Bure**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K. n. y. MHE. HENRY D. SHEKIFFU)** aliuliza: -

Kwa kuwa kwa kipindi kirefu Bunge limekuwa likiiomba Serikali itamke wazi haki ya walemavu ya kusomeshwa bure: -

(a) Je, ni lini Serikali itatoa mwongozo na tamko rasmi kwa walemavu kusomeshwa bure na kuwaonya Walimu wanaowasumbua walemavu kwa kuwafukuza na kukatisha masomo yao kwenda kutafuta ada na kadhalika?

(b) Kwa kuwa vifaa vya kufundisha walemavu wasioona ni ghali na ni haba mashuleni; je, ni hatua zipi zimechukuliwa kurekebisha upungufu huo wa vifaa mashuleni, kwa mfano Shule ya Wasioona ya Irente – Lushoto?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K. n. y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu; Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 kifungu cha tatu (3), Serikali inatoa elimu kwa wote bila kubagua mtu kwa msingi wa rangi, dini, kabila, jinsi au maumbile. Kupitia MMEM 2002 – 2006 Serikali inatekeleza mpango huo kwa kutoa Elimu ya Msingi bure na ya lazima kwa watoto wote. Katika Elimu ya Sekondari kwa utaratibu wa sasa mzazi au mlezi hutakiwa achangie angalau kiasi kidogo gharama za elimu hiyo cha Sh20,000/= kwa mwaka. Hata hivyo, Serikali imeweka utaratibu wa kuwasaidia wale wasiokuwa na uwezo wa kulipia ada ya watoto wao waliofaulu vizuri kuingia Sekondari. Kuwa na ulemavu peke yake siyo sifa ya kutosha kupewa msaada huo kwa sababu kinachoangaliwa ni uwezo wa mzazi kumlipia.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Wasioona ni ghali sana. Wizara yangu katika Mipango ya MMEM na MMES imetenga kiasi kikubwa zaidi cha fedha mwaka huu wa 2005/2006 za kununulia vifaa mbalimbali vya wenye ulemavu, kujenga madarasa na majengo mengine yanayozingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Aidha, aina 30 za vitabu vinavyohusu mtaala katika breli zitachapishwa na kusambazwa nakala 24,000 kwa ajili

ya Wanafunzi Wasioona. Aidha, Walimu Wataalam 300 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya Breli, Lugha ya Alama na Stadi za Maisha. Nina hakika kuwa Shule ya Wasioona ya Irente iliyoko Lushoto itanufaika na mpango huu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.Imedhihirika wazi kabisa kwamba Taasisi Binafsi na Madhehebu mbalimbali ya Dini yamejitahidi sana kusaidia walemavu ambao hawana ndugu wa kuwasaidia. Je, huu si wakati mzuri wa Serikali kuunga mkono nguvu za Taasisi hizo kwa kuzipa ruzuku chini ya Wizara hii ya Kazi ambayo Naibu Waziri wake amejibu swali hili ili kuwe na utaratibu wa kudumu wa kuweza kuwahudumia kwa kusaidia kule kwenye Taasisi ambazo zimeshaanza kazi hizo kama Irente, Buigiri hapa Dodoma na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K. n. y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Utamaduni kuanzia mwaka wa kwanza wa mpango wa MMES imeamua kuchangia Shule za Watu Binafsi na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali kwa kiwango kile kile kinachopelekwa katika Shule za Serikali. Kwa mfano shule hiyo ikiishathibitishwa, tuna Afisa Elimu Kiongozi, inapewa Sh.7,000,000/= kwa ajili ya darasa, Sh.9,000,000/= kwa ajili ya nyumba ya mwalimu na kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2005 tulitumia jumla ya Shilingi bilioni 2.5 katika mpango huo na tumesaidia shule mbili za watu binafsi kuchangia ujenzi wa madarasa na kwa mwaka huu tumetenga kiasi kikubwa zaidi kwa ajili ya kutoa ruzuku ya wanafunzi wanaosoma pale Sh.15,000/= kwa kila mwanafunzi. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali bado ina Sekondari za Kutwa na za Bweni ambazo hugharamiwa na Serikali na kwa kuwa ninaishukuru Serikali kwa kupunguza ada kuwa Sh.20,000/=. Je, hiyo ada ya Sh.20,000/= ni kwa ajili ya Shule za Sekondari za Serikali za Kutwa ama kwa Shule za Sekondari za Serikali za Bweni tu?

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu Shule za Walemavu. Kwa hiyo, tuendelee na walemavu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imechukua hatua ambayo inastahili pongezi ya kuwasomesha watoto wengi yatima na wale ambao ni walemavu na kwa kuwa kila mtoto anapopewa fursa hii akiingia darasa la tisa au *form one* anategemewa aendelee na msaada huu mpaka akifika *Form Four.*

Je, Serikali inaweza kutoa tamko rasmi hapa Bungeni kwamba Walimu wasiwasumbue watoto hawa ambao tayari wamepewa msaada wa Serikali ili waweze kusoma bila bughudha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K. n. y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, tunawasihi na tunawaagiza Walimu Wakuu wasiwasumbue watoto, lakini wakati huo huo tunawaomba wazazi na walezi wakumbuke wajibu wao wa kuchangia Sh.20,000/= ili watoto wao hata kama hawakufukuzwa wasijisikie wanyonge. Hata hivyo, nitumie nafasi hii vile vile kumpongeza Sana Profesa Maghembe kwa kuisimamia vizuri Shule ya Watu wenye Ulemavu ya Mramba na kuweza kupata msaada wa Wizara wa kujengewa madarasa matatu. *(Makofi)*

Na. 258

**Utoaji wa *Statement* kwa Mtuhumiwa**

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD (K. n. y. MHE. RAMADHAN NYONJE PANDU** aliuliza: -

Kwa kuwa kila mtuhumiwa aliyetenda kosa anao uhuru wa kutoa maelezo yake *(statement)* mbele ya Afisa au Askari Polisi wa zamu aliyeko kituoni: -

(a) Je, ni sheria gani ya nchi/au ya Jeshi la Polisi inayompa haki au fursa Askari Polisi anapomkamata mtuhumiwa au mlalamikiwa kumchukua hadi nyumbani kwa mlalamikaji na kumhoji au kuchukua maelezo mbele yake kabla hajafikishwa kituoni?

(b) Kwa kuwa, kitendo kama hicho kimetokea dhahiri; je, Serikali haioni kwamba kitendo hicho kinamdhalilisha mtuhumiwa na hakimpi haki kamili na uhuru wa kujieleza?

(c) Kama sheria hiyo haipo na taratibu hizo hazikubaliki katika Jeshi la Polisi; je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho ni cha kujipendekeza kwa Askari wa aina hiyo kwa mlalamikaji na kwamba kina mazingira ya rushwa au kurubuniwa kwa Askari huyo na kama ikithibitika kuwa hilo ni kosa ni hatua gani za kinidhamu zinastahili kuchukuliwa dhidi ya kosa kama hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Nyonje Pandu; Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, chini ya sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai namba 9 ya mwaka 1985 Jeshi la Polisi limepewa uwezo wa kisheria wa kukamata, kupekua, kuhoji na kuandika maelezo ya watuhumiwa, pia kuandika maelezo ya mashahidi. Kwa mujibu wa sheria hiyo, upekuzi kama sehemu ya upelelezi unaweza kufanyika popote, ikiwa ni pamoja na nyumbani kwa mtuhumiwa.

Lakini mashtaka yote lazima yapokelewe katika chumba cha mashtaka kilichopo katika kila Kituo cha Polisi na shughuli za kumhoji mtuhumiwa kwa mujibu wa sheria

zinapaswa kufanyika ndani ya Kituo cha Polisi. Hivyo hakuna sheria yoyote ya Nchi au Kanuni ya Jeshi la Polisi, inayomruhusu Askari Polisi baada ya kumkamata mtuhumiwa kumchukua hadi nyumbani kwa mlalamikaji au nyumbani kwa mtuhumiwa na kumhoji au kuchukua maelezo yake kabla hajamfikisha na kumfungulia mashtaka kituoni. Kitendo kama hicho kama kiliwahi kufanyika ni ukiukwaji wa sheria za utendaji wa kazi za polisi na akibainika Askari Polisi mhusika anastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kifungu Na. 25 cha Kanuni za Jeshi la Polisi kama kilivyofafanuliwa katika *Government Notice* No. 193 ya mwaka 1995.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wapo watuhumiwa waliopelekwa rumande kwa muda mrefu na kesi zao hazijapatikana ushahidi ambayo mtu huyo huyo ukimpeleka Mahakamani pia Jaji anakuambia kuwa Serikali inaendelea na upelelezi. Je, ni kesi zipi za upelelezi wa muda mfupi na kesi zipi za upelelezi wa muda mrefu? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, kule Pemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watuhumiwa kuwekwa ndani muda mrefu na upelelezi kuchukua muda mrefu ningependa kwa niaba ya Serikali kutoa maelezo yafuatayo; kwanza mtuhumiwa akishakamatwa na polisi ndani ya masaa 24 anatakiwa kufikishwa Mahakamani, labda itokee mazingira ambayo siyo ya kawaida. Lakini katika mazingira ya kawaida masaa 24 apelekwe Mahakamani. Kwa hiyo, Watanzania wajue hilo na ukikuta kuna kituo kinaweka watuhumiwa kwa zaidi ya masaa 24 wengine sijui siku tatu/nne wajue ni uvunjaji wa sheria na waripoti. Hii nataka Watanzania wajue hivyo. (*Makofi*)

La pili, upelelezi kuchukua muda mrefu, kwanza Mahakamani uko utaratibu kwamba upelelezi lazima uchukue siku 60 kama baada ya siku 60 polisi hawana sababu yoyote waliyoitoa kwa Hakimu, Hakimu ana haki ya kuiondoa ile kesi Mahakamani. Lakini nataka vile vile Watanzania wajue kwamba Jeshi la Polisi sasa ili kuharakisha upelelezi, wapelelezi wote wa Wilaya, *OC- CIDs* kuanzia mwaka huu wa fedha wote watakuwa na magari ili arahishe upelelezi ndani ya Wilaya lakini Jeshi la Polisi tumewekea sasa maabara ya kisasa (*forensic laboratory)* ambayo ina zana za kisasa ambazo zitafanya upelelezi uchukue muda mfupi na wa hakika. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba hili la upelelezi kuchukua muda mrefu sasa Serikali imeshachukua hatua kamilifu. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, leo mambo Hoyee! Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, mtuhumiwa anapokamatwa analazima kuandika *statement* ikiwa hataki kuandika (*statement)*, maelezo yake atatoa Mahakamani inakuwaje? Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za sheria mtuhumiwa anawajika kutoa maelezo kwa jambo ambalo anatuhumiwa nalo. Ila tu ana hiari kwamba maelezo hayo anapenda ayatoe mbele akiwa na wakili wake au akina jamaa zake, huo uhuru anao kwamba haya maelezo sitaki kutoa nikiwa peke yangu, nataka nitoe mbele ya wakili wangu au mbele ya jamaa zangu huo uhuru anao. Lakini kutoa maelezo ni wajibu atoe maelezo ili hayo maelezo hayo ndiyo atakayompeleka huko Mahakamani. (*Makofi*)

Na. 259

**Bei ya Zao la Pamba**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu Na. 30 hapo tarehe 13 Aprili, 2005 ambalo nilitaka kujua mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia hadi mwezi huo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya ununuzi wa zao hilo ambao bado walikuwa hawajalipa tofauti ya bei kwa wakulima kama ilivyoagizwa na Serikali kufuatia kubadilika kwa bei katika soko la dunia na kwa kuwa Serikali ilisema kuwa hadi wakati huo ni Kampuni 9 tu kati ya Kampuni 34 zilikuwa zimelipa mapunjo hayo na kwamba ifikapo mwezi Machi, 2005 kampuni ambazo zitakuwa hazijalipa mapunjo hayo zitanyimwa leseni ya kununua pamba katika msimu ujao 2005/2006:-

(a) Je, ni Kampuni ngapi kwa majina ambazo hadi kufikia mwezi Machi, 2005 zilikuwa hazijalipa mapunjo ya bei kwa wakulima kama Serikali ilivyoelekeza?

(b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa dhidi ya kila mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Zoezi la kuwalipa wakulima tofauti ya bei kama ilivyoamriwa na Serikali kwa msimu wa 2004/2005 lilikumbwa na matatizo makubwa ya kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kuwalipa wakulima hao. Malinganisho ya takwimu zilizowasilishwa na Halmashauri za Wilaya na zile za wanunuzi wa pamba zilitofautiana sana na hivyo kusababisha malinganisho hayo kurudiwa na kuhakikiwa upya.

Zoezi la uhakiki wa takwimu lilibainisha kuwa kulikuwa na udanganyifu katika kiasi cha madai ya malipo ya mpunjo. Kutokana na utata huo wanunuzi wa pamba hawakuweza kuwalipa wakulima katika kipindi kilichotarajiwa.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2005 jumla ya wanunuzi 24 walikuwa hawajalipa mapunjo ya bei ya pamba kwa wakulima. Kwa kuwa orodha ya

wanunuzi hao ni ndefu na kwa kuzingatia Kanuni za Bunge lako Tukufu, kuhusu muda wa kujibu swali, orodha hiyo atapatiwa Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuifuatilia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ufuatiliaji wa ulipaji wa mapunjo unaonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 6 Julai, 2005 jumla ya wanunuzi 7 walikuwa wamelipa madeni yote ya mapunjo ya bei. Wanunuzi hao ni *SM Holdings, Afrisian, Cargill, Bibiti*, Gaki, Ushirombo na *KCCL.* Aidha jumla ya wanunuzi 17 walikuwa wamelipa sehemu ya madeni ambayo hayakuwa na utata na kubakiwa na sehemu ya madeni ambayo uhakiki wake unaendelea kufanyiwa utafiti. Jumla ya Shilingi 517,730,273 zimelipwa kwa wakulima kama mapunjo ya tofauti ya bei kwa wakulima katika kipindi hicho kati ya Shilingi 1,451,914,190 ambazo zinatakiwa kulipwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokuwepo kwa takwimu sahihi za malipo kwa wakulima kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali iliamua kutowafungia wanunuzi ambao walikuwa hawajalipa wakulima hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2005. Kufuatia kuanza kwa msimu wa kununua pamba wa 2005/2006 na baada ya kuzingatia maamuzi katika ngazi za Serikali za Wilaya na Mikoa, wanunuzi ambao wamelipa sehemu ya mapunjo wamepewa vibali na Serikali kuendelea kununua pamba wakati wanakamilisha taratibu za kumaliza kulipa mapunjo ya wakulima. Orodha ya wanunuzi hao pia atapatiwa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, pale ambapo Serikali za Wilaya na Mikoa zimeridhika na mikakati ya ulipaji wa mapunjo kwa wakulima kutoka kwa wanunuzi hao, ikiwemo kuwepo kwa uthibitisho wa ulipaji huo, Serikali za Wilaya na Mikoa zimetoa vibali kwa wanunuzi hao kuendelea kununua pamba msimu wa 2005/2006 ili wakulima wasiendelee kuteseka kwa kukosa mahali pa kuuza pamba yao. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanunuzi wanunuzi wa pamba hujipanga na kupanga bei ya kununua pamba kwa sababu wanafuatilia mwenendo wa bei katika soko la dunia. Lakini wakati huo huo wakulima ambao wanategemea Vyama vya Ushirika vina hali mbaya hawafanyi hivyo.

(a) Je, Serikali iko tayari kuchukua maamuzi ya kuvisaidia vyama vya Ushirika kwa kukamata wale waliofuja mali hizo na kuziuza na kuvifutia madeni vyama vya Ushirika ikiwemo Nyanza na *SHIRECU* na baadaye kuvipa ruzuku ili ziwasaidie wakulima ili wajipange nao kama wanunuzi wanavyofanya? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa bei ya sasa hivi wanunuzi wanaonunulia pamba Vijijini huko ni kati ya Shilingi 230 na 240 kwa kilo ya pamba ya mbegu, bei ambayo haikidhi hata gharama ya kuzalisha bei ya kilo ya pamba ambayo ni zaidi ya Shilingi 250. Je, Serikali inaweza ikasema hadi jana katika soko la dunia bei ya pamba ilikuwa Shilingi ngapi ili wakulima wajue wanapunjwa Shilingi ngapi? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la wanunuzi binafsi kujipanga utaratibu ambao tunauita kama (*cater*) kimsingi hairuhusiwi na si utaratibu ambao unaruhusiwa na Serikali. Kwa hiyo, kitendo hicho tu kwanza chenyewe si halali. Kwa hiyo, hata kama vyama vya Ushirika navyo vingekuwa na nguvu ya aina fulani haviruhusiwi vile vile kuunda haya magenge ambayo si halali.

Lakini Serikali kuvisaidia Vyama vya Ushirika ili viweze vikaingia katika ushindani ambao ni wa uhakika Serikali imeendelea kufanya hivyo kwa mfano wa Nyanza ambao ameutoa kwa mfano, Nyanza ilikuwa inadaiwa na wakulima fedha kiasi ambacho kilichosababisha kwamba Nyanza sasa isiweze kupata kibali cha kununua pamba.

Lakini kwa jitihada za Serikali pamoja na uongozi wa Nyanza hivi sasa Nyanza imeshapata kibali cha kupata mkopo kutoka *CRDB* kwa dhamana ya kwamba Nyanza ilikuwa inadai Bodi ya Pamba na kwa hiyo, msingi wa kupatia mkopo huo ilikuwa ni kwamba Serikali iweke dhamana kwa sababu bodi ya pamba ni chombo cha Serikali kwa hiyo, Serikali imewasaidia Nyanza kupata fedha za kununua pamba. Kwa hiyo, hivi ninavyosema kwamba utaratibu uko katika hatua za mwisho za kuwapatia fedha watu wa Nyanza. Utaratibu unaendelea hata katika vyama vingine vya Kanda ya Nyanza. (*Makofi*)

La pili, kuhusu bei, kama tulivyokuwa tukisema mara kwa mara kwamba suala la bei linabadilika katika soko la dunia na kama alivyokuwa amesema yeye mwenyewe kwamba bei ambayo ameitaja sasa ndiyo hiyo hiyo inayoendelea kule lakini hivi sasa siwezi nikasema kwa uhakika kwamba mpaka jana ilikuwa kiasi gani ili wakulima waweze kulinganisha, lakini bei inayoendelea sasa ni hiyo ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge na kusema kweli ndiyo hiyo iko katika mwelekeo wa bei ambayo inaendelea kwa hivi sasa. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Kampuni hizi zilifanya udanganyifu katika kununua mazao ya wananchi. Serikali itamke wazi humu ndani Bunge iseme haya Makampuni 17 ambayo bado hayajawalipa wananchi wetu huko kwa nini wasilipe deni na waongeze na riba juu zaidi? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la msingi kusema kweli madai hayo yanatokana na ile tofauti ya bei kati ya Shilingi 300 na 250 ambayo ilikuwa imetangazwa na *BEDIRA* lakini baadaye Serikali ikaingilia kati kwa hiyo ikaonekana kwamba ni tofauti. Kwa kusema kweli hakukuwa na udanganyifu. Nilichokizungumza hapa ni kwamba takwimu zilizokuwa zinawasilishwa sasa ili malipo hayo ya mapunjo yafanyike ndizo zilikuwa zinaonekana zina tofauti na tofauti yenyewe ilikuwa inatoka kwa wauzaji wenyewe wa pamba ambao ni wakulima pamoja na watu wengine. Kwa hiyo, kukawa na mabishano. Kwa hali hiyo haitegemewi kwamba katika njia hiyo kutakuwa na namna yoyote ya kwamba kuwe na riba kutokana na madai hayo ambayo wanadaiana wakulima na wanunuzi. (*Makofi*)

Na. 260

**Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

(a) Je, utata wa ki-mkataba uliojitokeza wa ujenzi wa barabara kati ya Dar es Salaam na Kibiti Wilayani Rufiji umepatiwa ufumbuzi gani?

(b) Je, Serikali inatoa maelezo gani ya uhakika ya kuwahakikishia wananchi wa Wilaya za Mkuranga na Rufiji na Watanzania kwa ujumla kwamba, sehemu ya barabara kati ya Kimanzichana na Kibiti itajengwa bila kusimamia?

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, kabla swali langu halijajibiwa naomba kufanya marekebisho madogo mstari wa pili kutoka mwisho kwenye sehemu (b) badala ya neno Kimanzichana isomeke Mkiu, kwa sababu barabara hiyo imeshajengwa sasa imefikia mpaka Mkiu.

**SPIKA:** Swali ulililoletewa lilisema Kimanzichana sasa sijui.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Ujenzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde naomba akubaliane na mimi sasa ama tulirudishe swali hili tukalifanyie kazi upya ama nilijibu kama lilivyokuwa awali kwamba Kimanzichana.

**SPIKA:** Wewe jibu kama ulivyoletewa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mbunge wa Rufiji lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa barabara ya DSM – Kibiti umekuwa ukifanywa kwa kutumia kikosi cha wataalam *(force account)* cha *TANROADS* na kusimamiwa na mhandisi mshauri *M/s Gauff Igenieure* kutoka Ujerumani na kufadhiliwa na Mfuko wa Kuwait. Kutokana na fedha kutotolewa kwa wakati utekelezaji wa mradi umekuwa na ucheleweshο mkubwa hadi kufikia hatua ya mradi kusimamishwa ilipofika mwezi Februari 2005 hadi hapo matatizo ya upatikanaji wa fedha yatakapotatuliwa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2005 Serikali imetuma barua rasmi kwa Mfuko wa Kuwait kuwafahamisha uamuzi uliotolea wa kuwa mradi huu sasa utatekeleza na kikosi cha Watalaam wa *TANROADS* na bila kusimamiwa na Kampuni ambayo mkataba wake na muda wake umekwisha. Aidha jumla ya Shilingi bilioni 5.75 za ndani zimetengwa kupitia Bajeti ya Serikali ya mwaka huu wa fedha 2005/2006. Fedha hizi zitatosha kukamilisha kilomita 45 zilizobakia bila kuhitaji fedha za nje kutoka mkopo wa Kuwait. Kwa uamuzi huu, fedha za mkopo kutoka Mfuko wa Kuwait zilizopangwa kukarabati barabara hii zitahamishiwa barabara ya Ndundu – Somanga zitakapopatikana.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuipongeza Serikali ya CCM kwa kuamua sasa kujenga barabara hiyo kwa fedha zetu wenyewe badala ya fedha za nje. Lakini nina swali moja kama ifuatavyo:-

Waziri wa Ujenzi wakati walipokuwa wanaweka jiwe la msingi katika moja ya barabara kule Biharamulo alisema kwamba “ifikapo mwisho wa mwaka 2006 mtu akisafiri kutoka Kampala mpaka Kagera, Mwanza, Shinyanga, Singida, Dodoma, Dar es Salaam hadi Mtwara atakuwa amepita kwenye barabara ya lami. Je, ni miujuza gani itatumika kujenga kwa lami na kukamilika ifikapo mwaka 2006 sehemu ya barabara kati ya Ndundu na Somanga ili watoto wetu wa Makonde, Wamakua na Wamwera waweze kuamini kauli hiyo ya Serikali? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi nimpongeze Mheshimiwa Bakari Mbonde kwa kufuatilia sana juu ya barabara hii na hasa akizingatia watoto wa Kimakonde, Kimakua wa Rufiji na Wamachinga kupita katika barabara hiyo. La pili haihitaji miujiza kutengeneza barabara hii kutoka Mwanza hadi Mtwara kwa lami, inahitaji uamuzi na usimamizi bora. Sisi Wizara ya Ujenzi nadhani tunao na tunaweza kufanya hivyo. (*Makofi*)

Na. 261

**Barabara ya Mtwara – *Mbamba Bay***

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME (K.n.y. MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, uamuzi wa kujenga barabara ya Mtwara – *Mbamba Bay* haipiti Barabara ya Nanyamba, Tandahimba, Newala hadi Masasi na kwa kuwa Serikali imesema kuwa barabara hiyo itaendelea kutengenezwa kwa kuchongwa tu ili ipitike hadi hapo fedha zitakapopatikana:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa matengenezo ya kuchonga chonga katika barabara hiyo kunaifanya barabara kuwa mto, yaani ardhi iko juu na barabara iko chini na kufanya barabara hiyo ipitike kwa shida wakati wa masika?

(b) Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais mwaka 1995 alikiri ubovu wa barabara hiyo wakati wa Kampeni huko Nanyamba. Je, kwa nini fedha za ndani zisitumike kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kabla ya mwaka 2006?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, ninapenda kwanza nitoe maelezo kama ifuatavyo: Barabara ya Mtwara – *Mbamba Bay* yenye urefu wa Kilometa 822, ni Barabara Kuu (*Trunk Road*) inayounganisha Mikoa ya Mtwara na Ruvuma. Aidha, sehemu ya barabara hiyo kutoka Mtwara kuptia Mingoyo hadi Masasi yenye urefu wa Km. 200 ni ya kiwango cha lami. Barabara ahii ni mojawapo ya miradi inayokusudiwa kutekelezwa chini ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor)*. Tayari barabara ya Mtwara – *Mbamba Bay* imekwisha kufanyiwa upembuzi yakinifu. Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu (km 211) ni barabara ya Mkoa (*Regional Road*) ambayo inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia

Ofisi ya Wakala wa Barabara Mtwara. Barabara hii huunganisha Wilaya zote nne za Mkoa wa Mtwara na Makao Makuu ya Mkoa. Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara huifanyia matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya dharura na ya sehemu korofi barabara hii kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*). Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara imefanya matengenezo yafuatayo kwenye barabara hii:-

(i) Matengenezo ya Kawaida katika kilometa 157 na kiasi cha shilingi milioni 115 zimetumika kugharimia matengenezo hayo.

(ii)Matengenezo ya muda maalum ya kilometa 6 katika barabara ya Masasi – Mpeta yamekamilika na kiasi cha shilingi milioni 90.072 zimetumika. Matengenezo katika kilometa 4 kati ya Mbawala na Ngorongoro kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 66.923 yanaendelea, hapa Mbawala siyo Mheshimiwa Mbawala, Mbawala jina la kijiji. Kazi ya kuweka tabaka jipya la lami Milima ya Nanyamba (km 3.6) na Namaleche (km 1.8) kwa gharama ya shilingi milioni 104.00 na kuweka lami kilometa 3.5 za barabara ya Masasi – Mpeta kwa gharama ya shilingi milioni 270 inaendelea kutekelezwa. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu imepanga katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 kufanya matengenezo katika sehemu ya Mangamba – Nanyamba chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Misaada la *NORAD*, kurejesha lami kwenye milima mikali ya Namaleche na Nanyamba, na kuweka lami nyepesi *(Otta Seal)* kilometa 3 kutoka Mpeta kuelekea Masasi kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Baada ya maelezo hayo, ninapenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika utangulizi, Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuitengeneza barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi ili iwe katika hali nzuri.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Serikali na ufinyu wa Bajeti, ni vigumu kwa sasa kuweza kuijenga barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala - Masasi (Km. 211) kwa kiwango cha lami ifikapo 2006. Kipaumbele hivi sasa ni ujenzi wa Barabara Kuu kwa kiwango cha lami. Gharama za kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami inakadiriwa kuwa kiasi kisichopungua shilingi bilioni 94.95.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa kuwa barabara inayozungumziwa ya Mtwara – Tandahimba – Newala ndiyo barabara inayounganisha Wilaya zote za Mkoa wa Wilaya. Lakini siyo hivyo tu barabara hiyo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Mtwara. Kwa kuwa kuna barabara ya lami kutoka Mtwara kupitia Mingoyo kwenda Masasi na barabara ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi inapitia Mingoyo, hivi Serikali ina utata gani wa ile barabara ya *Mbamba Bay* ambayo inahusisha *Mtwara Corridor Development Plan* kwa nini isipitie sasa Tandahimba kwenda Masasi kwa sababu barabara ya Masasi – Mingoyo kuna lami tayari. Kwa nini isipitie kule Barabara ya *Mtwara Corridor* ambayo inakwenda *Mbamba Bay?* (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la awali na wakati tukieleza kwamba umuhimu wa kwanza wa barabara kutia lami tunatilia barabara kuu *(Ttrunk Roads*) baadaye ndiyo tufuatie *Regional Roads* vile vile barabara ya kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay* sisi wenyewe hatuna uwezo wa kutumia fedha zetu kutengeneza barabara hii tunasaidia hata ile *Feasibility Study* tumesaidia na Wajapan. Kwa mantiki hiyo, Wajapan hawatakubali upitishe barabara sehemu ambayo siyo *Trunk Roads.* Hii ni misaada mara nyingine ukubali na masharti yake, masharti haya sisi tulionao na mazuri tu kwamba tutengeneze *Trunk Road* ya Km 822 ambayo inatoka Mtwara hadi Masasi – *Mbamba Bay.* Huo msingi mmojawapo. Msingi wa pili ni ule ule kwamba wakati wewe unalilia huna kiatu mwenzako mwingine anasema hana mguu. Kwa hiyo, ni vizuri wale waliopata lami wastahimili wakangojea lami tuipitishe kwenye *trunk roads* halafu tutakuja kwenye *rural road*s.

Na. 262

**Mahitaji Umeme – Nzega**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:

Kwa kuwa mara kwa mara wananchi wa Nzega wametoa kilio chao wakiomba kupatiwa umeme katika miji midogo ya Puge, Ndala na Bukene:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinatakiwa ili kuunganisha umeme katika vijiji hivyo?

(b) Je, ni lini wananchi wa Nzega wataondokana na matumizi ya koroboi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Vijiji vya Puge, Ndala na Bukene vimeingizwa katika mradi wa kupeleka umeme vijijini ujulikanao kama *Energizing Rural Transformation* utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia na unategemewa kuanza mwaka wa fedha huu lakini hususan mwakani 2006 baada ya kukamilika kwa makubaliano na Benki ya Dunia. Gharama za utekelezaji wa miradi katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni kama ifuatavyo:-Puge na Ndala ni Tshs bilioni 1,100. Bukene ni Tshs 842 milioni

(b) Wananchi wa Nzega wataanza kutumia umeme mara mradi nilioutaja wa kupeleka umeme vijijini hivyo utakapo kamilika, kama nilivyosema awali tunatarajia kwamba mradi huo utaanza mwakani 2006.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pia namshukuru Naibu Waziri na Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo wametekeleza ahadi hii ahsanteni sana. Kwa kuwa kwenda Puge mpaka Ndala kuna

Vijiji ambavyo viko maeneo ya katikati, je, navyo vimeingizwa kupata umeme kama Kijiji cha Nkiniziwa, Puge yenyewe, Utwigu, Itiro na kadhalika.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida katika suala zima la usambazaji umeme baina ya kijiji kikubwa na kijiji kingine kikubwa kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, wasambazaji wa umeme shirika letu la Ugavi nchini *TANESCO* hupendelea kuhakikisha kwamba wanapata wateja wengi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, wale ambao wako katika njia inayopita umeme na mahali ambapo wapo wateja wa kuweza kuwaunganishia, basi *TANESCO* hufanya hivyo.

Kuhusu vijiji mahsusi ambavyo amevitaja, nadhani itabidi kutazama katika ratiba ambayo ipo ya utekelezaji. Lakini mimi nina hakika kuwa uzoefu wa *TANESCO* wanavyofanya katika suala la usambazaji hawawezi kuacha kijiji ambacho katikati yake kuna biashara ya kuweza kupatikana kwa upande wao.

Na. 263

**Umeme Utokanao na Makaa ya Mawe Mchuchuma**

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya Kampuni ya *BP Power* ya Afrika Kusini ya mwezi Aprili, 2004 iliyowasilishwa *NDC* na nakala kupelekwa Serikalini imeonyesha kuwa mpango wa usambazaji wa umeme kwa Tanzania kwa miaka 2 ijayo ambao ni wa bei nafuu na wa uhakika ni wa makaa ya mawe ya Mchuchuma.

(a) Je, ni kitu gani kinachoifanya Serikali kusita kukubali mwelekeo huo?

(b) Je, kuna hazina ya makaa ya mawe kiasi gani katika nchi hii na yanaweza kuzalisha umeme kiasi gani na kwa miaka mingapi ijayo?

(c) Je, inawezekana Tanzania kuwa mzalishaji na muuzaji wa umeme katika nchi za *SADC* na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la kuandaa mpango wa kuendeleza sekta ya umeme ni la Wizara ya Nishati na Madini. Kampuni ya *BP Power* ya Afrika Kusini iliagizwa na *NDC* kufanya upembuzi yakinifu wa kuungnaisha kituo cha kuzalisha umeme cha Mchuchuma kwenye gridi ya Taifa. Wataalam wa Wizara ya Nishati na Madini na

*TANESCO* walipitia ripoti ya Mshauri ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa inatofautiana na *Power System Master Plan* ya Serikali kutokana na Mshauri kutumia vigezo tofauti pamoja na njia za utafiti ambazo hazikidhi matakwa ya sekta ya umeme. Maoni ya Wizara ya Nishati na Madini yakijumuishwa na maoni ya *TANESCO* yalitumwa kwa Mshauri tangu tarehe 15 Juni, 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kwamba, hazina ya makaa ya mawe hapa Tanzania iko Songwe – Kiwira Mkoani Mbeya na Mchuchuma Katewaka katika Mkoa wa Iringa Wilayani Ludewa. Hazina hiyo inakadiriwa kuwa tani bilioni mbili na iliyothibitishwa, Mchuchuma pekee ni tani milioni 125. Kiasi cha makaa wa tani milioni 30 kinatosha kuzalisha umeme wa Megawati 400 hapo Mchuchuma kwa muda wa miaka 20.

Makaa ya mawe yanayotumika kwa sasa ni yale ya Songwe Kiwira ambako kuna mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati sita. Ilikadiriwa kuwa tani 150,000 zingetumika kwa mwaka lakini kutokana na hali duni ya uzalishaji wa mkaa huo uzalishaji umepungua hadi kufikia tani 96,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 1992.

(c) Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa Tanzania kuwa mzalishaji na muuzaji wa umeme katika nchi za *SAPP (Southern Africa Power Pool)* na *EAPP (East Africa Power Pool)* baada ya kukamilika mradi wa *Interconnector* kati yetu na nchi za Zambia na Kenya.Ushiriki katika swoko la biashara ya umeme ndio nguzo ya ushirikiano kati yetu na nchi za Afrika Mashariki pamoja na *SADC* *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Muda wa Maswali umekwisha, lakini muda wa mwongozo upo.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA**: Mheshimiwa Spika, jibu alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni la swali lingine kabisa ambalo sikuuliza. Jibu alilotoa ni la swali langu la wiki mbili zilizopita. Naomba atoe jibu la swali la leo. *(Kicheko/Kicheko)*

**SPIKA:** Basi kwa tatizo hilo kwa kuwa muda wa maswali umekwisha, tutalitafutia nafasi nyingine. Huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu jamani. *(Kicheko)*
Matangazo, kuna Kamati moja imepangiwa kufanya kikao leo nayo ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake anaomba Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane saa 5 asubuhi chumba Na. 231. Hakuna matangazo zaidi, endelea na *Order Paper.*

## HOZA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2005/2006
### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita 2004/2005 kumekuwepo na matukio mengi ya misiba iliyotugusa wote. Kwa hiyo napenda, kwanza, kutoa pole kwa familia na wananchi wa Majimbo yote ya uchaguzi ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzetu wamekwishaitwa mbele ya haki. Pili, kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopatwa na misiba mwaka uliopita. Mwenyezi Mungu aendelee kuziweka Roho za Marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, tunapohitimisha mwaka wa mwisho wa Uongozi wa Awamu ya Tatu, wa Taifa letu, na mkutano wa mwisho wa Bunge lako Tukufu kwa kipindi hiki, ni muhimu kutoa shukrani chache. Kwanza, kwa Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuhitimisha awamu hii salama, nchi yetu ikiwa na amani na utulivu. Pili, kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wakuu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Waziri Mkuu Frederick Tluway Sumaye - Mbunge, kwa uongozi wao imara wenye mafanikio makubwa katika awamu hii. Tatu, kukushukuru na kukupongeza sana wewe Mheshimiwa Spika Pius Msekwa, Mheshimiwa Naibu Spika, Juma J. Akukweti - Mbunge, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Eliachim J. Simpassa - Mbunge na Anne S. Makinda - Mbunge, kwa uongozi uliotukuka wa shughuli za Bunge katika kipindi cha uongozi wenu. Uongozi wenu umeimarisha heshima ya Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa kwamba mafanikio ya awamu ya tatu yataendelezwa na uongozi wa awamu ya nne. Kwa msingi huo napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza wagombea wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, walioteuliwa na Vyama vyao vya Siasa, hususan wale wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete (kwa nafasi ya u-Rais), Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein (Mgombea Mwenza) na Mheshimiwa Amani Abeid Karume (nafasi ya u-Rais Zanzibar). Hawa ni hakika wataendeleza mafanikio ya awamu ya tatu kwa sababu wote walikuwemo katika timu ya uongozi ya awamu hiyo. Nawatakia ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikirejea kwenye mawasilisho ya Bajeti ya Wizara yangu, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Eliakim Simpassa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, na Waheshimiwa Wabunge wote Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa ushirikiano wao na uchambuzi wao makini wa Bajeti ya Wizara yangu. Kwa kipindi chote cha uhai wa Kamati hii, Wizara yangu imefaidika sana na ushauri, maoni na maelekezo ya Kamati hii. Imefanya kazi nzuri sana. Tunawashukuru na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, Bunge lako tukufu limekwisha pokea na kuzingatia misingi ya jumla ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006,

hususan kupitia hotuba za Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Nawashukuru na kuwapongeza kwa hotuba zao nzuri na zenye matumaini makubwa. Kufuatia misingi hiyo ya jumla, Hoja yangu itajielekeza mahsusi katika kuainisha malengo na mikakati ya utekelezaji katika Sekta ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yameendelea kuwa yale yale ya kusimamia Sera na Sheria za Ardhi zinazohusu utoaji, uhifadhi na utumiaji endelevu wa ardhi nchini, uendelezaji makazi endelevu Mijini na Vijijini; upimaji wa ardhi na utayarishaji wa ramani; upimaji na uhifadhi wa alama za mipaka kati ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo; kutafsiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya ki – utawala (Kama vile Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji) ndani ya nchi yetu; na mwisho kuwaendeleza kitaaluma na Ki – utumishi wafanyakazi wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara yangu imepata mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoja na:- Kuandaa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, kutunga Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999, Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya Mwaka 2002 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2004. Kazi hiyo imeenda sambamba na utayarishaji wa kanuni zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa na Sera na Sheria hizi, Wizara yangu imejikita sasa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwamilikisha ardhi kwa madhumuni ya kupata mitaji kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 51 ya Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi katika miaka 2000 – 2010 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2000. Wizara imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma ilitolewa katika Wilaya zote kuwawezesha wananchi kuelewa na kutambua umuhimu wa ardhi, haki na wajibu wao juu ya ardhi kwa mujibu wa Sheria hizo. Sambamba na kutoa elimu kwa umma, vitabu vya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya Mwaka 1999, Sheria ya Mahakama ya Ardhi Na.2 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake zilisambazwa kwa Watumishi wa Sekta ya Ardhi, Viongozi wa Mikoa, Watendaji wa Kata, Serikali za Vijiji, Ofisi mbalimbali za Serikali na Asasi zisizo za kiserikali. Nakala zaidi ya 40,000 za Sheria, Kanuni na Miongozo zimesambazwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Wizara yangu ya Ardhi imeweza kutatua tatizo sugu la ukosefu wa viwanja hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Wizara imeweza kupima viwanja 30,655 ambavyo vimeweza kugawiwa kwa wananchi kwa utaratibu ulio wazi na wa ufanisi kwa wananchi kuchangia gharama za upimaji. Wananchi wanaendelea na ujenzi. Kuwepo kwa viwanja vingi kwa wakati mmoja kumeondoa mianya ya rushwa katika mchakato mzima wa ugawaji wa viwanja, vilevile utapunguza ujenzi holela katika miji yetu kwa kiwango kikubwa. Mradi huu wa upimaji viwanja vingi kwa wakati mmoja unaendelea kutekelezwa katika miji mingine. Sambamba na upimaji viwanja, Wizara imeweka mkakati maalum wa kuandaa hati za kumiliki ardhi kwa wamiliki ambao kwa miaka mingi walishindwa kupata hati zao. Ni matarajio ya

Wizara kuwa baada ya wananchi hao kuzipata Hatimiliki watazitumia hati hizo kujipatia mtaji.

Mheshimiwa Spika, kwa asilimia 70 ya Watanzania, ardhi ni rasilimali pekee na ya msingi waliyonayo. Hivyo, ili kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), ni budi kumwezesha mwananchi kuitumia rasilimali ardhi kupata mtaji. Hili litawekezakana tu iwapo wananchi vijijini watapatiwa hati ya kumiliki ardhi kimila. Wizara kwa kutumia Sheria ya Ardhi ya Vijiji, imeweka utaratibu utakaowawezesha wananchi kupata hati ya kumiliki ardhi kimila. Utaratibu huo unaanza na upimaji mipaka ya vijiji, kutambua mipaka ya maeneo ya wanakijiji, kutoa cheti cha kijiji, kujenga masjala za ardhi za Wilaya na Kijiji, kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Ardhi kwa Halmashauri ya Kijiji na wananchi wote kijijini na hatimaye kutoa hati ya kumiliki ardhi kimila.

Hadi sasa, jumla ya Vijiji 6,800 vimepimwa nchi nzima na Wizara imeanza utekelezaji kwa kuchagua wilaya mbili za mfano nchini ambazo mchakato ulioelezwa hapo juu umetekelezwa. Hadi sasa, wananchi 434 wamepatiwa hati zao na utekelezaji unaendelea. Kwa kupata hati miliki za kimila wananchi vijijini wanapata fursa ya kurasimishiwa ardhi zao hivyo kuweza kuzitumia miliki hizo kupata mitaji. Mpaka sasa baadhi ya wanavijiji wamefanikiwa kupata mikopo ya Benki kwa kutumia hati hizo. Utaratibu huu ni mafanikio makubwa kwa Serikali ya awamu ya tatu. Hati ya kumiliki ardhi ni mkombozi mkubwa katika kuondokana na umaskini iwapo wananchi watakuwa tayari kuzitumia kupata mitaji.

Mheshimiwa Spika, wakati asilimia 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na kutegemea ardhi kama rasilimali ya msingi, asilimia 70 ya Watanzania waishio mijini huishi katika maeneo yasiyopimwa. Wengi wa wananchi hawa wanazo rasilimali kubwa na zenye thamani kubwa katika maeneo hayo. Kwa kuwa rasilimali hizi (nyumba) zipo katika maeneo yasiyopimwa ni mtaji mfu, wenye nazo hawawezi kuzitumia kupata mitaji kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. Wizara yangu kwa kutumia Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999 imeweka mkakati wa kurasimisha makazi hayo. Mkakati huo umeanza kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2004/2005, makazi 200,000 yametambuliwa na utoaji wa leseni unaendelea. Kwa kutoa leseni ya makazi, rasilimali hizi sasa zinaingizwa katika mfumo rasmi (kurasimishwa). Baada ya urasimishaji, wenye rasilimali hizo wanaweza kuzitumia kupata mitaji. Hili si jambo dogo kwa nchi yetu. Kwa kuchukua hatua hii, mizania ya uchumi wetu itabadilika sana hasa ikizingatiwa kuwa rasilimali zilizoko huko ni asilimia 70 ikilinganishwa na zilizo katika maeneo yaliyopimwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya awamu ya tatu ni kuimarisha ukusanyaji kodi hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Wizara ya Ardhi ilipewa jukumu la kukusanya kodi ya pango la Ardhi tangu mwaka 1995/96 kwa kushirikiana na Halmashauri zote. Wakati Wizara inapokea jukumu hilo Serikali ilikuwa inakusanya wastani wa Shilingi 236,000,000 kwa mwaka. Baada ya Wizara

kuanza kukusanya, kiwango hicho kimekuwa kikiongezeka kila mwaka hadi kufikia jumla ya Shilingi 7,148,797,217 katika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Mahakama za Ardhi ya Mwaka 2002, Wizara imeunda Mabaraza 23 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, moja kwa kila Mkoa isipokuwa matatu ni katika Mkoa wa Dar es Salaam (moja kwa kila wilaya). Mabaraza yote yameanza kufanya kazi. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaendelea kufufua Mabaraza ya Kata na kuunda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi hiyo, inatoa mafunzo ili kuhakikisha kuwa Mabaraza hayo yanaundwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Wananchi sasa wanaweza kutatua migogoro yao pale walipo bila kulazimika kufanya safari ndefu. Hatua hizi zinaimarisha usalama wa miliki zao na amani katika vijiji vyao, hivyo kuruhusu muda mwingi zaidi utumike katika shughuli za kiuchumi ili kupunguza umasikini. *(Makofi)*

. Mheshimiwa Spika, katika miaka kumi iliyopita Wizara imefanikiwa kuweka mfumo madhubuti, rahisi na wazi wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya ardhi kwa kutumia teknolojia ya kompyuta katika uandaaji, utunzaji wa kumbukumbu, kutoa taarifa na mawasiliano kwa ujumla. Wizara inaweza kutoa barua ya toleo katika muda wa dakika tano baada ya malipo kufanywa, kutoa hati ya kumiliki ardhi katika kipindi cha miezi miwili ikilinganishwa na muda wa zaidi ya miaka kumi katika kipindi kilichopita. Huduma nyingine kama vile, kutoa vibali vya uwekaji rehani, usajili wa nyaraka mbalimbali nazo zinatolewa katika muda mfupi zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Mfumo huu umeiwezesha Wizara kutoa huduma kwa ufanisi na uwazi hivyo kupunguza kero kwa wananchi, kudhibiti mianya ya RUSHWA, kuongeza mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi yake kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya tatu imejitahidi kwa nguvu zote kuimarisha usalama na amani na nchi jirani zetu. Tanzania inapakana na nchi kumi zikiwemo Seychelles, Comoro, Msumbiji, Malawi, Zambia, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi cha miaka 10, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara yangu ilichukua hatua za kuhakiki mipaka hiyo na kutoa tafsiri na ufumbuzi pale palipohitajika kufanya hivyo. Uhakiki huu wa mipaka ya kimataifa umechangia sana katika kudumisha usalama na amani mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ramani za msingi za miji ni muhimu katika kupanga matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na huduma za jamii. Katika kipindi cha miaka kumi, Wizara yangu ilibuni na kutekeleza Mpango wa Taifa wa utayarishaji wa ramani nchini na kufanikiwa kupiga picha za anga za miji 85 na kukamilisha ramani zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi imebuni na kutoa elimu ya kutekeleza dhana ya Mipango Shirikishi ya Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini. Miongozo ya Mipango Shirikishi imesambazwa vijijini na wananchi wanaitumia kupanga matumizi ya ardhi yao. Vijiji vilivyozingatia mipango hii, vimeweza kupunguza migogoro, kuhifadhi mazingira na kuongeza uzalishaji.

. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya nyumba nyingi za kuishi mijini na vijijini ni duni na gharama za ujenzi wa nyumba hupanda mara kwa mara, Wizara ililazimika kuboresha kituo chake cha Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi kwa kukibadilisha kuwa Wakala. Wakala unatoa matokeo ya tafiti mbalimbali ya vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu pamoja na teknolojia rahisi za ujenzi ambazo matumizi yake yameenea kwa wananchi walio wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanywa, Wizara yangu imeweza kupata kombe la ushindi katika maonyesho ya Siku ya Utumishi wa Umma iliyofikia kilele tarehe 23 Juni mwaka huu. Nawapongeza sana watumishi wote wa Wizara kwa ushindi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 5,896,650,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ambavyo ni pamoja na kodi ya pango la ardhi, usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria, uuzaji wa ramani, picha za anga na uchapishaji wa nyaraka na ada za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba. Hadi kufikia Juni, 2005 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 7,148,797,217 ikiwa ni asilimia 121 ya lengo

Mheshimiwa Spika, Wizara iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 5,690,672,400 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, Shilingi 1,670,195,800 ilikuwa kwa ajili ya mishahara, na Shilingi 4,045,060,300 kwa matumizi mengineyo *(Other Charges: OC).* Hadi kufikia Juni, 2005 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 4,045,060,300 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, miradi ya maendeleo iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 673,000,000. Hadi kufikia Juni, 2005, Wizara imepokea kiasi cha Shilingi 650,000,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara iliendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi zenye misingi na lengo la kuimarisha utawala bora ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini. Huduma hizo ni pamoja na kutoa miliki za ardhi, utwaaji ardhi kwa manufaa ya umma; utatuzi wa migogoro ya ardhi; usajili wa hatimiliki pamoja na nyaraka mbalimbali; kutoa vibali vya uwekaji rehani, hakimiliki za ardhi na uhamisho wa miliki; uthamini wa mali; na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria Mpya za Ardhi. Pia, Wizara ilichapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali kwa ajili ya umilikishaji ardhi kwenye Halmashauri. Pamoja na kutoa

huduma hizo, Wizara iliendelea na ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara ilitwaa ardhi na kubatilisha miliki kwa ajili ya kuwezesha matumizi endelevu ya ardhi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Tanga na Ruvuma. Aidha, jumla ya miliki za viwanja na mashamba 125 zimebatilishwa na kumilikishwa kwa waombaji wapya. Kama nilivyowahi kueleza katika kipindi kilichopita, ili kutekeleza Sheria Mpya za Ardhi, madaraka ya kugawa ardhi yamekasimiwa kwa Halmashauri. Wizara inaendelea na jukumu la kushughulikia maombi ya viwanja kwa ajili ya Balozi mbalimbali, maeneo ya uwekezaji chini ya Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre – TIC)* na maeneo ambayo matumizi yake ni ya manufaa kwa Taifa kama viwanja vya ndege, migodi, mahoteli na fukwe.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ugawaji Ardhi ulifanywa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma na hivyo kufanya jumla ya Halmashauri zenye Kamati za Kugawa Ardhi kuwa 106. Mbali na wilaya mpya kama vile Mvomero, Kilolo, Namtumbo, Kilindi na Sikonge, Halmashauri kongwe za Mji wa Lindi, Halmashauri za Wilaya za Nachingwea, Chunya, Kisarawe, Mpanda, Nkasi na Ruangwa hazijawasilisha majina ya wajumbe wa Kamati hizo. Natoa wito kwa Halmashauri hizo zifanye hivyo ili ziweze kutekeleza jukumu la kugawa ardhi kwa mujibu wa sheria. Pia, ikumbukwe kuwa, usimamizi na uendeshaji wa masuala ya ardhi unahitaji utaalam. Hadi sasa, bado kuna upungufu mkubwa wa maafisa wa sekta ya Ardhi katika Halmashauri. Mathalani, Halmashauri zipatazo 40 hazina Maafisa Ardhi Wateule wa kusaini nyaraka mbalimbali za kumilikisha ardhi kulingana na sheria za ardhi. Hivyo, nazidi kusisitiza kuwa Halmashauri zote nchini zihakikishe zinaajiri Maafisa Ardhi wenye sifa zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jukumu lake la kusaini na kusajili hati miliki za ardhi zilizowasilishwa kutoka Halmashauri mbalimbali na ambazo zimetayarishwa Wizarani. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya hati 6,529 zilisainiwa na kati ya hizo, 3,393 zilitoka Halmashauri na 3,136 ziliandaliwa Wizarani. (Jedwali Na. 3). Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara imeshughulikia utatuzi wa migogoro mbalimbali ya ardhi nchini. Katika Mkoa wa Dar es Salaam, uhakiki wa miliki za viwanja uliendelea katika maeneo ya Tegeta, Mbezi na Tabata kwa lengo la kujenga hazina ya kumbukumbu sahihi za miliki za Ardhi. Pia, maeneo yenye migogoro sugu ya ardhi na umiliki katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Arusha, Pwani, Lindi na Mwanza yalikaguliwa na katika mwaka huu wa fedha Mikoa ya Mara, Mtwara, Mbeya na Tabora itakaguliwa.

Wizara imeboresha utatuzi wa migogoro kwa kujenga kumbukumbu sahihi za miliki za ardhi, na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika michakato mbalimbali ya utoaji huduma. Hata hivyo, utafiti umeonyesha kuwa chanzo kimojawapo cha migogoro mingi ya viwanja na mashamba ni kutokana na wananchi kuhodhi ardhi bila kuiendeleza. Natoa wito kwa wamiliki wa ardhi kuzingatia masharti ya uendelezaji ili kuepuka

migogoro na uvamizi wa ardhi iliyomilikishwa. Aidha, nasisitiza Halmashauri zote nchini ziboreshe utunzaji wa kumbukumbu kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara imeweza kushughulikia kazi za usajili wa hati miliki na nyaraka za kisheria zipatazo 13,874. Kati ya hizo, zimesajiliwa hati miliki za ardhi 5,464 na nyaraka 8,410 mbalimbali za kisheria. Pia, Wizara imekamilisha utoaji na usajili wa vibali 2,633 vya uhamisho wa miliki na uwekaji rehani wa hati na haki za kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara yangu kuzindua utoaji na usajili wa vyeti vya ardhi ya kijiji na hatimiliki za kimila katika ngazi ya wilaya na vijiji katika kijiji cha Halungu wilayani Mbozi mwaka jana, utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji na ujenzi wa masjala za mfano ngazi ya wilaya na kijiji umeendelea katika wilaya mbalimbali nchini. Hadi mwezi Juni, 2005 masjala mbili za mfano zimejengwa na vyeti vya vijiji 102 vimetolewa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni 2005, Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 144,350,652.10 sawa na asilimia 44 zaidi ya lengo kutokana na ada ya uthamini wa mali na nyumba zipatazo 2,655 ikilinganishwa na lengo la kukusanya Shilingi 100,000,000. Kwa mwaka 2005/06, Wizara imepanga kukusanya ada ya Shilingi 150,000,000 kutokana na uthamini wa nyumba na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, Wizara yangu ilikuwa na jukumu la kuanzisha "*Valuation Data Bank*" kwa lengo la kuwezesha uthamini wa mali mbalimbali kufanyika kulingana na bei ya soko ya mali zinazofanana. Hadi kufikia mwezi Juni, 2005 takwimu 10,200 za viwango vya thamani ya ardhi na majengo katika soko *(valuation market rates)* zimeingizwa kwenye kompyuta. Wizara yangu imepanga kuendelea na kazi hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 kwa lengo la kujenga viwango vya bei ya soko kwa kila aina ya nyumba. Baada ya kukamilisha zoezi hili, kijitabu kitachapishwa na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini ili kitumike na wathamini kama kiongozi cha kazi.

. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na jukumu la kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria Mpya za Ardhi katika mwaka wa fedha 2004/2005 kwa kutumia njia mbalimbali hususan vyombo vya habari, semina na mikutano. Elimu hiyo ilitolewa kwa viongozi, watendaji na wananchi katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Jumla ya wadau 6,950 walifundishwa Sheria hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, nakala 2,926 za vitabu vya sheria hizo na Kanuni zake na nakala 3,026 za Mwongozo wa Kufundishia Sheria hizo zilisambazwa. Pia, Wizara ilishiriki katika sherehe za Sabasaba na Nanenane ambako maelezo ya Sheria hizo yalitolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu juu ya mkakati wa Wizara yangu kuanzisha mifumo ya kuhifadhi kumbukumbu kwa kutumia kompyuta kama njia maridhawa ambayo itarahisisha utendaji kazi za kila siku na kuboresha huduma kwa wananchi. Wizara yangu imeendelea na uboreshaji wa mifumo ya kumilikisha Ardhi, kufuatilia mienendo ya barua za wananchi na majalada ya viwanja,

kukadiria kodi ya pango la ardhi, kufanya upekuzi wa hati katika ofisi ya Msajili wa Hati na kumbukumbu za upimaji *(Survey Registration System).* Katika kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na Ofisi zake zilizoko Mikoani, mtandao wa mawasiliano ya ndani *(Local Area Network - LAN)* umewekwa katika Ofisi ya Usajili wa Hati Kanda ya Kati (Dodoma). Hivi sasa mawasiliano kati ya Wizara na ofisi za Usajili wa Hati za Kanda za Moshi, Mwanza, Mbeya na Dodoma yamerahisishwa kutokana na uanzishwaji wa tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni 2005, jumla ya kumbukumbu za majalada 152,826 ya wamiliki wa viwanja na mashamba pamoja na taarifa za wamiliki wa viwanja wapatao 56,710 wametambuliwa na kumbukumbu zake kuhifadhiwa kwenye kompyuta. Kumbukumbu za hati katika ofisi za Kanda za Dodoma, Mbeya, Dar es Salaam, Moshi, Mwanza na Mtwara zimeendelea kutambuliwa. Hadi sasa, jumla ya hati 102,100 zimetambuliwa na zinaendelea kuingizwa katika kompyuta. Taarifa za kumbukumbu za upimaji wa viwanja 456,710 nchi nzima zimekamilika na kuingizwa katika kompyuta. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itaendelea na mpango wa kujenga mitandao ya mawasiliano ya ndani katika Ofisi za Usajili wa Hati za Kanda, kutambua viwanja vilivyopimwa na wamiliki wake katika mikoa ya Mwanza na Morogoro kwa lengo la kupanua hazina ya kumbukumbu na wigo wa makusanyo ya kodi ya pango la ardhi. *(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara iliahidi kuunda Mabaraza 23 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mabaraza 23 yameundwa moja katika kila mkoa, matatu kati ya hayo katika mkoa wa Dar es Salaam na Wenyeviti 22 wa Mabaraza hayo wameteuliwa. Pia, mwongozo wa kutoa elimu juu ya Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002 umekamilika. Nakala 1,800 za Mwongozo zimesambazwa katika Halmashauri mbalimbali. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kuchapisha nakala zaidi, kusambaza na kutoa elimu kwa wananchi na watendaji wa Wilaya, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mabaraza ya Nyumba na Mabaraza ya Usuluhishi ya Ardhi ya Mikoa yaliyopo yaliendelea kusikiliza na kuamua mashauri yaliyokuwa yamefunguliwa. Jumla ya mashauri 551 ya nyumba na 1,465 ya usuluhishi wa ardhi yaliamuliwa. Mashauri 28 ya nyumba na 211 ya usuluhishi wa ardhi yaliyobaki yatasikilizwa na kutolewa hukumu ifikapo tarehe 30 Septemba 2005. Hivyo, hadi kumalizika kwa kipindi cha mpito cha miaka miwili hapo tarehe 30 Septemba 2005, Mabaraza ya Nyumba na Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi yatakuwa yamekamilisha kazi zake. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005 jumla ya maombi 1,896 yamefunguliwa katika Mabaraza mapya ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na kati ya hayo maombi 366 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara inatarajia kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya saba zitakazobainika kuwa na migogoro mingi. Hii itapunguza kero kwa wananchi wanaolazimika kusafiri hadi makao makuu ya mkoa kufungua kesi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kujenga uwezo wa matumizi ya teknolojia ya kisasa katika Upimaji na Utayarishaji wa Ramani na Upimaji Majini *(*

*hydrographic survey).* Lengo ni kuongeza tija katika upimaji na ramani ili kuwezesha usimamizi na uendeshaji wa shughuli nzima za kumilikisha ardhi, kutatua migogoro, upangaji matumizi ya ardhi na hifadhi ya mazingira. Ramani za msingi za nchi ni nyenzo muhimu katika Ujenzi wa Kumbukumbu na Takwimu za *Taifa (Development of a National Spatial and Statistical Data Infrastructure).* Mfumo huu huonyesha raslimali na miundombinu iliyojengwa tayari na hivyo kuwezesha kubuni, kuamua, kupanga, kutekeleza na kuratibu mipango mingine ya maendeleo ya Taifa katika sekta zote kwa ufanisi na uhakika wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ingeanza utayarishaji wa ramani za msingi za miji 38 katika Kanda ya Ziwa Victoria kwa kutumia picha za anga zilizopigwa mwaka 2003 na kupiga picha za anga miji 30 katika Kanda ya Magharibi, Mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa, Iringa na Mbeya. Pia, Wizara yangu ilitarajia kutumia picha za anga za juu (*satellite imagery) katika* utambuzi wa vipande vya ardhi, utayarishaji na uhuishaji wa ramani. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upimaji picha *(photo control)* kwa ajili ya utayarishaji wa ramani za msingi za miji 38 umefanyika. Uchoraji wa ramani za msingi za miji minane umekamilika na uchoraji wa miji mingine utaendelea katika mwaka huu wa fedha. Miji 36, badala ya 30, katika Kanda ya Magharibi imepigwa picha. Jiji la Mwanza lilipigwa picha kwa ajili ya kufanikisha Mradi wa Kupima Viwanja 3,500 kwa utaratibu uliotumika kwenye Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Picha za *satellite* za eneo la kati ya Jiji la Dar es Salaam zilinunuliwa na kutumiwa kwa kutambua miliki katika makazi yasiyopangwa. Picha hizo zitatumiwa pia kuhuisha ramani za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina jumla ya ramani 1,264 katika skeli ya 1:50,000, ambazo huonyesha sura ya nchi vijijini na mijini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ramani 1,000 kati ya 1,264 zimeingizwa katika kompyuta ili ziweze kuhuishwa na kutumiwa kikamilifu kwa teknolojia za kisasa. Kazi hii imefanyika kupitia kituo chetu cha Kanda, *(Regional Centre for Mapping of Resources for Development - RCMRD)* kilichopo Nairobi. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu inatarajia kukamilisha uingizaji wa ramani zote za nchi za skeli ya 1:50,000 katika kompyuta, kukamilisha kuchora ramani za msingi za miji 38 katika Kanda ya Ziwa Victoria, kufanya *ground photo control* ya picha za miji 35 katika Kanda ya Magharibi na kuongeza uwezo wa kutayarisha ramani kwa kompyuta na hivyo kuongeza kasi ya upatikanaji wa ramani mpya na uhuishaji wa zile za zamani.

Mheshimiwa Spika, Wizara inalo jukumu la kutayarisha ramani ya maeneo ya nchi yaliyoko chini ya bahari na maziwa. Hadi sasa haijawezekana kupata vifaa vya msingi na wataalam wa kutosha kutokana na gharama kubwa inayohitajika. Kutokana na hali hiyo, inabidi kutafuta wafadhili. Hivyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara ilikamilisha Pendekezo la Mradi *(Project Formulation Proposal)* la upimaji katika eneo la Bahari ya Hindi na kuliwasilisha Wizara ya Fedha ili kutafuta mfadhili. Aidha, Shirika la Kimataifa la *International Hydrographic Bureau (IHB)* limepokea Pendekezo la Mradi na kuahidi kuliwasilisha katika Kamati yake ya "*Capacity Building*" mwezi Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, Idadi ya wananchi wanaotaka maeneo yao ya ardhi yapimwe ili kupata hatimiliki na kuingia katika mifumo rasmi ya uchumi wa nchi inaongezeka kwa kasi kila mwaka. Upimaji huu, pamoja na mambo mengine, hupunguza migogoro ya mipaka, na huwezesha mikataba ya miamala kama mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Wizara yangu imeendelea kufuatilia upimaji viwanja mijini na mashamba vijijini na hata kufanya baadhi ya kazi hizo moja kwa moja kufuatia upungufu mkubwa wa wataalam, fedha na vitendea kazi katika ngazi za Halmashauri za Miji na Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, jumla ya viwanja 18,000 na mashamba 1,777 yalipimwa nchini. Bado Halmashauri za miji na wilaya hazijaweka msukumo wa kujipatia uwezo wa kutoa huduma za upimaji ardhi kwa ufanisi. Natoa wito tena kwa Halmashauri zote kuongeza juhudi kujenga uwezo katika upimaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, upimaji ardhi Tanzania Bara, kwa ajili ya hatimiliki, ulianza kufanyika mwaka 1894. Rejea ya upimaji huo imekuwa ngumu kutokana na wingi wa taarifa zilizokusanywa katika miaka zaidi ya 100 iliyopita. Ili kuwezesha uwekaji wa kumbukumbu za upimaji uliopita na unaoendelea, juhudi zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha kwamba taarifa na kumbukumbu hizo zinaingizwa katika kompyuta na hivyo kurahisisha rejea na kuimarisha usalama wake. Asilimia 50 ya kazi hii imekamilika kwa Jiji la Dar es Salaam na kazi itaendelea kwa miji mingine nchini. Sambamba na juhudi hizo za kuimarisha kumbukumbu za upimaji nchini, Sheria ya Upimaji ya Mwaka 1957, inayotumika sasa, inahitaji kutungwa upya. Ili kutekeleza azma hii, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itaandaa Sera ya upimaji na utayarishaji ramani itakayozingatia Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa viwanja vilivyopimwa, hasa mijini, Serikali iliamua kuanzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja *(The Plot Development Revolving Fund-PDRF)* mwaka 2000. Lengo la mfuko huu ni kutoa fedha, kwa njia ya mikopo, kwa Halmashauri ili ziweze kutayarisha michoro ya mipango miji, kulipa fidia, kupima na kumilikisha viwanja na uwekaji wa miundombinu kama barabara, maji na mitaro ya maji taka kwenye maeneo ya viwanja vilivyopimwa. Hadi kufikia Juni 2005, Mfuko ulikuwa umekwishakopesha jumla ya Shilingi 576,041,111 kwa waombaji 34 na maombi mengine 22 yenye jumla ya Shilingi 3,184,712,481 yanaendelea kushughulikiwa na Wizara kulingana na upatikanaji wa fedha.

. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 kazi ya upimaji vijiji iliendelea katika Mikoa ya Lindi, Mbeya, Iringa, Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Juhudi zilielekezwa zaidi katika maeneo ya Babati, Ngorongoro, Arumeru, Hai na vijiji vilivyo kandokando ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Tarangire ili kusaidia utatuzi wa migogoro ya mipaka iliyojitokeza katika maeneo hayo. Aidha, Halmashauri nyingi za Wilaya zinakawia sana kusuluhisha na kurekebisha mipaka mbalimbali ya Vijiji na Wilaya na hivyo kupunguza kasi ya upimaji wa mipaka ya Vijiji. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 upimaji wa vijiji utaendelea katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Iringa na Mbeya. Natoa wito kwa halmashauri za wilaya kufanya juhudi za makusudi kutatua migogoro ya mipaka iliyopo ili kuwezesha upimaji kuendelea kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutoa ushauri wa kitaalam kusaidia kutatua migogoro ya mipaka kati ya mkoa na mkoa na wilaya na wilaya ndani ya nchi. Wizara inaendelea kushughulikia migogoro ya mipaka kati ya Mwanza na Kagera, Kagera na Shinyanga, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, mgogoro kati ya Wilaya za Hai na Arumeru umeshughulikiwa kwa Wizara kutoa tafsiri ya *Government Notices (GN)* zilizopo. Bado Halmashauri na mikoa husika haijafikia makubaliano licha ya msaada mkubwa uliotolewa na Wizara yangu.

. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka jana, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na nchi za Kenya, Uganda na Malawi kuimarisha mipaka kati yetu na nchi hizo. Kwa mpaka wa Tanzania na Uganda, wenye urefu wa kilomita 110, mazungumzo yamefikia hatua za ulipaji wa fidia ya mali za wananchi zilizokuwepo mita 10 ndani ya mpaka upande wa Tanzania. Protokali ya mpaka itahuishwa ili kujumuisha alama 402 za mpaka zilizoongezwa mwaka 2003. Nchi za Tanzania na Kenya zimekubaliana kurejesha alama za mpaka zilizong'olewa kwenye maeneo husika na kuongeza alama nyingine kwenye sehemu ambazo mpaka hauonekani kwa urahisi kuanzia Ziwa Jipe hadi Oloitoktok.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi zilikamilisha upembuzi yakinifu wa kudhibiti Mto Songwe. Mawaziri wa nchi zote mbili waliweka saini makubaliano ya Mpango wa Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe wenye miradi 13. Mkutano wa Wafadhili ulitarajiwa kufanyika nchini Malawi tarehe 26 Aprili, 2005. Hadi sasa, Tanzania inasubiri wito wa Malawi kufanya mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilitoa taarifa juu ya utata wa mpaka kati ya Tanzania na Zambia. Serikali imefanya ukaguzi wa maeneo yenye utata. Taarifa ya ukaguzi huo imewasilishwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuitisha mkutano wa pamoja utakaotoa fursa kwa nchi zote mbili kukagua na kurejesha alama za mpaka huo kwa njia shirikishi. Natoa wito tena kwa Halmashauri za Wilaya kulinda alama za mipaka yake na kuhakikisha kuwa makazi ya mipakani yanazingatia mipaka na sheria.

Jumla ya viwanja 30,655 vimepimwa jijini Dar es Salaam chini ya Mradi wa Upimaji Viwanja 20,000 kwa gharama ya Shilingi bilioni 22.8. Jumla ya viwanja 21,122 vimemilikishwa kwa wananchi na kuiingizia Serikali kiasi cha Shilingi bilioni 22.82 na uuzaji wa viwanja unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ya Fedha iliiruhusu Wizara yangu kutumia Shilingi bilioni 4.9 kama *"Revolving Fund"* ya kupima viwanja mijini. Kwa kutumia fedha hizi, Wizara yangu itaendelea kuziwezesha Halmashauri za miji kupima viwanja. Tayari mradi wa aina hii unatekelezwa katika jiji la Mwanza ambapo jumla ya Shilingi milioni 830 zimetolewa na Wizara ili kupima viwanja 3,500.

. Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuanzisha Hazina ya Ardhi kwa nia ya kuwa na vipande vya ardhi vilivyo tayari kuendelezwa kwa ubia kati ya wamiliki wa sasa na wawekezaji kwa matumizi mbalimbali kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC).* Maeneo

743 yalifanyiwa utafiti nchini kote. Kati ya hayo, maeneo 286 yameonekana yanafaa kwa uwekezaji, maeneo 415 yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi, na maeneo 42 yameonekana hayafai kabisa. Wizara yangu tayari imekabidhi orodha ya maeneo hayo 286 kwa *TIC.*

. Shughuli za uendelezaji wa makazi bora huchangia katika kuendeleza uchumi wa watu wanaoishi katika maeneo hayo na hatimaye kupunguza umaskini. Vile vile, nyumba bora ni muhimu katika maendeleo ya mwanadamu kwani huchangia katika kuwa na afya bora na kumwezesha kujiendeleza kiuchumi. Kwa ujumla, hali ya makazi nchini bado hairidhishi. Ongezeko la wakazi mijini ni la wastani wa asilimia 5 kwa mwaka wakati uwezo wa Halmashauri za miji na wilaya kutoa huduma kulingana na kasi ya ukuaji huo ni mdogo. Hadi sasa, inakadiriwa kuwa asilimia 70 ya wakazi wa mijini wanaishi katika maeneo yasiyopangwa na yasiyo na huduma muhimu. Kwa upande wa vijijini, takwimu zinaonyesha kuwa upungufu wa nyumba kwa ujumla haupo bali tatizo ni ubora wa nyumba. Idadi kubwa ya nyumba hizo zimejengwa kwa vifaa hafifu na zinaweza kudumu kwa wastani wa miaka saba tu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, unahitaji kuhuisha Sheria ya Mipango miji na Vijiji (Sura ya 378) ya Mwaka 1956 na Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 3 ya Mwaka 1984. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa kazi ya kuhuisha Sheria hizo itakamilika katika mwaka wa fedha 2005/2006. Vilevile, maandalizi ya rasimu ya sheria ya kusajili wataalamu wa fani ya Mipango Miji na Vijiji kwa lengo la kusimamia taaluma na kujenga maadili bora ya kazi za wataalam hao yanaendelea. Sheria hizo zitaiwezesha Wizara yangu kuelekeza nguvu zaidi katika kuandaa Mipango ya Kimkakati ya Miji, Mipango ya Uendelezaji Upya maeneo ya kati ya miji, Mipango ya Uendelezaji wa nyumba bora zenye bei nafuu na kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilikamilisha maandalizi ya mpango wa kusimamia ukuaji na uendelezaji wa mji wa Chalinze. Maandalizi ya mipango ya Kimkakati ya Miji ya Lushoto na Masasi yatakamilishwa katika mwaka 2005/2006 ambapo maandalizi ya mpango kama huo kwa mji wa Bukoba yataendelea kufanyika. Vilevile, chini ya Tangazo la Serikali Namba 353 la Mwaka 2004, miji midogo 90 ilitangazwa kuwa Mamlaka za Miji Midogo. Ili kusimamia ukuaji wa miji hiyo, Wizara itatoa mafunzo juu ya uandaaji wa mipango miji *(Interim Land Use Plans).* Katika mwaka 2005/2006, mafunzo hayo yatatolewa kwa Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Mtwara, Lindi na Ruvuma. Nia ya mipango hii ni kuelekeza uendelezaji wa matumizi ya ardhi na huduma muhimu za makazi katika miji hiyo. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo zina miji na vitongoji ambavyo vimekwishatangazwa kuwa mamlaka za miji midogo, zione umuhimu wa kuandaa mipango ya namna hiyo ili kuwezesha miji kukua kwa mpangilio mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu iliahidi kukamilisha mipango ya uendelezaji upya maeneo ya kati ya miji ya Kigoma na Sumbawanga. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, mipango hii imekamilika. Aidha, maandalizi ya mipango ya namna hiyo kwa miji ya Tanga na Singida yameanza

na yataendelea katika mwaka huu wa fedha. Hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utayarishaji wa mipango ya namna hiyo hapa nchini imeainishwa katika Jedwali Na. 13. Ninaomba Halmashauri za Miji ambazo zina maeneo machakavu, ziainishe mipaka ya maeneo hayo na kuwasilishwa Wizarani kwa ajili ya kutangazwa na kuandaliwa mipango ya uendelezaji. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu iliidhinisha jumla ya michoro 96 kutoka katika Halmashauri za Miji mbalimbali hapa nchini yenye jumla ya viwanja 32,634. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya, inatarajia kuandaa michoro ya mipango miji ya maeneo ambayo hayajapangwa na hayana huduma muhimu za makazi nchini. Miji itakayohusika ni Tabora, Mwanza, Mbeya na Moshi. Halmashauri za Miji zinahimizwa kuendelea kuandaa michoro ya maeneo mapya na kufanya rejea ya michoro kwenye maeneo mbalimbali ya miji ambayo michoro iliyobuniwa imepitwa na wakati. Michoro iliyorejewa inabidi ipitishwe na Halmashauri ndipo iwasilishwe Wizarani kwa ajili ya idhini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza hapo awali, wakazi wengi wa miji yetu wanaishi katika makazi yasiyopangwa na yasiyotambuliwa na mfumo rasmi wa uchumi na hivyo kushindwa kutumia miliki zao katika kupunguza umaskini licha ya maeneo hayo kuwa na rasilimali zenye thamani kubwa. Kwa kutambua hilo, Serikali imeanza kutambua maeneo hayo ili yaingie kwenye mfumo rasmi wa uchumi kwa kuwapatia leseni za makazi. Serikali imeanza na Jiji la Dar es Salaam linalokadiriwa kuwa na nyumba 400,000 katika maeneo yasiyopangwa. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, makazi 200,000 yametambuliwa. Idadi hii ni sawa na lengo lililowekwa. Kati ya idadi hiyo, wamiliki wa makazi 167,676 wamehakikiwa na kumbukumbu zao kuingizwa katika kompyuta. Ni nia ya Wizara yangu kutambua wamiliki wote katika maeneo yote Jijini Dar es Salaam ifikapo Juni 2006.

. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatarajia kutoa leseni za makazi kwa wananchi wote waliotambuliwa isipokuwa wale waliojenga katika maeneo yasiyofaa na ya hatari kwa makazi. Utoaji wa leseni za makazi, chini ya fungu la 23 la Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, ulizinduliwa tarehe 9 Mei, 2005 katika Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam ambapo wananchi 11 wa kwanza walikabidhiwa leseni zao za makazi. Aidha, Wizara yangu imetoa vifaa na mafunzo kuziwezesha Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke kuendelea na utoaji wa leseni za makazi kwa wananchi. Pia, ni kusudio la Wizara kujenga mfumo wa kuboresha makazi mijini na kudhibiti kupanuka kwa makazi holela kwa kuimarisha miliki.

Baada ya kukamilisha Sera ya maendeleo ya makazi ambayo inajumuisha uendelezaji wa nyumba, Wizara yangu inakusudia kutunga Sheria ya Nyumba *(Housing Act)* ili kuwezesha utekelezaji wa maamuzi muhimu ya uendelezaji wa nyumba yaliyotolewa kwenye sera hiyo. Wizara itaanza maandalizi ya Sheria hiyo katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliiahidi Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itarekebisha Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990 ya Shirika la Nyumba la Taifa ili kuboresha ukusanyaji wa kodi, kurahisisha upatikanaji wa maeneo yenye majengo chakavu na yasiyofaa kuishi kwa ajili ya kuyaendeleza na kuongeza uwezo wa Shirika

wa kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Baada ya kufanya uchambuzi zaidi wa suala hili, ililazimu kurekebisha baadhi ya vifungu vya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002 ya Mahakama za Ardhi, Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990 ya Shirika la Nyumba la Taifa na kufuta Sheria Na. 17 ya Mwaka 1984 ya Kodi za Nyumba. Mabadiliko haya ni kwa manufaa ya wenye nyumba na wapangaji wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama kubwa za usanifu wa majengo zimekuwa zikichangia kwenye gharama za ujenzi, na kwa kiasi fulani kuwa kikwazo kwa baadhi ya wananchi wanaotaka kujenga mijini. Wizara itaanza utaratibu wa kuandaa michoro mbalimbali ya nyumba ambayo itauzwa kwa gharama nafuu. Michoro hiyo itaweza kutumika katika mikoa mbalimbali ili kusaidia kupunguza gharama hizo. Katika mwaka wa 2005/ 2006 kwa kushirikiana na mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Ruvuma, Tabora, Dodoma, Mwanza na Mbeya, Wizara itaandaa michoro ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, tangu Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali uanzishwe mwaka 1992, kumekuwepo na mwamko mkubwa kwa watumishi wa umma kuomba mikopo kwa lengo la kujenga na kununua nyumba za kuishi. Hadi kufikia mwezi Juni 2005 yamepokelewa maombi 1,676 yenye thamani ya Shilingi 9,532,893,371.75. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 waombaji 22 walipewa mikopo yenye jumla ya shilingi 77,078,610.00. Hii inafanya idadi ya watumishi waliopewa mikopo tangu mfuko uanze kufikia 519 ambao ni sawa na asilimia 31 ya waombaji wote. Kati ya watumishi waliopewa mikopo, wanawake ni 195 sawa na asilimia 37.6. Mgawanyo wa watumishi hao kimkoa na kijinsia inaonyeshwa katika Hadi sasa fedha zilizokopeshwa ni Shilingi 1,650,611,818.75. Hata hivyo, maombi ambayo hayajashughulikiwa ni 1,157 yenye thamani ya Shilingi bilioni 8.9.

Mheshimiwa Spika, hali ya urejeshaji mkopo ni nzuri. Tangu mfuko uanze hadi kufikia mwezi Juni, 2005, marejesho halisi yalifikia Shilingi 392,798,848.50 ambayo ni sawa na asilimia 107.42 ya marejesho tarajiwa ya Shilingi 365,654,234.70. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 marejesho yamefikia Shilingi 98,371,414.25 kati ya Shilingi 79,881,397 zilizotarajiwa kukusanywa. Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana 2004/2005, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili mfuko huu upatiwe fedha zaidi za kukopesha. Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ya Fedha imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa madhumuni hayo katika mwaka huu wa fedha. Sasa, Wizara yangu itaweza kutoa mikopo kwa baadhi ya watumishi ambao maombi yao yamepokelewa.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ni nyenzo muhimu katika juhudi za kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya jamii kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Mipango hii inatilia mkazo matumizi endelevu ya ardhi pamoja na rasilimali zake. Kutokana na hali ilivyo sasa ushindani wa matumizi ya ardhi unaongezeka na hivyo kuleta migogoro katika sehemu mbali mbali na kusababisha kujitokeza kwa matumizi mabaya. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri za wilaya na vijiji kuwezesha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango hiyo. Hadi Juni, 2005 Kamati ya

Kitaifa imekamilisha rasimu ya kwanza ya uchambuzi wa taarifa na takwimu. Kazi hii itaendelea katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuwezesha Halmashauri za Wilaya kuunda timu za upangaji na kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyao. Uwezeshaji huo umefanyika katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Mafia, Handeni, Iringa, Njombe, Songea, Tunduru, Mbinga, Kyela, Rungwe, Mbozi, Sumbawanga Vijijini, Nkasi na Mpanda. Katika wilaya hizo, wajumbe wa Timu wamepewa mafunzo kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ngazi ya vijiji na wilaya. Rasimu ya Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa matumizi bora ya ardhi ngazi ya Wilaya itawasilishwa kwa wadau mapema katika mwaka wa fedha 2005/06. Wakati huo huo, uhuishaji wa miongozo ya utayarishaji mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi vijijini unaozingatia Sheria Mpya za Ardhi umekamilika. Kazi ya uchapaji na usambazaji itafanyika katika mwaka wa fedha 2005/06. Ili kuwezesha mipango hii kutoa mchango katika kupunguza umaskini na kuhifadhi mazingira, natoa wito kwa halmashauri za wilaya kuipa kipaumbele mipango ya matumizi ya ardhi kwa kuijumuisha katika mipango ya maendeleo na kuongeza ushirikiano na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Wakala ni kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya tafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu ili kuboresha hali ya nyumba za kuishi na kuinua maisha ya wananchi mijini na vijijini. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wakala uliendesha semina za uhamasishaji kwa maafisa Maendeleo ya Jamii, Kata na Wilaya; Madiwani na wataalam wengine 134 kutoka Halmashauri za Wilaya za Ileje, Mbozi, Uyui, Manyoni, Singida Vijijini, Singida Mjini na Iramba

Aidha, mafunzo ya vitendo kwa vikundi vya ujenzi kwa washiriki 81 yalifanyika katika Wilaya za Temeke, Ilala, Kinondoni, Manyoni, Singida Vijijini, Singida Mjini na Iramba. Pia, jumla ya majengo 17 yalijengwa, kati ya hayo, matatu ni ya mfano. Ili kuhakikisha kuwa teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu inawafikia wananchi walio mijini na vijijini, Wakala ulitangaza tafiti zake katika vyombo mbalimbali vya habari na kushiriki katika maonyesho mbalimbali ambapo watu zaidi ya 10,000 waliyatembelea. Vilevile, Wakala umesajiliwa kuwa Kandarasi Daraja la VI. Kwa sasa, Wakala unafanya matayarisho ya kuingia katika mfumo wa kimataifa (*ISO 9000 Compliant*) wa utoaji huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wakala utafanya kazi zifuatazo: - kuendesha semina za uhamasishaji ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu katika Wilaya tatu, itatoa mafunzo kwa vitendo (practical training and demonstrations) katika Wilaya tatu zilizopata semina za uhamasishaji katika mwaka wa fedha 2004/2005, utaendelea kutangaza na kusambaza teknolojia za ujenzi kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa, pamoja na kazi za msingi za utafiti, uhifadhi, ushauri, usambazaji na upimaji wa ubora wa vifaa mbalimbali vya ujenzi katika maabara ya Wakala na katika maeneo ya ujenzi. Naendelea kutoa wito kwa

Halmashauri zote nchini kuwasiliana na Wakala ili kutumia teknolojia zake katika kuboresha makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Nyumba la Taifa ni pamoja na kujenga nyumba mpya kwa ajili ya kupangisha na kuuza, kuhudumia nyumba za pango zilizopo na kuendesha shughuli za ujenzi kama mkandarasi. Shirika linategemea sana kodi ya pango ya nyumba zake kama chanzo kikuu cha mapato. Kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na.1 wa Mwaka 1992 na Marekebisho ya Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990 yaliyofanyika hivi karibuni, Shirika la Nyumba la Taifa linatakiwa kujiendesha kibiashara ili liweze kukuza mtaji wake na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa. Zoezi la kuongeza kodi za nyumba linalenga kuliongezea Shirika uwezo wa kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kulipa kodi mbalimbali za Serikali. Hadi Juni 2005 Shirika lililipa kodi kiasi cha Shilingi 15,690,127,104.

Mheshimiwa Spika, Shirika limekuwa likiendelea kuzifanyia matengenezo nyumba zake. Shirika limekuwa likitilia mkazo umuhimu wa matengenezo makubwa ya majengo *(structural repairs)* ili kuziweka nyumba katika hali ya kuridhisha na kukidhi haja ya wapangaji. Hadi kufikia Juni, 2005 Shirika limetumia Shilingi 2,374,736,950 kugharamia matengenezo ya nyumba 1,264. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Shirika litaendelea kutoa kipaumbele katika matengenezo ya nyumba kulingana na mpango wake wa miaka mitano ili kuhakikisha majengo yanakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2005, nyumba 4,304 kati ya 4,928 zilizoidhinishwa kuuzwa zimelipiwa kikamilifu na kulipatia Shirika mapato ya Shilingi 5,805,808,125.40. Mapato yaliyopatikana yameliwezesha Shirika kukamilisha ujenzi wa nyumba 198 za kuuza katika mikoa ya Dar es Salaam *(Boko na Mbezi Beach),* Mwanza (Isamilo) na Arusha (Kijenge). Kati ya nyumba hizo 191 zimejengwa Boko, 5 Mbezi Beach na 2 Kijenge. Aidha, majengo 6 ya vitega uchumi yamekamilika. Ujenzi wa majengo 8 ya vitega uchumi unaendelea katika miji ya Dar es Salaam na Arusha. Pia, Shirika limekamilisha ujenzi na ukarabati wa jengo la Mkuu wa Mkoa wa Kigoma -Ikulu Ndogo na kukarabati jengo la Wizara ya Kilimo na Chakula - Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Shirika litajenga jumla ya nyumba za kuishi 154 kwa ajili ya kuuzwa katika maeneo ya Boko, Tuangoma na Mbweni J.K.T. (Dar es Salaam), Isamilo (Mwanza), Kijenge na Mwandamo (Arusha). Aidha, Shirika litaanza ujenzi wa majengo makubwa 11 ya vitega uchumi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa hawajawa na utamaduni wa kulipa kwa wakati kodi za nyumba wanazopanga. Shirika linaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wapangaji wote ambao hawataki kulipa kodi.

Nazidi kusisitiza kuwa wapangaji wote waliobahatika kupewa upangaji wa nyumba za Shirika, waelewe kuwa nyumba za Shirika ni mali ya Watanzania wote, na kwamba mapato yanayotokana na nyumba hizo ni kwa ajili ya kuwapatia wananchi wengine nyumba. Haki yao ya kuendelea kuwa wapangaji wa nyumba hizo italindwa na kuheshimiwa iwapo tu watalipa kodi zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ni muhimu kuwa na watumishi waliojengeka kitaaluma na kuwa na vitendea kazi ambavyo vitawawezesha kutoa huduma bora. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya ofisi, kuwapatia watumishi stahili zinazoendana na ajira zao pamoja na kudumisha utawala bora. Msisitizo ulikuwa kudhibiti nidhamu, kupiga vita rushwa, na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara imeboresha utendaji kazi kwa kuajiri watumishi wengine 73 na inatarajia kuajiri watumishi 80 wa fani mbalimbali katika mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, ukarabati wa jengo la Ardhi unaendelea, na ukarabati wa ofisi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Singida na Mara umekamilika. Katika mwaka huu wa fedha, ofisi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Iringa, Manyara, Mwanza na Lindi zitakarabatiwa. Vilevile, Wizara inatarajia kununua jenereta ili kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ni moja kati ya Wizara zinazopokea wananchi wengi wanaohitaji huduma mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 idadi ya wananchi wanaohitaji huduma imefikia wastani wa 15,782 kwa mwezi. Kutokana na idadi kubwa ya wateja wanaoingia jengoni, Wizara imeweka mifumo mbalimbali ya kutoa huduma kwa haraka na kwa wepesi; mifumo hiyo ni pamoja na *front desk*, mtandao wa kompyuta, na barua pepe. Aidha, jumla ya barua 13,762 zilipokelewa na kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Ili kuongeza tija, nidhamu na ufanisi kazini, Wizara yangu ilitoa mafunzo juu ya Mfumo wa Wazi wa Upimaji Utendaji Kazi na Maadili ya Utendaji Kazi Serikalini kwa watumishi 605. Pia, watumishi 192 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 watumishi 112 wa Wizara na watumishi 10 kutoka Halmashauri za Miji na Wilaya watapatiwa mafunzo katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI ni janga ambalo limeendelea kusumbua jamii kwa kupoteza nguvukazi pamoja na kutumia fedha nyingi kwa matibabu na matunzo kwa waathirika. Wizara yangu iliendelea na juhudi za kutoa elimu ya Waelimisha Rika ili kuokoa watu na fedha kwa kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya watumishi 149 kutoka Vyuo vya Ardhi, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba na ofisi za Msajili wa Hati za Kanda walipatiwa mafunzo hayo. Wizara inatarajia kuunda Kamati za Waelimisha Rika kwa ajili ya kusimamia utoaji huduma kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro vinaendelea kutoa mafunzo ya Cheti na Diploma katika fani za Urasimu Ramani, Umiliki Ardhi na Uthamini, Uchapaji Ramani na Upimaji Ardhi. Fani hizi ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la mafundi sanifu wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 idadi ya wahitimu ilikuwa 84, kati yao 44 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 40 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora Idadi hii inatarajiwa kuongezeka na kufikia wahitimu 128 katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa taifa tarehe 30 Aprili, 2005, suala la ardhi na makazi lilipewa uzito maalum.

Baadhi ya mambo muhimu aliyotamka Mhe. Rais katika hotuba hiyo, ni pamoja na yafuatayo, ninanukuu: "Hatuwezi kushinda vita dhidi ya umaskini kwa silaha ambayo hatuna. Silaha ya uhakika aliyonayo kila Mtanzania ni ardhi. Kwa kutumia ardhi kama ardhi, na ardhi kama mtaji, tunaweza kuushinda umaskini ……." Akaongezea: "Tuone wivu na ardhi yetu, lakini zaidi sana tuwe na wivu wa maendeleo yanayoweza kupatikana kwa kutumia vizuri zaidi ardhi tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliyoyaeleza katika hotuba yetu yanazingatia maelekezo niliyoyanukuu kutoka hotuba ya Mheshimiwa Rais. Natoa wito kwa Watanzania wote kuchangamkia zoezi linaloendelea hivi sasa nchi nzima la kupima na kumilikishwa ardhi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hii ni njia mojawapo yenye uhakika wa kuwa na ajira binafsi. Hakuna mpango wa kuuza ardhi kwa wageni wasio raia. Sheria ziko wazi juu ya upangishaji ardhi kwa wageni. Tuepukane na kauli za kuwatia hofu wananchi kana kwamba Serikali yao haiwajali. Sera na Sheria zinawalinda wananchi, na yeyote anayekiuka Sera na Sheria hizo atashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, narudia wito wangu wa mwaka jana kwa wananchi kwamba, Mipango na mikakati yote iliyowekwa na Wizara yangu itafanikiwa tu iwapo wananchi watashirikiana na Wizara katika kufuata na kuzingatia utaratibu wa kupata huduma zinazotolewa na Wizara na Asasi zake, na kuwa wepesi kuwafichua wale wote wanaokiuka Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hajat Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge, Naibu Waziri. Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu kwa juhudi na mshikamano wao katika kufanikisha malengo ya Wizara na Taifa kwa ujumla katika kipindi chote tulichofanya kazi pamoja.

Pia, itakuwa ni ukosefu wa fadhila kama sitaishukuru Kamisheni ya Umoja wa Ulaya *(European Commission)* ambayo imeisaidia Wizara kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za *Ardhi (Strategic Plan for the Implementantion of Land Laws – SPILL),* na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi *(UN-HABITAT)* ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa katika utayarishaji na utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kuboresha makazi nchini.

Vilevile, mashirika yasiyo ya Kiserikali yaliyoshirikiana na Wizara katika kutoa elimu ya Sheria za Ardhi na Mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi Vijijini. Msaada wao tunauheshimu na kuuenzi na nawaomba wadau wengine zaidi kujitokeza kusaidia jitihada za Serikali kuboresha huduma za ardhi na makazi kwa wananchi. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hotuba yangu, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Wananchi wa Jimbo na Wilaya ya ILEJE kwa ushirikiano wao na jitihada zao za kujiletea maendeleo binafsi na ya pamoja.

Nawashukuru sana kwa heshima na imani waliyonipa kuwa mwakilishi wao kwa awamu hii ya Tatu. Tumejitahidi kwa pamoja kupiga hatua ya maendeleo katika Sekta zote muhimu katika Wilaya yetu. "Wenye macho hawaambiwi tazama". Hata hivyo safari ya maendeleo bado ndefu, nami niko tayari kuendelea kushirikiana na wananchi wote wa Wilaya ya Ileje katika safari hiyo yenye matumaini, na Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kama ilivyokuwa kwa mwaka 2004/2005 itatekeleza kwa nguvu moja kazi ilizojipangia ili iweze kuchangia vema katika mkakati mzima wa kupunguza umaskini nchini. Sasa, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2005/2006 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 9,043,330,000 kama Makusanyo ya Mapato ya Serikali.

(ii) Shilingi 2,380,235,044 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

(iii) Shilingi 9,342,160,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(iv) Shilingi 2,100,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Jumla ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 13,822,395,044.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe, na pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akuketi) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia makadirio hayo.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2004/2005; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati yangu ningependa kutumia nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati yangu kutoa pole na rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kilombero kwa msiba wa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abuu Towagale Kiwanga aliyefariki dunia tarehe 2 Juni, 2005.

Aidha tunatoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Margareth J. Bwana aliyefariki dunia tarehe 23 Juni, 2005. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ya Kilimo na Ardhi ambao naomba niwatambue:-

Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Mussa A. Lupatu, Mheshimiwa Phillip A. Magani, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Charles H. Kagonji na Mheshimiwa Robert K. Mashalla.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa. Paul N. Makolo, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mhe. Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Edward N. Ndeka na Mheshimiwa Salama Khamis Islam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo zaidi ya 11 yaliyolenga katika uboreshaji na utekelezaji wa mipango na kazi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu maagizo yote yametekelezwa kwa ukamilifu wake. Hata hivyo bado baadhi ya maagizo ambayo utekelezaji wake ni endelevu. Kamati yangu iliridhika na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika kutekeleza maagizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha uliopita. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

Moja, Utoaji wa vyeti 57 vya ardhi ya vijiji na hati za kimila Wilayani Mbozi, pili, kutoa Elimu ya Sheria ya Ardhi Na.5 kwa Wananchi, tatu, uthamini wa mali 2,003 ulioiingizia Serikali jumla ya Sh.123,246,664/= na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 23 na nne, uzinduzi wa Masjala ya Ardhi za Wilaya ya Iringa na Kijiji cha Kiwele na kutoa hati miliki za kimila 12.

Tano, kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* Wizara imeweza kutambua maeneo ya uwekezaji 286 yenye jumla ya hekta 416,441 nchi nzima. Pia, maeneo mengine 317 yasiyopimwa yenye hekta 1,970,774 yalitambuliwa.

Sita, jumla ya hati 5,548 za ardhi zilisainiwa, hatimiliki za ardhi 5,464 na nyaraka zihusianazo na miliki za ardhi 5,162 zilisajiliwa. Utoaji wa vibali vya uhamisho wa miliki na uwekaji rehani wa hati na hati za kumiliki ardhi 2,633 umekamilishwa.

Saba, kukamilisha upigaji picha za anga katika miji 35 katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa, Mbeya na Iringa.

Nane, Upimaji wa Viwanja 18,000 na mashamba 1,777 nchini kote.

Tisa, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi na Mabaraza ya Nyumba yaliamua jumla ya mashauri 1,061 ya Ardhi, 449 ya nyumba, rufaa za mashauri ya ardhi 67 pamoja na 97 za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, Kamati yangu pia ilielezwa matatizo yaliyoikabili Wizara hii ambayo baadhi yake ni:-

(i) Ukosefu wa ramani za msingi *(Base Maps)* kwa nchi nzima ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na upimaji wa viwanja na mashamba;

(ii) Gharama za fidia ni kubwa sana kiasi cha kuzuia utwaaji wa maeneo kwa ajili ya kupima viwanja vya kutosheleza mahitaji ya wananchi Mijini;

(iii) Ukosefu wa Mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na ununuzi wa nyumba zinazojengwa na Mashirika kama Shirika la Nyumba *(NHC)*, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na kadhalika;

(iv) Mipaka kati ya nchi yetu na nchi jirani kutotambulika kutokana na alama kuharibika, kung’olewa au kuwa mbali sana;

(v) Pamoja na juhudi za kutoa elimu juu ya Sheria mpya za Ardhi, bado wananchi walio wengi wana uelewa mdogo juu ya Sheria hizo;

(vi) Halmashauri nyingi hazijaajiri Wataalam wenye sifa za kusimamia na kutoa huduma za ardhi. Aidha, Ofisi za Ardhi kwenye Halmashauri hizi hazipewi kipaumbele katika kugawiwa rasilimali na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni na mapendekezo ya Kamati, nichukue fursa hii kutoa pongezi na shukrani maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kukubali kutembelea mradi wa nyumba za kuuza wa Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), Boko.

Katika ziara hii, pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais aliagiza Sheria zinazokwamisha maendeleo ya Shirika kwa kuwalinda sana wapangaji zifanyiwe marekebisho na Bunge kabla yeye hajamaliza muda wake wa kuwa madarakani. Aidha, Mheshimiwa Rais alikiita kitendo cha watu kuishi katika nyumba za kupanga bila kulipa kodi husika kuwa ni kitendo cha ubinafsi na cha unyonyaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Muswada wa marekebisho hayo tayari umewasilishwa Bungeni na kupitishwa na kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, bila shaka ataridhia mabadiliko ya Sheria hii ili ianze kutumika. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa Shirika la Nyumba sasa litaendelea kujiendesha kibiashara na kwa ufanisi zaidi.

Pia, litaboresha na kupanua miradi yake, hivyo kuboresha makazi ya wananchi Mijini na Vijijini. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kwamba Shirika la Nyumba chini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi liendeleze maeneo yake yaliyoko Mijini kwa kujenga nyumba za kisasa badala ya kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Bajeti 2005/2006, katika kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 na malengo ya bajeti kwa mwaka 2005/2006 kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilipata maelezo ya kina ya majukumu ya Wizara, malengo ya Wizara na utekelezaji wake kwa mwaka uliopita na mipango iliyowekwa kwa mwaka ujao wa fedha 2006/2007.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza malengo na miradi mbalimbali ya kuboresha makazi nchini na pia kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Katika kuzidi kuboresha utendaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Kamati yangu inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado katika sehemu kubwa ya nchi hakuna mipango mizuri ya utumiaji wa ardhi, Kamati inaishauri Serikali isaidie upatikanaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na halikadhalika upimaji wa viwanja vya mashamba na maeneo ya burudani, kwa mfano, Viwanja vya Michezo na kadhalika.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika**,** kipato cha mishahara kwa wafanyakazi na hata pato la mwananchi wa kawaida bado ni dogo na hivyo kutomudu kununua au kujenga nyumba. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha chombo maalum cha kutoa mikopo ya muda mrefu ili wananchi waweze kujenga nyumba bora za makazi na pengine kununua nyumba zilizokwishajengwa na Shirika la Nyumba, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) au Shirika lolote lingine.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa mipaka ya nchi yetu na nchi jirani haitambuliki vyema kutokana na alama kuharibika. Kamati imeishauri Serikali kuongeza kasi ya kulishughulikia tatizo hili ili hapo baadaye lisije kuwa tatizo kubwa kwa sehemu za nchi yetu kumegwa na Mataifa mengine na hivyo kuhatarisha amani, utulivu na ushirikiano wa nchi yetu na jirani zake.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika sana na utendaji wa Wizara juu ya kuendeleza makazi kwa wananchi. Hata hivyo, Halmashauri nyingi bado hazijakidhi haja, hivyo kutokwenda sambamba na mafanikio ya Wizara. Kamati inashauri kuwepo na mahusiano baina ya Halmashauri na Wizara husika ili usimamizi uweze kufanyika kiufanisi na hivyo kuwapatia Wananchi makazi bora na utumiaji mzuri wa ardhi.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uanzishwaji wa Mabaraza ya Nyumba katika Wizara /Halmashauri; bado wananchi wanapeleka kesi zihusuzo nyumba katika Mahakama za kawaida. Kamati inaishauri Wizara izidishe bidii za kuwaelimisha wananchi kwa kutoa vipeperushi au kwa njia yoyote nyingine ili kuwapatia ufahamu wa namna migogoro inayohusu ardhi inavyoweza kushughulikiwa.

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado kuna tatizo la watu kupewa viwanja na kushindwa kuviendeleza hata zaidi ya miaka kumi (10) kwa baadhi ya watu, Kamati inashauri kuwa Wizara ihakikishe kuwa sheria inafuatwa ili wenye nia hasa ya kuviendeleza viwanja hivyo ndio wapatiwe.

(vii) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana imejengeka kuwa unapopatiwa kiwanja na kujenga msingi tu unakuwa tayari umekiendeleza. Hatuna hakika kama hii ndiyo maana iliyokusudiwa. Matokeo yake kuna viwanja vingi ambavyo vimejengwa msingi tu na kutelekezwa kwa miaka nenda rudi. Kamati inaishauri Wizara itoe mwongozo wa namna sahihi ya kuendeleza viwanja hivyo.

(viii) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya watu huomba viwanja kwa ajili ya ujenzi wa makazi na kusema wako tayari kuwafidia wenye mashamba ili wapate viwanja hivyo. Matokeo yake hawaviendelezi kama walivyoomba bali huendeleza mashamba hayo kwani nia hasa ilikuwa ni kutaka shamba na sio ujenzi wa nyumba za makazi. Kamati inaishauri Wizara iwe ikifanya ufuatiliaji ili kubaini udanganyifu na kuwachukuliwa hatua ipasavyo.

(ix) Mheshimiwa Naibu Spika**,** ili kufikia dira ya Wizara Kamati inashauri Halmashauri ziajiri Wataalam wa Ardhi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kidunia katika suala zima la uboreshaji wa makazi.

(x) Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya ziara za Kamati yetu katika Taasisi za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilibaini kuwa jengo lenye mitambo ya kutengeneza ramani ni bovu sana, kwani lilijengwa tangu enzi za utawala wa Wajerumani. Ubovu huo unatishia usalama na mazingira yanayotakiwa katika kutunza na kutumia mitambo na zana na Kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliishauri jengo hili likarabatiwe. Hata hivyo, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imefahamishwa na Wizara kuwa Hazina imeitengea Wizara Shilingi milioni 130 katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006 ili kuandaa michoro pamoja na maandalizi ya awali ya jengo jipya. Naipongeza sana Serikali. Kamati inaamini kuwa kazi hii haitachukua muda mrefu kukamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Mafuta House*, limeongelewa sana hapa Bungeni, nataka kuikumbusha Serikali kuwa Shirika la Nyumba la Taifa na Shirika la Petroli walitumia fedha nyingi kugharamia ujenzi wa *Mafuta House. (Makofi)*

Ni haki Mashirika haya mawili ama yapewe hisa kulinga na fedha walizofidiwa gharama waliyotumia katika kusaidia kujenga *Mafuta House,* fedha hizo zisaidie kuimarisha ujenzi wa miradi mingine na hivyo kuimarisha Sekta ya Nyumba ambavyo ni muhimu katika kutatua matatizo ya nyumba nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba kumpongeza sana Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo - Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Tatu Ntimizi - Mbunge, kwa uhodari wao katika kuongoza Wizara hii muhimu na kwa ushirikiano mkubwa tuliopata toka kwao kuanzia wakati wa ziara katika Taasisi zao hadi Vikao vya Kamati kuchambua Bajeti ya Wizara.

Aidha, nawashukuru Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Bibi Salome Sijaona, ambaye kwa kweli ni mama mahiri sana, amefanya kazi yake vizuri sana. Mama huyu tumpongeze sana, pamoja na wasaidizi wake wote kwa ushirikiano mzuri wakati wa Vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na ushirikiano wao wakati wa kuchambua na kupitia vifungu mbalimbali vya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani za dhati kwako na hasa Katibu wa Bunge Bwana Damian Foka, pamoja Makatibu wa Kamati hii Bi Nenelwa Mwihambi na Ndugu Abdallah Hancha kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kutoka kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Cheyo, anagombea na Mheshimiwa Tatu Ntimizi anagombea, Kamati imesema niwaeleze kwamba tunawatakia kila la kheri, bila shaka watapita tu kwa sababu wamefanya kazi njema. *(Makafi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa heshima kubwa, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liijadili na kukubali kuipitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| • Matumizi ya Kawaida | TSh. | 11,722,395,044.00 |
| • Matumizi ya Maendeleo | TSh. | 2,100,000.000.00 |
| Jumla | TSh. | 13,822,395,044.00 |

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijali mimi pamoja na sisi sote tukaweza kuamka na afya nzuri asubuhi na tukaweza kushiriki katika shughuli hizi bila pingamizi lolote. Kabla ya yote, naomba nitoe shukrani na pongezi zangu kwa Uongozi mzima wa Kambi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Lwakatare, Kiongozi wa Upinzania Bungeni kwa ushirikiano tunaoupata katika kutimiza malengo na mjukumu yetu hapa Bungeni.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Gedion Cheyo - Mbunge na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi - Mbunge na Naibu Waziri, bila kumsahau Katibu wao Mkuu Mama Salome Sijaona Ngonyani kwa ushirikiano niliioupata katika kutimiza majukumu yangu kwa kipindi ambacho nimekuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nitoe taarifa juu ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao umefanyika jana katika Wilaya ya Bariadi ambapo katika uchaguzi huu ulihusisha Vijiji 11. Katika Vijiji hivyo 11 Kambi ya Upinzani ilishinda Viti kumi na Kiti kimoja Mgombea wa CCM alipigiwa kura ya hapana kwa kuwa alibaki peke yake baada ya kumwekea pingamizi mgombea wa *UDP* kwa nafasi hii. Naomba niwashukuru wananchi wa Bariadi, kwa jinsi walivyoonesha uzalendo wao wa kuchagua Kambi ya Upinzani na hii inaonyesha kwamba ndio mwelekeo wa uchaguzi utakavyokuwa Oktoba 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitaomba mniwie radhi kwa kusema kuwa, ugomvi mkubwa kati yetu na Serikali unakuwa kwenye sehemu moja tu, ambayo ni matumizi ya kawaida. Hapa Wizara imeomba kupewa ongezeko la asilimia 106 kwa bajeti ya matumizi ya kawaida na ongezeko la asilimia 63 kwa fedha za matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, matumizi ya kawaida ni kupandisha kima cha posho za safari, simu na umeme. Kitu tunachoshindwa kuelewa ni kwamba sasa hivi tuko kwenye kufungishana mikanda ili kuweza kuwakuta wenzetu waliotangulia. Tulitegemea yale yanayoimbwa kuhusu maendeleo kuwa ni ya kweli. Sasa tujiulize ni wafanyakazi wangapi katika Wizara wanapata hizo posho za simu na umeme? Inawezekana posho ya mtu kwa siku mbili ni sawa na mshahara wa miezi miwili wa mtumishi anaelipwa kima cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara kuhusu ulipaji wa kodi ya majengo ikusanywayo Mikoani na Wilayani inaonyesha inaweza kuleta matatizo au inaleta matatizo, kwani kodi kwa jengo inakadiriwa tu, hakuna kigezo zaidi ya macho ya mkusanyaji kulingana na anavyoliona hili jengo. Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara itoe mwongozo kuhusu kodi za majengo zilipwe vipi, yaani waweke *standard* moja. Mfano, nyumba yenye vyumba viwili au vitatu, basi kodi yake ya jengo iwe moja, na kadhalika. Kodi isiangalie uzuri wa nyumba.

Pia, ukiachilia mbali kodi ya Wizara, kuna kodi ambazo zinakusanywa na Halmashauri, Manispaa na City ambao nao pia wanatoza kodi za majengo. Hii ni kuwaongezea mzigo wananchi wetu. Tunaomba Wizara hapa iangalie ili iweze kufuta hizi kodi ambazo zinatolewa na hizi Taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu niliyoitoa hapa Bungeni mwaka jana 2004, niliongelea kuhusu hati za umilikaji ardhi wa miaka 33, zitolewazo kwa wazawa kwamba zibadilishwe na umiliki uwe ni wa miaka 99 kama ilivyo kwa wageni, kwani utaratibu huu unawakandamiza wazawa wakati wageni wanakuwa na haki zaidi. Mfano mzuri kwa sasa, wawekezaji wanochotaka katika uwekezaji ni kupata hati ya umiliki wa ardhi, wakishapata ni wao wataamua hiyo ardhi yao waifanyie nini kwa kipindi cha miaka hiyo yote. Nimeyarudia kwa uchungu, kwani Serikali imeshindwa kwa makusudi kulifikiria suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Tanzania ina Wizara nzima inayoshughulikia masuala ya ardhi, ina Chuo Kikuu kishiriki kinachoshughulikia masuala ya ardhi tu na kuna Idara za Mipango Miji katika kila Halmashauri na Mabaraza ya Miji, hali ya makazi ya wananchi inazidi kuwa mbaya siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba mkubwa wa viwanja vilivyopimwa umewalazimisha wananchi wengi kujenga makazi kwenye maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu na ambayo hayana huduma za msingi kama vile mitaro ya maji machafu, vyoo vya umma, barabara, viwanja vya kuchezea watoto na sehemu za kuzikia za uhakika. Mathalani, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wakazi wote wa Jiji la

Dar es Salaam wanaishi kwenye maeneo yaliyojengwa holela na yenye msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hali hii imewalazimisha baadhi ya wananchi wengine kujenga sehemu za mabondeni na hivyo kuhatarisha usalama wa maisha na mali zao wakati wa mvua za masika. Ukosefu wa sehemu za uhakika wa biashara za Machinga na uhaba wa Vituo bora vya mabasi na maegesho rasmi kwa ajili ya vyombo vya usafiri hususan magari, umetokea kuwa ni kero kubwa kwa wananchi wengi hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Pamoja na yote haya, pia, kuna udhaifu mkubwa sana katika kusimamia sheria zinazotawala makaazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo haya, sheria ndogondogo zinazotungwa na Halmashauri na Mabaraza mengi ya Miji hazizingatii hali halisi ya kimaisha ya wakaazi wa Miji husika. Mathalan, katika baadhi ya Miji, kuna sheria inayowakataza wakaazi kufanyia matengenezo nyumba zao zinazochakaa kwa maelezo kwamba maeneo ziliko nyumba hizo yametengwa kwa ajili ya kujenga maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya sheria hii ni kwamba katika Miji mingi kuna nyumba nyingi chakavu zinazokaribia kuanguka huku wamiliki wake wakisubiri zianguke na wao kupoteza haki ya kumiliki viwanja husika kwa sababu hawana uwezo wa kujenga maghorofa. Ni wazi kabisa kuwa sheria ya namna hii siyo tu kwamba ni ya kiukandamizaji, lakini pia ni yenye kuongeza kiwango cha umasikini miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, alieleza kuwa kuna maeneo 317 yasiyopimwa yenye hekta 1,970,774 yalitambuliwa na sababu kubwa ya kushindikana kupimwa ni kukosekana kwa *base maps.* Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutueleza kama kunakuwa na picha zinazopigwa toka angani, *reference points* za kuanzia na kumalizia upimaji na vitu vingine vitakavyokuwemo ndani ya ramani hizo tunadhani zinawekwa kabla ya kazi yenyewe kuanza. Hivyo basi, *base maps* zinakuwa na kazi gani?

Nakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Damas Nakei alilalamikia upandishwaji wa gharama za upimaji kwa wananchi Jimboni kwake kwa ajili Watendaji kufuatilia *reference points* Mjini Arusha kitu kinachozidisha gharama halisi za upimaji. Tunaomba tena ufafanuzi wa hayo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imebaini baadhi ya Kasoro zilizomo ndani ya Sekta hii ya Ardhi.

Pamoja na kwamba hivi karibuni Serikali imebuni mradi wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam, bei za viwanja hivyo ni za juu mno kwa watu wa kawaida kuweza kuzimudu. Matokeo yake ni kwamba vingi kati ya viwanja hivyo vitaangukia katika mikono ya watu wachache wenye uwezo na wananchi wa kawaida ambao ndiyo wengi wataendelea na ujenzi holela katika maeneo yasiyofaa.

Kasi ya kuboresha maeneo ya makazi ambayo hayajapimwa kwa kukata barabara, kuweka maeneo ya ujenzi wa Shule, Vituo vya Afya na viwanja vya kuchezea watoto ni ndogo mno. Matokeo yake ni kwamba huduma muhimu, mathalan za magari ya zimamoto na magari ya wagonjwa bado ni vigumu kuwafikia wakazi walio wengi katika maeneo hayo.

Kuna udhaifu mkubwa katika kuandaa maeneo ya biashara za Machinga na maeneo mengine muhimu kama Vituo vya Mabasi ya daladala. Kutokana na hali hii, kuna baadhi ya Mitaa ambayo wakazi wake wanapata adha kubwa kutokana na msongamano mkubwa wa biashara hizo na wingi wa daladala zilizogeuza Mitaa hiyo kuwa stendi za kupakia na kushusha abiria.

Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria ndogo ndogo zinazotawala makazi na hususan katika maeneo ya Mijini, bila ya hatua zozote kuchukuliwa.

Serikali imeshindwa kabisa kukitangaza kitengo chake cha mradi wa utafiti wa nyumba za bei nafuu, yaani *National Housing and Building Research Agency* (*NHBRA)* na matokeo yake ni kwamba wananchi walio wengi hawanufaiki na kuwepo kwa kitengo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ikipata ridhaa ya wananchi kwa kutupa kura zao kuwa na Serikali, itachukua hatua zifuatazo:-

Kwanza kubinafsisha Shirika la Nyuma la Taifa, kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Serikali ya CCM imesharuhusu watu binafsi kujenga na kumiliki majengo yenye thamani yoyote ile na pia imekuwa na utaratibu wa upendeleo wa kurejesha baadhi ya majumba yaliyotaifishwa kwa wamiliki wake wa awali. Hakuna sababu za msingi kwa Serikali kuendelea kumiliki majumba ya watu wengine ambayo iliyapora katika miaka ile ya utaifishaji. Serikali itaweka utaratibu wa kuwarejeshea majumba yao wale wote waliokuwa wametaifishiwa na hawakulipwa fidia na baada ya zoezi hili italibinafsisha Shirika la Nyumba la Taifa.

Pili, upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa, Serikali itahakikisha kwamba katika kipindi cha miaka miwili tu, katika Miji yote nchini viwanja vilivyopimwa na vinavyopatikana kwa bei ndogo ndivyo vitatafuta wajenzi, badala ya hivi sasa ambapo wananchi mbalimbali wenye nia ya kujenga ndio wanaohaha kutafuta viwanja hivyo. Huduma za barabara, maji na umeme kwenye makaazi zitakwenda sambamba na upimwaji wa viwanja vipya.

Tatu, Serikali itasitisha mara moja ukiukwaji mkubwa wa Sheria za Mipango Miji uliopo hivi sasa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Serikali itaweka mkakati imara wa kuhakikisha kuwa kila penye makaazi na hasa kwenye maeneo ambayo yamejengwa kiholela, barabara zinapitishwa, mitaro ya maji machafu inakuweko au kufanyiwa ukarabati, vyoo vya umma vinasambazwa, taka zinazolewa kwa wakati na madimbwi yanayotuama maji wakati wa mvua yanatoweka. Serikali pia itahakikisha kuwa uhaba wa sehemu za kuzikia, Vituo bora vya Mabasi, sehemu za uhakika kwa

biashara za Machinga, viwanja vya kuchezea watoto na bustani za mapumziko unapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Gharama za ujenzi kwa kiasi fulani zitapungua kutokana na azma ya Serikali ya kurekebisha viwango vya kodi. Serikali itakiimarisha na kukitangaza kwa nguvu zote kitengo chake cha Mradi wa Utafiti wa Nyumba za Bei Nafuu na kuwahamasisha wananchi wote wa Mijini na Vijijini wakitumie kujengewa nyumba bora kwa gharama nafuu. Aidha, katika maeneo ya Mijini, Makampuni zaidi yatahamasishwa kwa ajili ya kujenga nyumba za gharama nafuu na kuzigawa kwa wananchi mbalimbali kwa mikopo ya masharti nafuu na ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ndogo iliyotungwa na baadhi ya Manispaa inayowakataza wakazi wa baadhi ya maeneo kufanyia matengenezo nyumba zao kwa madai kwamba maeneo hayo yametengwa kwa ajili ya maghorofa, hii sisi itafutwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu, Wizara ya Ujenzi mwaka huu, tuliongelea kuhusu mikopo ya nyumba, naomba nirudie tena kuwa Serikali hii na nchi hii ni ya Watanzania wote ambao ni watumishi wa Umma, watumishi wa sekta binafsi, wafanyabiashara na wakulima. Hivyo basi, Serikali kutoa kipaumbele kwa ajili ya kuwakopesha watumishi wa Serikali peke yao, ni kutotenda haki, kwani kada zote za Watanzania nilizozitaja ni walipakodi na kwa njia moja au nyingine mikopo ya Serikali nayo wanawajibika kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema kuwa mikopo ya nyumba itolewe kwa Watanzania wa kada zote, kwani wote wanastahili kupewa haki hiyo kwa kuwa Serikali ni ya wote. Kitu cha kuzingatia ni namna ya kutimiza masharti yatakayowekwa ya kukopeshwa nyumba au mikopo ya fedha kwa ajili ya kujijengea nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kambi ya Upinzani haina kizuizi na upitishwaji wa bajeti hii, ila inaomba fedha za matumizi ya kawaida kweli yawe kwa manufaa ya Watendaji na isiwe kwa manufaa ya wajanja wachache au zikaingia kwenye shughuli nyingine kabisa zisizokuwa na uhusiano na Wizara hii, kwani huu ni mwaka wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu kwa Chama changu cha *CUF* kwa kuniamini na kunirudisha tena kugombea Kiti cha Ubunge katika Jimbo la Ziwani.

Ninakihakikishia Chama changu cha *CUF* kuwa nitakileta ushindi mkubwa kwa ushirikiano na viongozi wenzangu. Pia, nawashukuru wapigakura wa Jimbo la Ziwani kwani wao ndio waliniwezesha kufanya yote niliyoyafanya, naomba tena wanipe ridhaa yao. Pia, nachukua nafasi hii kumkaribisha yoyote ambaye ana ubavu aje katika Jimbo la Ziwani lakini ajitayarishe kupoteza *deposit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitaishukuru familia yangu ambayo imenivumilia kwa muda mwingi niliokuwa nje ya familia yangu.

Pamoja na mitihani mikubwa niliyokutana nayo kuanzia Dar es Salaam kwenye Vikao vya Kamati na hapa Dodoma kwenye Vikao vya Bunge, naihakikishia kuwa nimefaulu asilimia mia na ninawaahidi kukidhi haja zao ipasavyo mara nitakaporudi. *(Makofi)*

Aidha, ninaishukuru Kambi ya Upinzani chini ya Kiongozi wetu Mheshimiwa Lwakatare kwa ushirikiano na mwongozo alionipatia katika kipindi chote ambacho nimekuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu mlionipatia katika maswala mbalimbali.

Mwisho kabisa, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Pius Msekwa - Spika wa Bunge na Naibu Spika - Mheshimiwa Juma Akukweti, pamoja na Wenyeviti kwa hekima zao katika kuliongoza Bunge hili wakati wa kipindi chote cha uhai wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo kawaida tunaanzia na wale ambao wamechangia mara moja au hawajachangia kabisa. Sasa kwenye orodha ya leo tunao walioomba, wako watano ambao nadhani wanatosha nitawataja wote ili waweze kujiandaa. Nao ni Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Edson Halinga. Naona wote watapata nafasi. Kwa hiyo, sasa naanzia na Mheshimiwa Halima Kimbau atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Naanzia kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, halikadhalika Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi chote ambapo walikuwa wanaiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda, kuwapongeza sana kwa jitihada yao ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia kukusanya kodi zote za ardhi na kutumia kila njia hata kuweza kukusanya kiwango kikubwa na wao kuweza kubakishiwa kiwango kikubwa cha kuweza kuendeleza Wizara yao na Idara zao zote ambazo zinatupatia huduma sisi Watanzania tunaohitaji matumizi ya ardhi bora. Lakini pia napenda kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mama Salome amekuwa karibu sana na Watendaji wenzake. Ni wazi kwamba sio rahisi kuweza kupata mafanikio katika utendaji kama hukuwa karibu sana na wenzako. Lakini siyo tu karibu sana na wenzake wa Wizara lakini pia karibu na hata wateja wake na ndio maana mafanikio yamepatikana kwa sababu sisi kama wateja wake tunapofika Wizarani tunapata huduma nzuri. Hivyo, ndio maana tumefikia kwamba mpaka sasa hivi wengi wanaongelea kwamba hii Wizara imepata mafanikio makubwa hasa kwenye kuondoa suala la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma, Wizara hii ilikuwa inanuka sana. Kila mmoja alikuwa akiiongelea Wizara ya Ardhi kwenye suala la rushwa. Lakini sasa hivi pamoja na kwamba binadamu hakamiliki, lakini amejitahidi sana yeye na Watendaji wenzake kuona kwamba rushwa inaondoka na watu kupata haki zao kwa ufanisi kuliko huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote ya pongezi, napenda kuwaomba watusaidie kwenye mambo mawili. Wamejitahidi kutupimia viwanja vingi tu Dar es Salaam na wanategemea kupima vingine katika Miji mingine kama Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili utakuta mpaka leo unapotembela maeneo haya yaliyopimwa na watu kugaiwa viwanja na kulipia, lakini bado ujenzi umekuwa wa taratibu mno. Sasa ukifuatilia zaidi utakuta kwamba miundombinu ya kuwawezesha hawa walioomba viwanja waweze kujenga nyumba zao kwa haraka bado haijakamilika. Tunaona ni barabara tu ambazo zimesafishwa, Mitaa imepangwa na *TANESCO* kuanza kuweka umeme, lakini kwenye suala la maji bado linakwenda taratibu mno na ninadhani kila mmoja anafahamu kwamba huwezi kujenga bila ya maji.

Sasa ukitembelea kwa mfano Bunju, Mbweni utakuta mtu anaagiza gari la maji kwa gharama kubwa, lakini bado viwanja vile vilitolewa kwa matumaini kwamba miundombinu yote itakuwa tayari ili wananchi waweze kujenga kwa haraka na hatimaye tupate Miji ambayo inapendeza.

Sasa hili ningeomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji waone ushirikiano gani watakaowapa hawa watu wa maji na watu wa umeme hapo baadaye kuweza kusambaza maji kwa haraka ili wananchi waweze kujenga nyumba zao kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nampongeza Waziri kwa jitihada ya kuweza kuwapa hata hawa ambao wamejenga kiholela leseni za miliki. Lakini bado tunalo tatizo hili ambalo kwa muda mrefu wananchi wengi wa hali ya chini na hasa baada ya kuambiwa kwamba ardhi ni njia moja ya kuweza kumwondolea mtu umaskini, lakini haiwezi kuwa ni mali mpaka uwe na hatimiliki. Sasa tatizo liko kwenye hatimiliki.

Hivi viwanja vipya karibu wote wamepata hatimiliki, lakini watu wa zamani ambao wana nyumba zao tayari, suala la kupata hatimiliki imekuwa ni tatizo kubwa. Kwa

hiyo, wananchi wanashindwa kuweza kuziendeleza hizo nyumba zao ambazo wanazo kwa kuweza kuchukua mikopo pale ambapo wanahitaji. Lakini pia wanashindwa hata kujiendeleza kwa kutumia hatimiliki ya nyumba zao walizonazo kupata mikopo kwa ajili ya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiuliza kwa nini hilo linakuwa ni tatizo, swali kubwa utajibiwa huko kwenye Idara zetu za ardhi kwamba ramani haijapitishwa. Hilo ndio jibu ambalo ni la haraka haraka tu ambalo wananchi wanapewa. Ukifika kwenye Idara ya Ardhi, ukidai hatimiliki, basi utaambiwa au wananchi wataambiwa kwamba ramani haijapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli hapa nashindwa kuelewa kwa sababu viwanja hivi vinapimwa, mwananchi anaomba anapewa anachukuwa ramani yake ya jengo anaipeleke kwenye Halmashauri aidha ya Wilaya au Mji mdogo au ya Jiji, ramani yake ya jengo inapitishwa kwamba anaweza akajenga, lakini bado hatimiliki unaambiwa ramani haijapitishwa. Hapa mimi napata utata mkubwa.

Hivi inakuwaje mtu anajenga jengo la gharama kubwa lakini hana hatimiliki? Lakini huyu ambaye ana kiwanja kitupu kilichoota majani, wala hana mwelekeo wa kujenga kwa sababu yoyote ile ambayo anayo mwenyewe ana hatimiliki, iko sandukuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kupitia kwako, mimi ningeomba hili suala pamoja na jitihada nzuri ya Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake na Naibu Waziri, hebu waone ile njia waliyotumia kuweza kupata pesa za mkopo kutayarisha viwanja vipya, kutayarisha hatimiliki za viwanja vipya, basi wafanye haraka. Najua jitihada zipo, lakini jitihada hizo zinachukua muda mrefu mno na unafika mahali unaona kwamba inakuwaje anapata huduma mtu wa sasa hivi wakati yule mtu wa zamani bado yupo kwenye msongamano wa kusema kwamba bado hawezi kupata haki yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa Wizara hii, kwa jitihada zake, mengi ni ya kuwapongeza, lakini nitawapongeza zaidi na nina hakika watapata dua za watu wengi zaidi kama hawa watu ambao wana nyumba za zamani kwa mfano eneo la Ngamiani Tanga.

Ngamiani ni Mji wa zamani sana. Lakini kuna majumba pale watu hawana hatimiliki, ukienda Dar es Salaam kuna maeneo vile vile ambayo ni wazee wetu tangu babu zetu wana nyumba pale watoto wamerithi, wajukuu wamerithi, lakini bado unaambiwa huyu mtu hawezi kupata hatimiliki kwa ajili ya ramani haijapitishwa.

Najua humu kwenye hotuba yamo mengi tu yameandaliwa lakini nasema twende mbio badala ya kutembea. Twende mbio kwa sababu bado wananchi wanataka maendeleo na hakuna maendeleo bila ya ardhi na hakuna ardhi yenye thamani bila ya kuwa na hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ulikuwa ndio msisitizo wangu na nisingependa kuwachafulia kwa kuwapa mambo mengi ambayo mengi wameyafanya na

wanaendelea kuyafanya, ila tu kuwatakia kila la kheri na haya ambayo wanategemea kuyafanya na yale ambayo bado wana nia ya kuyafanya, wayafanye kwa jitihada zaidi na kwa haraka zaidi ili wananchi wote walio Bara, Pwani na walio Mijini na Vijijini wafaidike na ardhi yao ambayo ndio maliasili. Hapo ndio watakapoweza kuwaondolea umasikini wananchi kwa kupata hatimiliki ambazo zinaweza zikawapatia mikopo kama dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba, kwa kuwa leo ninaamini itakuwa ni siku yangu ya mwisho kuchangia katika kipindi hiki cha Bunge cha miaka mitano, kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti ambao walikuwa wakituongoza humu ndani katika kuendesha majadiliano ambayo tunatakiwa kujadiliana kwa taratibu.

Lakini pia, kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ambayo nimeihudumia, Mheshimiwa Mgana Msindai katika Kamati ya *LAAC* na Wajumbe wenzangu wote ambao tumeshirikiana kuisadia Serikali, kuishauri katika yale ambayo tulikuwa tukiletewa kwenye Kamati yetu.

Ni mategemeo yangu kwamba wote kwa nguvu za Mwenyezi Mungu tutarudi, mimi nina imani tutarudi kuanzia Naibu Spika, Mawaziri wote, Wenyeviti wote na nina hakika kabisa Wabunge wote wa CCM wale ambao wanaitakia mema nchi yetu, basi watarudi na nina hakika wote tunaitakia mema. Lakini kwa wale ambao kila siku hata kama vitu vipo hawaoni, vitu vinasemwa hawasikii, basi Mungu naye awaangalie katika hali hiyo hiyo kwamba na wao wasionwe wala wasisikiwe watakapoomba kura za wananchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Mimi kwa kweli nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na mama mahiri kabisa, Mama Sijaona. Mimi kwa sababu nimekuwa karibu sana na Wizara hii, naweza nikathibitisha utendaji mzuri wa Wizara hii kwa miaka hii mitano na kwa kweli wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yamefanyika katika Wizara hii hasa katika suala la kuboresha utendaji wa Wizara kwa ujumla, kupunguza rushwa, kuingiza teknolojia ambayo kwa kweli imeharakisha sana utoaji wa huduma za masuala ya ardhi na hati katika suala la upimaji wa viwanja. Sisi wakazi wa Dar es Salaam na mimi tukizungumzia kwenye Jimbo langu la Ukonga ambako viwanja katika ule mradi wa viwanja 20,000 vimepimwa, sisi ni mashahidi wa kazi nzuri iliyofanywa katika suala hili la viwanja 20,000 na mimi nimekuwa mtetezi wa mradi huu toka mwanzo hadi sasa.

Lakini vilevile, miradi ya kurasimisha makazi ya nyumba, miradi ambayo inaendelea, kwa kweli ni suala ambalo ni la kupongezwa na wengi tumekuwa tukilizungumzia ingawaje tulikuwa tunatumia lugha ya *regularization.* Lakini ndio hiyo hiyo kurasimisha kwa Kiingereza.

Lakini vilevile, siyo Wizara tu, wamesaidiwa na Mashirika mengine kama *UN-HABITAT* na Benki ya Dunia na mimi nalitolea ushahidi kwa sababu nimekuwa mtaalam katika mradi wa Benki ya Dunia ya kuboresha makazi katika Jiji la Dar es Salaam maeneo ya Buguruni, Manzese na kule Keko. Kwa hiyo, naelewa kwa sababu nami niko ndani ya ule mradi. Yote hayo kwa kweli ni juhudi za Wizara hii.

Vilevile, kwa kipekee nilipongeze Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mimi nimekuwa kwenye lile Shirika kama Mkurugenzi wa Fedha na Utawala kwa miaka sita, najua sana utendaji wake, najua sana matatizo yaliyokuwepo. Lakini nilishukuru sana Bunge lako kwa kupitisha Sheria ya kubadilisha ile Sheria ya Kodi ya Upangaji. Kwa kweli sheria ile kwa kubadilishwa kwake kutaboresha utendaji wa Shirika na mapato ya Shirika kwa ujumla ili Shirika lifanye kazi kibiashara. Suala lile nimepigia kelele bado nikiwa pale na hatimaye hili limetimia na kwa kweli ninapongeza sana Serikali na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ambavyo nimependekeza huko nyuma, bado mimi naendelea kupendekeza kwamba kuna haja ya baadhi ya Idara katika Wizara ya Ardhi zikaunganishwa na Shirika la Nyumba tukawa na *Agency* ambayo nimekuwa nikiita *National Lands and Housing Development Agency* ya kushughulikia maendeleo ya ardhi na makazi katika Miji yetu.

Mimi nasema hivi, ili Shirika hili lifanye kazi yake vizuri, lingepewa majukumu mahsusi ya kuendeleza maeneo ya makazi kama *Agency* na ikatumika ile Sheria ya *Agency* ambayo ilipitishwa hapa Bungeni hapo mwaka 1997. Kwa kweli nchi nyingine kama Tunisia zimefanikiwa sana kwa kuwa na *Agencies* kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine mimi ningeshauri kwamba suala la ujenzi wa nyumba, liwe kwenye Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Sasa hivi tunaona kwamba kuna suala la nyumba kwenye Wizara ya Ujenzi. Mimi naona kwamba kuna tatizo hapo. Mheshimiwa John Magufuli rafiki yangu aachiwe kujenga barabara na suala la nyumba aachiwe Mheshimiwa Gideon Cheyo ajenge nyumba na ajenge nyumba zote za Watumishi wa Umma na wasio Watumishi wa Umma, kwa sababu wote ni Watanzania.

Watumishi kwenye Sekta ya Mashirika ya Umma ni Watanzania wanatoa kodi, hata wale wanaofanya kazi kwenye sekta binafsi. Kwa hiyo, suala la nyumba kuwekwa kipande kwenye Wizara ya Ujenzi, mimi naona si sahihi lingewekwa kwa pamoja. Huu ni ushauri wa bure kabisa kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Pia, nije kwenye suala la la mikopo ya nyumba ili wananchi wajenge nyumba zao. Suala hili la mikopo ya ujenzi wa nyumba mimi naweza nikasema nimekuwa nikilizungumza hapa mara nyingi na niseme kabisa kwamba nilipoingia hapa Bungeni

mara ya kwanza nimezungumzia suala hili. Hotuba yangu ya kwanza ndani ya Bunge tarehe 2 Februari, 2001 ilikuwa juu ya suala la kuwa na vyombo vya kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na hasa nyumba kwa watu ambao hawana vipato vikubwa au watu masikini.

Pia, imekuwa bahati nzuri kama Mheshimiwa Spika hatanipa nafasi nyingine katika kipindi hiki, labda leo tena itakuwa ni mara ya mwisho kuzungumza katika Bunge hili la miaka mitano, nitazungumza katika Bunge linalokuja kwa sababu nina hakika wanaukonga watanirudisha. Lakini katika kipindi hiki cha miaka mitano, nasema nimeanza kuzungumzia suala hili na si ajabu nitamalizia leo kwa kuzungumzia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba katika watu wawili katika nchi hii ambao wamekuwa wakizungumzia kwa uchungu sana suala hili kwa miaka yote hii 10, ninaweza nikasema, suala la vyombo vya kutoa mikopo ya nyumba ni Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. Mimi naweza kusema watu hawa wawili wamezungumzia sana suala hili kiasi kwamba imekuwa sasa ni wimbo wao.

Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa maagizo, baadaye akaanza kutoa wito, akatoa rai, akatoa maombi kwamba jamani tunafanyeje ili watu wetu waweze kupata mikopo ya kujenga nyumba waweze kuishi na Mheshimiwa hata juzi kuacha jana, ameendelea kutoa rai kwa mabenki kutoa mikopo au kuingia kwenye ujenzi wa nyumba kwa ajili ya watu masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimelizungumzia hili suala kama nilivyosema ndani ya Bunge hili karibu mara sita. Tarehe 2 Februari kama nilivyosema, mwaka 2001 nimelizungumzia suala hili humu ndani, tarehe 23 Julai, 2001 nimezungumzia suala hili katika kuchangia hotuba ya Wizara hii, tarehe 15 Julai, 2002 nimechangia tena suala hili la mikopo ya nyumba nikichangia Wizara hii, tarehe 18 Julai, 2003 nimechangia tena, lakini tarehe 23 Julai, 2003 wakati nachangia katika Wizara ya kuondoa umasikini katika Ofisi ya Makamu wa Rais nimelizungumzia tena na hata mwaka jana 2004 nimeuliza swali tarehe 30 mwezi wa saba kuulizia kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nasema nimelizungumzia hili suala ndani ya Bunge kwa kipindi kirefu na siyo hivyo tu, hata kabla ya sijaingia Bungeni nimelizungumzia hili suala na kushiriki katika kutoa mapendekezo. Mimi katika *Thesis* yangu ya *Degree* ya pili nimefanya katika masuala ya mikopo ya nyumba. Lakini hata kwenye *Thesis* ya *Degree* ya tatu ya *Ph.D* utafiti wangu pamoja na kwamba ule ulikuwa kwenye umaskini wa nyumba kwa ujumla, lakini suala la mikopo ya nyumba nimelizungumzia kidogo.

Nikiwa *National Housing* toka mwaka 1995 tumelizungumzia suala hili, nimetoa mapendekezo yangu, lakina hata baada ya pale nilipokuwa Mbunge nimeandika *papers* nyingi na hapa nimshukuru sana Prof. Tibaijuka wa *UN-HABITAT* ambaye ameniwezesha zaidi ya mara mbili kwenda nchi za nje kutoa mada kuhusu suala la mikopo ya nyumba.

Nimekwenda China mwaka 2002 amenirudisha tena pale mwaka 2003. Pamoja na kwamba Tanzania haina mfumo huo, lakini nimekuwa mstari wa mbele kupendekeza na wananchi na watu wengine katika nchi nyingine ambazo wameshiriki katika *conference* zile wamekubali. Lakini Wizara ya Ardhi yenyewe kwa kutambua mchango wangu nimekuwa *facilitator* katika kuzungumzia ni namna gani nchi hii inaweza kuwa na *National Housing Finance Program*. Tumefanya ile kazi nikiwa mimi *facilitator,* sasa sijui ule mpango umeishia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema suala hili limezungumziwa sana siyo mimi tu, wataalam wengi sana, *UN-HABITAT* yenyewe imeshiriki katika kusaidia nchi hii kupendekeza namna gani tunaweza tukafanya watu wakapata mikopo ya nyumba; *Shelter Afrique,* mimi nikiwa *National Housing* tumeshirikiana nao wametoa ripoti nzuri sana, wamekuja wataalam wengine kutoka nje kina Dr. Daimond tumeshirikiana nao pale *National Housing* wataalam wa Chuo cha *UCLAS* wametoa mapendekezo mengi. Lakini wapo vilevile wataalam wengi wengine ambao wametoa namna gani tunaweza tukaboresha hali katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme kwamba hatua ambazo zimechukuliwa na nchi nyingi pamoja na Tanzania za kuhusisha Serikali kuu, Serikali za Mitaa au Sekta binafsi au Mashirika ya Kimataifa, hizi *development Agencies.* bado juhudi hizi zimeshindikana kwa sababu upande wa Serikali Kuu uwezo umekuwa mdogo kuweza kuweka mfumo wa kujengea wananchi nyumba zao na kuweka vyombo vya mikopo.

Lakini Serikali za Mitaa zimekuwa hazina uwezo vilevile kama ilivyo Serikali Kuu, wameshiriki zaidi kwenye miundombinu, sekta binafsi wao wanaangalia faida zaidi. Kwa kweli hawana sababu ya kwenda kwenye Sekta ya Nyumba kwa ajili ya watu maskini. Mashirika ya Kimataifa na wenyewe wamekuwa zaidi wanasema Sekta hii *is not productive investment,* kwa hiyo, wamekuwa wanashughulikia masuala mengine zaidi na *focus* yao imekuwa ikienda Vijijini. Kwa hiyo, kama mikakati hii imeshindwa, ni namna gani tunaweza tukaweka mikakati ya kuboresha au ya kuwezesha wananchi wetu na hasa masikini wakijenga nyumba zao, kwa sababu uwezo wa kupata mikopo katika mabenki ya kawaida imekuwa ni migumu na sekta binafsi hapa nimezungumzia ni pamoja na mabenki ambayo kuingia kwenye kutoa mikopo ya nyumba kwa watu maskini wanaona wanaweza wakapata hasara. Sasa tunafanyaje? Nitoe tena ushauri wa bure kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja na ndivyo kwa kweli inavyozungumzwa duniani kote, kwamba tuangalie wao watu maskini tuwahusishe zaidi kuliko kuangalia *program* ambazo zinatengenezwa katika *level* ya Serikali au watu wa nje. Tuanzishe vitu ambavyo vinaitwa *Community Mortgage Programs* kwa mfano, au *Cooperative Housing* na ikiwezekana kama Serikali inataka kusaidia ianzishe *Housing and Servings Bank* ambayo itakuwa kwa ajili hii. *(Makofi)*

Hii ya Mheshimiwa Rais kuomba *Citi Bank* waanzishe na *Bank* nyingine inaweza ikasaidia. Lakini kwa kweli wao kwa sababu wanakwenda kwenye faida zaidi, ni ngumu

na baada ya kufanya vile Serikali isaidie katika kuanzisha *Cooperative Housing Associations* pamoja na *Community Associations* ili wananchi katika maeneo yao waanzishe ujenzi wa nyumba watafute viwanja kwa kutumia hizi *Cooperative Associations* na hawa ndio watakaokuwa wanakopa kutoka Benki kama *Association* na wao wana wa-*tie down* sasa wale *Community Members* wale ili waweze kujenga nyumba zao na kurudisha mikopo kupitia kwenye *Association* zao.

Kwa hiyo, suala la ushirika wa nyumba ni suala ambalo tumeliacha lakini ndilo linaweza kutusaidia na hasa kwa watu masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilifanya hilo la kupeleka nguvu zetu kuhamasisha uanzishwaji wa *Community Mortgage Programs* kuanzisha *Housing Cooperative Associations* na sasa hizo *associations* zi-*mobilize funds,* zikope kutoka kwenye *Housing and Servings Bank* tutakayokuwa tumeianzisha makusudi ndipo tunaweza tukafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize na mimi kwa kuwashukuru sana wananchi wangu na Wapigakura wa Jimbo la Ukonga ambao kwa miaka mitano wamenipa ushirikiano mkubwa sana, Jimbo ambalo lina watu wengi kuliko Majimbo yote Tanzania, lakini maendeleo tuliyoyafanya niliyoyafuatilia wao wenyewe ni mashahidi michango yangu ndani ya Bunge na ndani ya Jimbo la Ukonga yamewafanya mpaka sasa wananiita Mzee wa *Tsunami*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja kwa kwamba wapo wanaojaribu kupitapita, hata wao wenyewe wanasema huyu Mzee wa *Tsunami* tutamuweza? Wananchi wanawaambia jaribuni tu, karibuni kwa sababu ni demokrasia. Lakini kwa kweli Mzee wa *Tsunami* kwa kazi aliyoifanya kwenye Jimbo la Ukonga na aliyofanya ndani ya Bunge, kwa kweli itakuwa ni ndoto kumng'oa na mimi hili nawaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo katika kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Vilevile, ninaomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Makamishna wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Napenda niungane na wenzangu walionitangulia kwa kusema kwa wazi kabisa kwamba Waziri wa Ardhi ni mtu hodari kabisa, anafanya kazi yake akiwa *serious* na kwa uadilifu mkubwa. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia tusisahau kwamba anahitaji pongezi nyingine humu Bungeni. Hakuna anayeongoza kukaa hapa Bungeni vizuri kama Waziri wa Ardhi. Kama kungekuwa na suala la nishani, nadhani angestahili nishani ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze vilevile Bibi Salome Sijaona, si kwa sababu ni mwanamke, lakini kwa kweli kazi yake ni nzuri sana, anahitaji pongezi. Yuko *serious* na anataka mambo yake aliyoyapanga yaweze kufanikiwa. Ukiangalia suala la rushwa kama mchangiaji mwingine alivyogusia kwa kweli pale Wizarani wamejitahidi.

Ukiangalia suala zima la upimaji na ugawaji wa viwanja, wamefanya vizuri na watu wamesifia sana. Ukiangalia hata suala zima la ku-*speed up* mambo ya utoaji wa hati wamejitahidi sana na hakuna usumbufu mkubwa ambao mtu unaweza kuupata katika kufuatilia. Lakini vilevile wamekuwa wakihimiza watu waweze kulipia viwanja wanavyomiliki. Hivi sasa kila mtu anafahamu kwamba akipatiwa kiwanja lazima akilipie kwa wakati tofauti na huko nyuma watu walikuwa wanalegealegea tu.

Kwa hiyo, nawapongeza sana Wizara kwa ufuatiliaji mzuri walionao. Ninapenda nigusie la kwanza kuhusu suala la utoaji miliki za ardhi. Napongeza kwa hatua ambayo zimeshachukuliwa na Wizara kwa kuanza kuwanyang'anya wale wote ambao hawaendelezi maeneo waliyopewa. Mimi ni shahidi kwamba kuna watu ambao wamepewa viwanja kwa zaidi ya miaka 10 mpaka 15 kwa ajili ya makazi na vingine kwa ajili ya uwekezaji, mpaka leo havijafanyiwa kazi. Kuna mapori, kuna uchafu, kuna watu ambao wanajificha huko na Halmashauri zetu kama tujuavyo si Halmashauri zote ambazo ziko makini katika masuala ya usafi. Kwa hiyo, hali iliyoko katika Miji yetu ni mbaya.

Sasa mimi kazi waliyoanza kuifanya ya kuanza kuharakisha utoaji au unyang'anyaji wa hatimiliki mimi naupongeza sana, lakini naomba waendelee kulegeza haya masharti ya namna ya kunyang'anya maeneo ambayo yanakaa bila kuendelezwa. Kwa sababu ukipeleka maombi ya kuomba kubatilisha hatimiliki katika viwanja inachukua muda mrefu sana.

Inawezekana kabisa katika kuandaa hizi sheria tulikuwa tunaangalia kwamba kuna watu maskini ambao hawawezi kujenga haraka, lakini mpaka sasa kuna maskini wengine wanataka kuendeleza kwa kujenga. Kwa nini hao maskini ambao wanataka kuendeleza, amehifadhi hela yake, ametunza vizuri, kwa nini asipewe nafasi ya kumiliki ardhi kwa wakati na anaona kabisa kuna ardhi ambayo inakaa bila kuendelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nielezee kidogo kuhusu usimamizi wa ardhi katika Mikoa na Wilaya. Sheria ya Ardhi na kanuni zake zinazungumzia Halmashauri za Wilaya na Miji, Wizara na Ardhi, hakuna maeneo ya wazi yanayozungumzia suala la Mikoa kwa maana ya Serikali Mikoa na Wilaya. Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya wanazungumziwa katika kipengele Na. 13 cha kanuni cha *The Land Allocation Committee Regulations* ya mwaka 2001. Uwajibikaji wa kugawa viwanja na ardhi ndani ya Halmashauri za Wilaya na Miji kipengele hicho kinasema kama kifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu. Kinasema hivi: "*The Role of the RC and the DC in relation to allocation Committees within their areas of Jurisdiction shall be to investigate the illegality when questioned of actions and decisions of such Committees shall inform the Minister of Lands accordingly or take appropriate action required*." Huu ndiyo mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi za *Regional Secretariat* ni kuunganisha shughuli za Wizara, shughuli za Mikoa na shughuli za Halmashauri za Wilaya na Miji hasa katika mambo yanayohusiana na sera na sheria na hasa inapotokea suala la tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za Wizara ya Ardhi hazifuati mwongozo huu wa kuangalia kwamba *Regional Secretariats* zinafanya kazi zake. Kwa mfano, wataalam waliosajiliwa na hata wale wateule shughuli zao zote za mawasiliano kutoka Wilayani kwenye Miji au kwenye Halmashauri za Wilaya zinakwenda moja kwa moja Wizarani hasa inapohusiana na masuala ya *Allocations of Land.* Moja ya kazi za Mikoa na Wilaya ni kushughulikia malalamiko ambayo Mheshimiwa Waziri atakuwa ameyapata kutokanana na hayo maamuzi yaliyofanywa na Miji au Wilaya yanayopelekwa kwa Waziri.

Naye Waziri kwa sababu ameletewa atamtaka Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya ashughulikie malalamiko ambayo Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya hana taarifa nayo. Unafanya nini hapo?

Kwa hiyo, utaratibu huu mimi nafikiri uzingatiwe vizuri wa kuhakikisha kwamba hizi *Secretariat* au Mikoa kwa ujumla wake na zenyewe zipate nafasi ya kujua ni nini kimefanyika na Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji ili inapotokea malalamiko yameletwa kutoka Wizarani, basi katika Mkoa au Wilaya, Serikali Kuu ipate picha kamili ya nini kilitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa natoa kama ushauri na vilevile kama changamoto kwa Wizara kwa sababu Wizara nyingine au Sekta nyingine kama Elimu au Kilimo, *Secretariat* huwa inajua kwamba Wilaya au Halmashauri wanatakiwa kufanya nini au wameagizwa kufanya nini na Wizara Mama.

Kwenye Wizara hii kuna hii *breakdown* ambayo kwa kweli linakosekana jambo ambalo linaleta matatizo. Wananchi wanapofuatilia Mkoani kwa Mkuu wa Mkoa au kwa Mkuu wa Wilaya malalamiko yake wanaona kwamba hakuna mawasiliano ambayo yamefanyika. Kwa hiyo, anachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile na mimi niungane na Mheshimiwa Milton Mahanga kutoa pongezi kwa Wizara au Serikali kwa ujumla kwa kushughulikia hizi sheria zinazokwamisha utendaji kazi wa *National Housing Cooperation* au Shirika la Nyumba la Taifa. Ni kweli kabisa tumeshuhudia na tumeona watu ambao kwa makusudi kabisa wamepewa nyumba za kuishi, lakini hawataki kulipa kodi kwa sababu eti sheria inamlinda. Unatazamia *National Housing* ifanye kazi namna gani? Haiwezi hata kidogo. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, ambaye alizungumza kuhusu sheria hii na kuhakikisha kwamba inaletwa Bungeni, mimi naipongeza sana ile Kamati. La sivyo tungeendelea kuona kwamba Shirika linakufa kwa sababu kuna mtu anasema analindwa na Sheria. Matokeo yake ni kama hayo tunayoyaona, Miji ni michafu, *National Housing* hawawezi kukarabati hata majengo.

Unapozungumzia usafi wa Miji ni pamoja na usafi wa majengo yaliyopo na mengi ya majengo haya ni majengo ya *National Housing,* sasa ni machafu, hawana hela kwa sababu mtu mmoja hataki kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo Waziri ametoa hapa maagizo kwa wapangaji kwamba sasa wawe makini katika kulipa na mimi naungana naye asilimia mia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, baada ya kuzungumza hayo machache, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Naibu Spika kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya katika muda huo wa miaka mitano. Lakini ninyi mmekuwapo hapa kwa sababu sisi tuliwachagua kama Wabunge na sisi Wabunge tunajipongeza kwa sababu tuliwachagua ninyi mnaofaa.

Hata hivyo, tunafikiri kwamba mtaendelea kudumu katika afya zenu na Mungu awajalie labda mtakwenda kugombea Ubunge, Mungu awasaidie mweze kurudi tena hapa Bungeni.

Nami vilevile nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Mbeya ambao walinileta hapa, nimeshirikiana nao vizuri sana, wamerahisisha kazi zangu sana na kuniwezesha kuwa Mbunge mzuri katika kuwawakilisha hapa Bungeni. Kwa hiyo, nawashukuru sana na wao nawatakia afya njema na ninawatakia maandalizi mazuri kabisa katika Uchaguzi Mkuu ujao ili wasije wakafanya makosa katika kuchagua mtu ambaye wanashirikiana naye vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunivumilia na kunisikiliza. Ninapenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba nijihusishe na pongezi zote zilizotolewa kwa Wizara hii kwa maana ya Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii.

Katika kukaa kwangu Bungeni, Wizara ya Ardhi ilikuwa moja kati ya Wizara iliyokuwa inaonekana kama jinamizi. Ilikuwa inaonekana kama Wizara moja *impossible,* haiwezekani wala watu walikuwa hawawezi kuona hasa kazi yake ni nini na sana ilikuwa inaji – *associate* tu na rushwa na uuzaji wa viwanja na kugawana viwanja na kugombana ndani ya viwanja.

Lakini kwa miaka hii ya karibuni Wizara hii imeanza kujionyesha kabisa ni nini Wizara inapaswa kufanya na nini kinawafikia wananchi. Kwa hiyo, ndiyo maana

nadhani sasa hata wote tunaiona Wizara ya Ardhi kama Wizara iliyo rahisi kuifikiria au kuiona. Kwa hiyo, pongezi kama walivyosema wenzangu ni za kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sitapenda kuzunguka. Mimi nataka nieleze jambo moja. Wakati wote tunazungumzia habari ya MKUKUTA na wengine wameweza hata kuita MKUKUTA kama ni kitu fulani lakini ni mpango rasmi wa kiserikali ambao unahusu wananchi kupambana na umaskini. Ni mpango rasmi wa Serikali.

Kwa wale ambao wanafuatilia, kuna haya malengo ya ulimwengu ambayo yanapaswa kutekelewa katika miaka ya 2020 mpaka 2025 MDGs, lakini MKUKUTA tunaweza kusema ni Mpango Mkakati wa Tanzania *specific* eneo lake kubwa ni hili la kupambana na umaskini kwa ngazi ya wananchi wa kawaida. Hakuna mtu anayeweza kupambana na umaskini bila kuwa na kitu au *asset* au mali na mali kubwa ni ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Mheshimiwa Rais ameniweka kuwa Mwenyekiti wa kitu kingine tunaita MKURABITA. MKURABITA ni sehemu tu ya mkakati wa kuondoa umaskini (MKUKUTA) na katika MKURABITA, kuna maeneo matatu tu ambayo unapozungumzia MKURABITA ni lazima uyatambue. Moja linaitwa ni Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za wananchi tena, tunaita Wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako Tukufu tulipofanya Semina Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba neno wanyonge liondoke, baada ya kutathmini na kuona kwa nini limetumika neno wanyonge tunasema neno hilo libaki.

Wanyonge kwa sababu gani? Nchi ya Tanzania sasa kama mtakavyoona ni nchi kubwa, Miji yetu ni mikubwa. Ukitaka kujua kama Tanzania ni nchi ambayo iko shaghalabaghala kimipango yake, wewe usafiri kwenye ndege usiku ufike hapa Dar es Salaam usiku. Hutaona Mtaa wa taa wala Mtaa wa kitu chochote. Yaani unaona tu taa zinawaka kila mahali. Hii ni kuonyesha kwamba Mji huu haujapimwa kitu chochote ni vurugu Dar es Salaam na Miji yake mingine. Ninyi mliowahi kusafiri na ndege usiku unapotua utaona taa zilivyozagaa kila mahali na hujulikani unapita wapi wala wapi.

Hiyo ni kwamba Dar es Salaam peke yake na sehemu nyingine kuna mali kubwa kabisa katika nchi hii kuliko hata fedha zote tunazopewa na wafadhili ambayo haina kazi. Ndiyo humu ndani ya Kitabu Waziri anasema Mali mfu.

Katika kazi ya MKURABITA tumefanya tathmini za mwanzo, mali ambazo zipo Tanzania katika Mikoa 10 tu na Wilaya 17 tu iliyofanyiwa kazi, kuna mali ya mabilioni 12 *USD* ambayo ni mfu. Waheshimiwa ninyi mnalala kwenye majumba yenu yote mnajua kulala tu afadhali hata kaburi unajizika basi. Lakini unalala katika nyumba ambayo haina faida yoyote kwako, nyumba ya thamani ya mamilioni lakini unalala wewe tu bado maskini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanyonge hapa siyo kwamba wenyewe ni maskini hawana mikono wala nini, ni wanyonge. Sisi wote tumelalia mali zetu, hatuna kitu chochote, ni wanyonge, huwezi kukopa Benki wala huwezi kufanya chochote. Ndiyo unyonge

wenyewe huo kwa asilimia karibu yote ya Watanzania ni wanyonge tu kwa maana hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wizara hii ilichokifanya ni kuanza sasa kwa hatua, nasema za kinyongenyonge na zenyewe kuanza kupimapima zile *squatters* za Manzese. Wanachokifanya, wanapima zile *squatters* halafu wanatoa namba ya yule mtu mwenye nyumba anapewa thamani ya kile kieneo kama ni milioni tatu na yeye anashangaa kha! Kumbe mimi ninamokaa humu ni milioni hizi zote. Sasa huyu siyo tu anapimiwa tu, yeye jina lake linaingia katika nafasi ya ki-*official,* yaani katika taarifa rasmi kwamba huyu ni Bin fulani mwenye eneo hili dogo lakini lina thamani hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale wenye fedha wanaanza kusema aha! Huyu Bin fulani, amina! Ametambuliwa na chombo kinachotambuliwa, kwa hiyo, wanaona rahisi kumkopesha. Sasa hilo ndilo linalozungumzwa kuwa tutumie ardhi yetu kuondoa umasikini.

Sasa kwa asilimia kubwa, majumba yote yale kule mnaita Mbezi - Dar es Salaam yote yale siyo mali ni *dead capital* au malimfu. Sasa tatizo tulilonalo sisi, Wizara hii imejitahidi kufanya hivi, kumtambua huyu mtu na eneo lake na thamani ya mali yake. Lakini inahitaji utambuzi huu usifanywe na Wizara hii peke yake, inatakiwa kwanza hata Serikali yenyewe na Waziri wa Mambo ya Ndani itoe vitambulisho vya raia.

Sisi Watanzania mafundi kweli. Leo naitwa Anne Makinda, nikiona nimezidiwa nabadilisha, nasema Anne Semamba, sasa Anne Makinda na Anne Semamba mbona wanaonekana watu wawili? Nikitaka kukwepa jambo fulani lazima nibadilishe jina kwa sababu hakuna kitambulisho halali kinachotambuliwa na nchi nzima kwamba leo Anne Semamba Makinda ni mimi, iwe nife ni mimi lakini vitambulisho hakuna.

Kwa hiyo, ndiyo maana nataka niipongeze Serikali kwa mpango wake wa kutafuta vitambulisho na ninaomba hii ifanyike haraka isiwe kama alivyosema Waziri wa Mambo ya Ndani, tunafanya nini sijui, tunafanya tathmini ya gharama! Tuifanye hii kwa sababu kwa kutokuifanya mnazidi kuwafanya Watanzania wawe maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Benki itakayokukubali wewe. Labda sisi tunajitambulisha kwa sababu ni Waheshimiwa Wabunge na ikifika miaka hii kama kesho ya uchaguzi wanadai kila kitu ulichokikopa wanakidai kwa sababu hawajui ukitoka hapo utakuwa mwingine, utakuwa Anne Semamba.

Kwa hiyo, tunahitaji vitambulisho. Lakini pia tunahitaji anuani ya mtu anapokaa. Kuna neno wanaita *Physical Address*. Sisi hatuna *Physical Address*. Hata mwambiwe *Physical Address,* mimi *Physical Address* kule Kijitonyama mbona siijui? Ikitokea kama unapiga simu unataka kwenda Hospitali nina mgonjwa hapa huwezi ukapiga simu ukamwelekeza mtu akafika. Hawezi kufika kwa sababu hakuna *Physical Address.*

Kwa hiyo, Wizara hii inachojaribu kufanya sasa ni kupima hizo mali lakini watapata tatizo la *Physical Address* kwa sababu tulishajenga kiholela siku nyingi, mtu

anajenga choo mbele ya nyumba ya mwenzake, ukipata tatizo la moto huwezi kuita gari la Zimamoto likafika pale. Haliwezi kufika, litapita wapi? Kwa hiyo, neno *Physical Address* ni muhimu.

Sasa basi Miji mingi iko katika hali hiyo, nadhani karibu yote labda hivyo viwanja 20 au 30 vinavyopimwa sasa na utakuta kwamba kwa nguvu ya Wizara hii kujaribu kutengeneza Mitaa na *Physical Addresses* kwa hali waliyonayo sasa, hawataweza kwa sababu wakati wanajitahidi kufanya hayo wanayofanya sasa, lakini Miji inaendelea kukua haraka. Inakua kiholela kabisa.

Kuna Vijiji sasa vinakuwa Miji, kuna Miji inakuwa Majiji, kuna Wilaya mpya zilizopatikana hazina *addresses* wala hakuna namna, hakuna uwezo wa Wizara hii, ki-*man power* haitoshi. Fedha wanazopewa hazitoshi, hata hao watu wa Benki ya Dunia wamejitahidi kuwasaidia lakini bado hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza *seriously* hatuwezi kuendelea namna hii. Hatuwezi kupambana na umaskini kwa mtindo huu wa kubaki tunajenga jenga ili mradi tu. Rafiki yangu Mbunge wa Ukonga ameeleza kwamba kungekuwepo na *cooperative* ya kujenga nyumba, mimi nasema *fare*. Lakini tuwe na *Master Plan* ya Miji yetu. Miji yetu iwe na ramani, yaani *Master Plan*. Sasa kama nilivyosema, uwezo wa Wizara hii pamoja na bidii zao zote bado ni mdogo.

Mimi nilifikiri kwamba kwa sababu tuna wataalam wazuri sana katika nchi yetu hususan ndani ya Wizara hii na Vyuo vyetu vile vya *UCLAS* na vingine vya ardhi vilivyotajwa humu, mimi nadhani tukae pamoja, pamoja na bidii hizi mnazofanya mbuni njia iliyo rahisi zaidi angalau ya kupima *preliminary survey,* halafu baadaye mpime kitaalam kusudi watu wasiendelee kupanua Miji yao bila utaratibu kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa kama haya ya kipindupindu hayawezi kukoma kwa mtindo huu. Maana kungekuwa na utaratibu wa Miji iliyopimwa, *Master Plan,* basi maji machafu yanajulikana yanakwenda wapi na bomba zinakwenda wapi. Lakini hatuwezi kufanya hivyo! Lazima tufanye *operation* kwanza ya kujaribu kuiweka Miji yetu katika hali nzuri halafu hizo *Proper Master Plan* ziendelee baadaye, lakini tuweze kuzuia uendeleaji wa Miji kuwa bila mipango inayostahili. Hili litatugharimu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba hizi *dead capital* ,Wizara inajitahidi na ni sehemu muhimu sana kwa MKURABITA hili suala la kuweza kuwagawia wananchi hati zao na waweze kukopa. Mabenki yana kigugumizi kwa sababu sisi hatuna *National Identity* na hizo mali kwa hiyo, kwa mtindo huo zikiweza kuthaminiwa na mtu anayetambulika, ndipo Benki wanakubali. Tena ipo dhana kwamba hata hati nyingine za kawaida zile za zamani hawazikubali sana kwa kuwa hazina uhakika.

Mimi nina hatimiliki, lakini akajenga mwanangu nyumba, akikopa mikopo kutumia ile hatimiliki akifika jina la kwangu mimi, nasema mnaninyang'anya kiwanja changu, mimi simtambui huyu, unaona! Bado kabisa Benki wanapata matatizo. Lakini tukienda kwa pamoja na kushirikiana na kuwa wabunifu zaidi kwenda mbali zaidi kuwa na *Master Plan* na *identification* zetu tupate na *Physical Address,* yaani anuani rasmi ya mtu, mimi nadhani Benki zetu zitabadilika, zitawakopesha Watanzania na Watanzania wale wabunifu watafanya shughuli zao kwa kutumia hela zilizoko kwenye Benki bila tatizo lolote lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, naomba Wizara iendelee na haya lakini Waheshimiwa Wabunge mtakaporudi Bungeni hapa, moja ya eneo la kulipigia kelele ni hili. Hatuwezi kuondoa umaskini bila mali zetu kuwa na thamani ya kuweza kukopesheka.

Kwa hiyo, ninyi wote naomba mrudi kwa kuwa mnafahamu haya mambo kusudi tupitishe sheria za mwanzo mwanzo tu kuweza kuraslimisha mali za wananchi wa Tanzania na tuweze kutumia mali zetu wenyewe kuweza kufanikiwa kujiendeshea maisha yetu vizuri zaidi kuliko kulalia nyumba ambazo sisi wenyewe ni mfu na mali inakuwa mfu, tunalilia umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitoe yale ninayoyaona katika Wizara yetu hii.

Kwanza kabisa napenda niishukuru sana Wizara hii na hasa kwa Wilaya yangu ilikowezesha hatimiliki za kimila zimepatikana na kwa watu wengi na zimetusaidia sana hasa kujenga utu wa mtu pale alipo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa kazi hii, naishukuru sana Wizara ambayo kwa kweli iliwatumia watumishi wake, Makamishna wote, Katibu Mkuu akiwa ndiye kiongozi na hata Waziri mwenyewe wamefika kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ni ngumu sana kwa mtu ambaye hana dhamira na uamuzi kamili. Kwa kweli tunaishukuru sana Wizara hii kwa uamuzi wa Viongozi wake kukubali kwenda Vijijini kukaa na kuishi na wananchi na kuwaelekeza. Napenda niwashukuru sana na Mungu awasaidie wazidi kusaidia katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara itusaidie, bado hatuna *ledger* za kutosha. Sasa inaonekana kuna watu wengine wataanza kughushi kununua *ledger* zisizo kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba *ledger* hizi pamoja na hati hizi ziwe kamilifu na ziwe zile zilizo aina moja kwa nchi nzima zisije zikachanganywa na watu wakaanza kughushi na zikatuletea matatizo. Hili ninaomba sana itusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Miji yetu hii tunayokaa haina hadhi, haina sifa ya kuwa Miji, tunazidi kutafuta upana wa Mji. Sasa katika upana wa Mji hatutaki sifa za hali ya majengo na Miji yenyewe.Sasa hili ni hatari katika maisha haya. Miji yetu hii tunayokaa haina barabara kama alivyosema aliyetangulia hapa, haina barabara, kila mtu anajijengea tu. Sasa hali ya maisha ya watu wanaoishi katika Miji hii ni ngumu sana.

Wizara hii imejitahidi sana, imejitahidi sana kusimamia suala hili lakini watu ni wagumu hawaelewi, maana ya hizi barabara na Wizara hii inasaidia sana kuwapa watu hali halisi ya maisha. Nchi yetu hii ya Tanzania imekumbwa sana na kipindupindu. Hii ni kwa sababu ya ujenzi wa Miji yetu haukuzingatia taratibu za kiafya na taratibu za maagizo ya Wizara ya Ardhi, kila mtu anajijengea nyumba haelewi hata choo aweke wapi wala kielekezwe wapi.

Sasa ukienda kama Mwanjelwa Mbeya, imekuwa ni kawaida kwamba ni afadhali magari yazunguke vichochoro yakutanishe huko barabarani. Huwezi ukabomoa Mbeya upya kule Mwanjelwa sasa kumekwishalemaa. Kile ni kilema cha ardhi katika nchi na ndiyo haya yanayoendelea katika sehemu nyingi. Nenda hata hapa Makole, hivi pana utaratibu gani? Makole hapa hapa tunapokaa Dodoma, ingia pale huna hakika unakwenda wapi wala unaelekea wapi. Sasa hali ya maisha haya ni ngumu sana na ni mbaya sana katika kutegemea watu wabadilike na wafanye mambo ya maana.

Mimi ningeomba Miji tunayoipa au kuipandisha ngazi kuwa Mji, uwe *Township*. Sasa hizi *Township* tumeanza kuzipa hadhi mradi tu watu wamekaa shaghalabaghala ni *Township* hata Ofisi zenyewe za *Township* haziko. Sasa mnawapa kwa misingi ipi? Tunazidi kuleta matatizo na tatizo kubwa nililojifunza mimi ni Wizara ziko karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tatu zinaingilia sana utaratibu wa Wizara hii ya Ardhi. TAMISEMI inapandisha *grade* ya Miji hii, ngazi za Miji hii. Hivi huwa imekwenda imeona hadhi na jinsi inavyoonekana katika Mji ule au wanakaa Ofisini tu mradi Vikao vimekaa wanapitisha?

Sasa hii TAMISEMI kwa kweli isiwe inapitisha tu hadhi ya Mji bila kuona uhalali na haki ya hali ya pale ilivyo. Kwa utaratibu TAMISEMI inaoufanya sasa kwa kweli tukubali ni makosa na itatuharibia utaratibu wa nchi. Naomba sana wawasiliane vizuri na watu wa ardhi wawaelekeze utaratibu mzuri wa heshima ya Kijiji au Mji kuliko kuwezesha tu kwamba hiki sasa ni Kijiji, hapa ni Mji bila kuwa na takwimu halisi na taratibu na michoro inayokubalika.

Mahali wanapokusanyika watu lazima pawe na utaratibu wa hali ya afya, pawe na mifereji ya maji. Vijiji vingi vimekwishavurugika, ardhi imekwishalika kwa sababu hakuna hata utaratibu wa namna ya kuweka maji yatiririke na mifereji iwekwe vipi. Sasa hii hali inatuletea matatizo sana katika hali inavyokwenda.

Manispaa ina hadhi gani mpaka iitwe Manispaa? Inafanya nini na inatakiwa iweje? Kuwe na maelekezo yanayoeleweka na yanayokubalika na Wizara ya Ardhi. Tukisema TAMISEMI ipendekeze tu, hatutakuwa na Manispaa zenye hadhi, zitakuwa ni

Manispaa za nchi yetu ya Tanzania lakini si Manispaa za nchi nyingine zinavyoeleweka, haitawezekana kuwa na vitu kama hivi.

Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hizi zinazoshughulika, leo tuna Wizara hii ya Ardhi inawapa mamlaka Vijiji kumiliki ardhi zao na kusimamia lakini wanafika Wizara ya Nishati na Madini wanawapa watu hati za kuchimba madini, wanatoka moja kwa moja Wizarani wanaanza kung'oa mawe na kuchimba mashimo bila hata kupata taarifa yoyote kwa Vijiji wala Wilaya. Hivi kweli tutajenga nchi?

Sasa viko Vijiji na wako watu wamedhulumiwa maeneo yao eti wachimbaji wa madini wameona kuna madini na wanasema sisi tuna haki ya kuchimba madini. Hivi kweli utaratibu huu utaeleweka? Mimi naomba kwa kweli Wizara hizi zisifanye mambo haya bila kujua hali halisi ya mipango ya Wizara ya Ardhi kwa ajili ya watu wa maeneo yale.

Nchi nyingine mali ya madini, wamiliki wa ardhi, lakini kwenye eneo *surface area* wamiliki wale walio na haki ya wana hati ya mila lakini anakuja mtu anachimba madini pale, ang'oa miti yake, anavuruga ardhi na halipwi. Akidai, wanasema wakae wazungumze. Sasa hii kwa kweli tunavuruga hali halisi ya watu na unyonge wa mtu wa Kijijini utazidi kuwa mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu za Wilaya hazina wataalam. Mimi nadhani nina watu watatu pale Wilayani Mbozi. Sasa hawa watapima viwanja vingapi kwa mwaka? Hakuna! Mimi nadhani Wizara hii imesahaulika katika suala hili na pengine utaratibu huu tunaosema TAMISEMI ndiyo ikubali kuidhinisha ajira ya Wilaya, tutakosa wataalam katika Wizara nyingine.

Kwa namna hii, tutakwama mafanikio ya maendeleo. Naona ni afadhali kwa kweli kuwe na utaratibu maalum, usimamiwe na utaalam wa Wizara ya Ardhi ili waajiriwe wataalam wanaojua mipango ya Miji na upimaji wawekwe katika kila Wilaya na Wizara hii ifuatilie ione utekelezaji kuliko hali tuliyonayo. Vinginevyo hali yetu itakuwa mbaya sana na tunakokwenda kutakuwa kugumu sana.

Napenda kusema kwamba Wizara hii ndiyo pekee ya misaada ya maendeleo. Nchi nyingi za wenzetu huko Ulaya wanaamua kujenga maghorofa, hii ya kupanua sehemu tu inaondoa sehemu za kuzalisha mali kwa wananchi. Ndiyo maana hata sehemu nyingi hata viwanja vya michezo huwezi kupata. Utapata wapi watu wametanua maeneo yao tu! Haiwezekani! Lazima kuwe na utaratibu na misingi inayosaidia.

Napenda kuwashukuru Wizara hii kwamba mtindo walionao huu walioanzisha wausimamie na hata kama wao hawarudi, basi watakaofuatia wasimamie kwa kuwa Watendaji wapo wasimamie wajue huu ndiyo uhai wa watu wetu nchini hapa.

Tukishapoteza nguzo na haja ya watu wetu katika ardhi, hatuwezi kwenda mahali popote. Kila mtu apate haki yake na hii hati ya mila kwa kweli ipitishwe, ni wajibu na ni

lazima kwa kila Kijiji mtu asiye na hatimiliki katika Kijiji chake aelewe kwamba hatakiwi hata kuwepo pale. Yuko pale anafanya nini? Anaishi vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwape nafasi watu wawe na hati ya kumiliki maeneo yao na wazalishe katika maeneo yao, ndiyo njia pekee itakayotusaidia na kutuwezesha kubadili maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze tena Wizara hii ya Ardhi na hasa Katibu Mkuu ambaye ni mwanamama na hii ndiyo dalili kwamba kwa kweli kuwa mwanaume hakuna maana ya kuwa una uwezo zaidi ya akinamama. Lazima tukiri akina baba kwamba akina mama wapo wenye uwezo na wapo goigoi kuliko wote. Tujue ndiyo dunia inavyokwenda kama walivyo goigoi wanaume wengine.

Kwa hiyo, hii tukubali na tuseme ndugu zangu tupitishe makadirio ya Wizara hii ili watusaidie na sisi tutajikongoja kufuata ushauri wao ili kwenda kwa pamoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja na ninaomba wote tuiunge mkono. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona, kwa kitabu hiki na mafanikio yake.

Nashukuru kwa kazi nzuri ambayo Wizara imeifanya, lakini bado Wananchi wengi hawajapata miliki. Mheshimiwa Waziri, naomba uangalie urasimu uliopo ofisini, inachukua muda mrefu mpaka mhusika kupata miliki baada ya kukamilisha hatua zote.

Kuhusu kupanga mipango na kusimamia maendeleo ya Miji na Miji midogo midogo inayoanzishwa, lazima iandaliwe mipango madhubuti ya kupata makazi ya kisasa. Je, hapa Dodoma zile nyumba ndogo ndogo mpya za karibu karibu ndiyo mipango Miji inavyoeleza?

Je, kuna uhusiano gani wa Mradi wa *HABITAT* wa Mheshimiwa Anna Tibaijuka na Idara yetu ya Mipango Miji? Mheshimiwa Anna Tibaijuka anasaidia wanawake wapewe upendeleo kwenye makazi ili waweze kuwa na nyumba. Je, Wizara yetu inasaidia wanawake kupata viwanja kwa makazi?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri inayofanyika Wizarani. Kero za viwanja Wilayani hasa Kongwa zimepungua sana kutokana na mabadiliko makubwa ambayo

yamefanywa na Wizara na maelekezo Wilayani kwa kuongeza uwazi katika *process* nzima. Kutokana na hayo basi, nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wetu wanajenga nyumba bila ramani. Nashauri Wizara isambaze kitabu chenye ramani rahisi kiujenzi zinazofaa vijijini. Hili likifanyika, litawezesha Wananchi kujenga nyumba bora, zinazopendeza badala ya hali ya sasa ya majengo ya ovyo ovyo yanayotofautiana mno na wakati mwingine yenye gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, haipeleki *OC* kwa Idara ya Ardhi Wilayani. Maafisa wa Ardhi Wilayani hawana hata pikipiki na hawana vifaa vya kisasa vya kupima viwanja, wapeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la upimaji mashamba vijijini bado ni gumu, halitekelezwi kirahisi. Wizara ione namna ya watu wetu kuwa na *title deeds* za mashamba yao kwa kuchangia sehemu ya gharama za upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliahidi kuwa, kutakuwa na kanda za utoaji hati za kumiliki ardhi. Suala hilo limefikia wapi hadi sasa. Hii ni kero kubwa sana, ikiwezekana kila Mkoa/Wilaya watoe hati huko huko na siyo Dar es Salaam. *The role of the Comissioner of Lands has to be looked afresh in the Land Law. Decentralize some decisions.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la ardhi za vijiji kuvamiwa na watu toka mijini, wenye fedha, kwa kuhonga baadhi ya viongozi wa vijiji. Mbaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata hayapo na hali ni mbaya. Wizara iagize Mabaraza haya kuwepo haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo migogoro ya ardhi kati ya Mkoa wa Manyara na Dodoma kwa Wilaya ya Kiteto na Kongwa, pia eneo linalotenga Wilaya za Kilosa, Kongwa na Kiteto. Wizara isaidie kuchambua na kueleza mipaka halisi inapitia wapi. Jambo hili ni muhimu japokuwa limekuwa likipuuzwa. Wananchi wa maeneo husika wanasumbuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uelewa wa sheria za ardhi vijijini ni mdogo, tunashauri elimu hiyo ipelekwe huko ili haki za familia moja moja kwa ardhi zao ieleweke. Vijitabu rahisi vilivyoandikwa kwa Kiswahili visambazwe vijijini kote na masuala muhimu ya ardhi yawe kwenye mitaala ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe makini sana na *EA Federation,* kuhusu suala la ardhi. Wakenya, Waganda na wengine, wasiruhusiwe kumiliki ardhi ya Tanzania; vinginevyo waingie ubia na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika maeneo machache yanayofuatayo: Kwanza, ujenzi holela katika vijiji, miji midogo na miji mikubwa. Historia ya vijiji vya ujamaa wakati unaanza ujenzi wake ulikuwa wa mpango maalumu. Nyumba zilijengwa kwa mistari na nyumba hadi nyumba nyingine kulikuwa na nafasi ya kutosha kabisa. Hali ilivyo hivi leo ni kinyume kabisa, nyumba zinajengwa kiholela hivyo, kuharibu mandhari nzuri iliyokuwepo huko nyuma. Naomba Serikali ivisaidie vijiji viwe na mipango mizuri ya ujenzi ili viwe ni vyanzo vizuri vya miji ya baadaye. Ikiwa vijiji vitakuwa na mipangilio mizuri ya ujenzi, basi na miji nayo itakuwa na mipangilio mizuri pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji Midogo ya Mangaka na Michiga iliyopo ndani ya Jimbo la Nanyumbu, inakua kwa haraka sana. Idadi ya wakazi inaongezeka siku hadi siku. Hivyo, Miji hiyo inahitaji kupimwa ili kupunguza tatizo la ujenzi holela. Ni vizuri Miji mipya ikaendelezwa kuanzia mwanzo ili kupunguza matatizo ya ujenzi holela yanayoikabili Miji ya zamani. Haipendezi kuacha Miji ikikua bila ya mipango mizuri ya ujenzi na baadaye kulazimika kuwa na bomoabomoa ili kuweka miji hiyo katika hali nzuri. Ni wajibu wa Serikali kubaini maeneo yote yanayoelekea kuwa Miji baadaye na kuyaandaa kwa ajili hiyo. Miji midogo ya Mangaka na Michiga ni miongoni mwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii moja kwa moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri wake na Watendaji Wakuu wa Wizara, kwa mabadiliko makubwa yanayoonekana sasa ya usimamizi wa ardhi na msukumo wa maendeleo ya makazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuipongeza Serikali ya Tanzania kwa kusimama imara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* kwa kuifanya ardhi kuwa mali ya nchi husika badala ya kuwa mali ya Shirikisho wakati Shirikisho la Afrika Mashariki likifikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu unatoa nafuu kwa Tanzania kuandaa na kutekeleza mpango mzuri wa kuwezesha Watanzania wengi kumiliki ardhi kama viwanja au mashamba kabla ya Shirikisho la Afrika Mashariki kufikiwa. Hivyo basi, nashauri mambo yafuatayo ambayo yameanza kutekelezwa yaendelezwe kwa kasi na Serikali kubeba sehemu kuu ya gharama zake kama ifuatavyo:-

- Kupima viwanja vingi zaidi katika Miji yote ya Tanzania ili wafanyakazi na wafanyabiashara wapewe wajenge na kumiliki viwanja kama sehemu halali ya nchi yao;

- Kutoa leseni miliki za ardhi kwa wakulima vijijini ili wawe na haki na hati za kumiliki maeneo yao ya ardhi ya jadi, Serikali igharamie upimaji;

- Yatengwe na kupimwa maeneo maalumu mapya ya uendelezaji wa viwanda na kuwe na miundombinu muhimu kuvutia wawekezaji wazalendo na wageni;

- Yatengwe na kupimwa maeneo mapya na maalumu ya uwekezaji wa kilimo kwa wakulima wakubwa wakiwemo wazalendo na wageni;

- Wizara iimarishe usimamizi wa taratibu na kanuni za upimaji wa mashamba ili kurahisisha kazi hiyo. Kumekuwepo na vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wa upimaji wa mshamba kama ifuatavyo: Wapimaji kuwa wachache na kutozingatia ratiba; wapimaji kutofuatilia na kutekeleza maombi ya Wananchi binafsi hasa katika maeneo yaliyopo mbali na ofisi zao; wapimaji kukosa usafiri wa kwenda katika maeneo ya upimaji mbali na ofisi zao; na wapimaji kutopendelea kwenda katika maeneo ya upimaji bila kupewa posho na uhakika wa chakula wakati wa saa za kazi wakiwa mbali na ofisi zao; na

- Uhusiano kati ya Wizara ya Ardhi na TAMISEMI/Halmashauri ni dhaifu sana. Halmashauri nyingi zina Maofisa wa Ardhi dhaifu sana na wengine wasio na sifa kamilifu. Tatizo kubwa ni kwamba, Maofisa hao mwajiri wao ni Halmashauri wala sio TAMISEMI, wala Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi! Hivyo uwezo wote uko mikononi mwa Halmashauri ambayo haina utaalamu wa ardhi. Hata hivyo, Afisa wa Ardhi katika Halmashari ndiye msimamizi mkuu wa Sheria ya Ardhi Wilayani kwa niaba ya Serikali na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Udhaifu wake na vitendo vyake kinyume na kanuni za ardhi ni fedheha kwa Wizara na Serikali inayomlipa mshahara au ruzuku kwa Halmashauri.

Kwa udhaifu wa aina hiyo, itakuwa vigumu kwa baadhi ya Halmashauri kwenda sambamba na mipango mikubwa inayokusudiwa kutekelezwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Katika masuala ya gharama za upimaji wa ardhi, Serikali inapaswa kuhakikisha fedha za gharama husika zinafika kwa wakati ndani ya Halmashauri na kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Wizara, kwa kuanzisha mpango wa kutoa leseni za umiliki wa nyumba bora katika maeneo ambayo bado hayajapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuiandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwelekeo mzuri wa utendaji wa Wizara hii chini ya Mheshimiwa Gideon Cheyo na Wasaidizi wake, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati, kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, mipaka ya Tanzania na nchi jirani bado haieleweki, kwa sababu utaalamu uliotumika wakati wa wakoloni wakigawana maeneo hayo, haukuwa unazingatia tabia ya mito kuhama, hususan mito ya Songwe, Ruvuma na Kagera. Mpaka wetu na *Mozambique,* yaani Mto Ruvuma, una tatizo la kutokuwa na alama *(beacons)* za kudumu. Mto unapobadilisha mkondo sehemu ya eneo huhama kutoka eneo la nchi nyingine. Hali hii inaweza kuwa chanzo cha uhasama na hatimaye kuzua vita kati ya nchi na nchi hasa pindi madini kama mafuta, gesi au dhahabu, yakigundulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara kwa kushirikiana na nchi jirani, wakae ili kupima upya mipaka hiyo kwa kutumia vifaa vya kisasa hususan *Global Positioning Systems (GPS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya ujenzi holela wa makazi Mijini na Vijijini unazidi kasi ya upimaji ardhi unaofanywa na wataalamu na matokeo yake, Miji yote itakuwa kama Jiji la Dar es Salaam, kwa ujenzi usiofuata sheria. Nashauri Serikali ilegeze masharti ya upimaji ili kuwaelimisha wanavijiji kupanga makazi yao kwa mpangilio kwa kutumia wanavijiji au hata wakazi wanaoishi pembezoni mwa Miji, wanachohitaji ni kuelekezwa na kutambua juhudi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi ngazi ya Kata na Vijiji yameundwa, lakini ufanisi wake unategemea kutolewa kwa elimu ya ardhi na maendeleo ya makazi kwa Wajumbe wanaounda mabaraza hayo. Aidha, upo utata kuhusu nani atawalipa Makatibu wa Mabaraza hayo.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maenedeleo ya Makazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa , Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo, ambao ni msingi muhimu kwa maisha na maendeleo ya watu wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ni nzuri, yenye kina na mwelekeo wa maendeleo ya watu wote wa nchi yetu hii ya Tanzania na Tanzania yenyewe kwa ujumla. Ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uzuri wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, sina budi kuiomba sana Wizara yetu hii, pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa inabidi kuwa makini na uangalifu mkubwa sana kuhusiana na suala zima la ardhi ya nchi hii ya Tanzania ibakie kuwa mikononi mwa Serikali yetu na Wananchi wa Tanzania wenyewe na wala siyo kwa wageni kutoka nje.

Tujiepushe sana na suala la ardhi ya nchi yetu isije ikawa kama ilivyo kwa wenzetu wa Zimbabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu ya ardhi ni lazima ilenge katika maslahi ya Wananchi wa Tanzania zaidi na isitoe mwanya hata kidogo kwa wageni kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninaliomba kwa Wizara yetu hii, pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni suala linalohusiana na mipaka ya nchi yetu na ya nchi jirani ambazo tunapakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara na Serikali kuweka alama zinazotambulika katika mipaka ya nchi yetu na nchi jirani tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalizungumzia hili kutokana na kubahatika kutembelea karibu mipaka yote ya nchi yetu, isipokuwa mpaka wetu wa Mkoa wa Ruvuma tukiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpaka wetu na Uganda tu ndio niliouona kuwa una alama zinazoeleweka vizuri kwa kuwekewa *beacon* zilizo wazi. Mpaka wetu na Msumbiji kuna miti mikubwa kwa upande wa Msumbiji ambayo kwa kweli haioneshi uimara wa alama sahihi za mpaka wetu wa Msumbiji. Vilevile hata mpaka wetu na Burundi alama ipo katikati ya Daraja la Rusumo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la mipaka yetu, ninaiomba Wizara na Serikali yetu kushughulikia suala zima la mpaka wa nchi yetu na Malawi. Mpaka huu upo katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi hutolewa taarifa kuwa mpaka huu hauna matatizo, lakini ukiangalia kwa undani kabisa, utaona kuwa mpaka huu una matatizo makubwa na ya hatari kwa nchi yetu hapo baadaye. Mpaka huo wa nchi yetu na Malawi ni Ziwa Nyasa ambalo liko katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia kuwa miradi yote inayohusiana na uboreshaji wa mazingira katika mabonde na maziwa mfano kama Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, yanaboreshwa kwa kugharamiwa na wafadhili kama vile Benki ya Dunia na kadhalika. Lakini Ziwa hili la Nyasa linashindwa kufadhiliwa kwa sababu ya huo mpaka wetu na Malawi kuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia kuwa wenzetu wa Malawi wao wansema mpaka wetu huo upo ufukweni upande wa ardhi ya Tanzania na wanasema kuwa maji na rasilimali yote iliyomo katika Ziwa ni ya kwao, wakati sisi Tanzania tunasikia kuwa ramani yetu inaonesha kuwa mpaka wetu unapita katikati ya Ziwa Nyasa. Vilevile tunasikia kuwa ramani ya Malawi na ile ya Dunia zinaonesha kuwa mpaka huo unapita katika ufukwe wetu wa Tanzania. Vilevile tunasikia kuwa kabla ya uhuru wa Tanzania, Malawi na Msumbiji, ziwa hili tulikuwa tukiliita Ziwa Nyasa lakini Malawi walipopata uhuru ziwa hili waliita Ziwa Malawi. Pia tunasikia kuwa miradi yote ukisema Ziwa Nyasa, wafadhili wanasema kuwa, hakuna Ziwa Nyasa wao wanajua kuwa kuna Ziwa

Malawi. Tukiangalia kama hali iko hivyo kama tunavyosikia, ndio inanipa hofu kubwa kuwa mpaka wetu huo utaleta matatizo makubwa na ya hatari kwa Taifa letu hapo baadaye kama suala hili halikushughulikiwa mapema ipasavyo ili kuweka sawa mpaka wetu huo kuwa sahihi na tukakubaliana kati ya nchi yetu, Malawi na Taasisi mbalimbali za Kimataifa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupata maelezo sahihi juu ya mpaka huo kutokana na hoja niliyoieleza hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama maelezo hayo ni sahihi na yapo kweli, ninaiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ishughulikie suala la mipaka ya nchi yetu hasa huo mpaka wetu na Malawi na kadhalika ili kuondoa utata na wasiwasi huo unaojionesha miongoni mwetu sisi Watanzania juu ya suala hili la mipaka ya nchi yetu. Ninaomba suala hili lishughulikiwe, kutokana na hali ya sasa katika nchi yetu kugundulika rasilimali nyingi kama madini, gesi asilia na pia tuna matumaini ya kugunduliwa mafuta na kadhalika hapo baadaye. Kwa hiyo, mpaka huo kama hautotambulika kisheria katika maeneo yote ya nchi zetu na katika Jumuiya za Kimataifa, tunaweza kuja kuitumbukiza nchi yetu katika migogoro na nchi nyingine jirani kama inavyotokea kwa nchi za Nigeria na Cameroon, kama eneo hili itagunduliwa nishati yoyote na nishati hiyo ikaleta utata wa kuwa ipo katikati ya nchi ya Tanzania na Malawi kutokana na tatizo hili la mpaka na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa, suala hili litashughulikiwa, ninarudia tena kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naandika leo hii kukumbushia ombi langu nililolitoa wakati wa bajeti ya 2004/2005. Siku ile nilimwomba Mheshimiwa Waziri, awaruhusu *surveyors* wake waweze kuja Jimboni Namtumbo, kwa lengo la kulipima eneo la majenzi mapya katika eneo la Mji Mpya wa Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili jipya ni la mashamba ya wakazi wa Kijiji cha Namtumbo, ambao wamelitoa bila malipo ili majenzi ya makazi na maofisi yaanze kujengwa. Hadi sasa matofali ya kujenga Boma la *DC* yapo tayari, pia yapo matofali ya kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya yapo. *DC* anajengewa ofisi na nyumba yake ya makazi ipo tayari na *DC* anaishi humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Namtumbo inashindwa kuanza kujenga makazi ya Wananchi, kwa sababu kibali cha Wizara yako Dar es Salaam hakijatoka. Je, ni lini utatoa kibali chicho?

Mheshimiwa Waziri mwaka 2004, ulinieleza kuwa, Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona, ungelimwagiza hili ombi langu litekelezwe hasa ukikumbuka mwaka

huu ni wa uchaguzi, niwaeleze nini kuhusu suala hili kutekelezeka ? Suala hili ni kero kwa wakazi wa Namtumbo, ambao wanataka kuanza kujijengea makazi mapya.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Pili, nawapongeza mno kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara hii na sasa kuondoa kero ya viwanja Dar es Salaam.

Ningependa kufahamu Wizara ina mipango gani ya Miji midogo mfano Ndala, Puge na Nata katika Jimbo la Nzega kutumia fursa ya Miji hiyo inayokua kwa kasi ipimwe ili ramani zipatikane?

Ningependa kufahamu Wizara itanisaidiaje, ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kifedha, kiutaalamu na vifaa katika zoezi la kupima viwanja Ndala, Puge, Nata na Nzega Mjini, kuna upungufu wa wataalamu katika Wilaya Nzega, mfano, Mpimaji, Afisa Mipango Miji na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kheri, baraka za Mwenyezi Mungu katika kazi zao za kila siku. Mbarikiwe.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri aliyoionesha hasa kuwa yeye amesimamia vizuri kuhakikisha Watanzania wanakuwa na hatimiliki ili ziwawezeshe kupatiwa mikopo ili kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesaidiwa vizuri sana na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Hajjat* Tatu Ntimizi, ni mama mchapa kazi, msimamizi na mfuatiliaji kwa yote yaliyoamuliwa na Waziri na maswali kujibiwa vizuri Bungeni. Ahsante sana.

Nawaomba Wananchi wa Wilaya ya Ileje kwenye Jimbo la Mheshimiwa Gideon Cheyo, Wana-CCM wampe kura nyingi ili tuendelee naye, tumemzoea vizuri sana na Mungu ambariki ashinde kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Wananchi wa Jimbo la Igalula, wampe kura nyingi Mheshimiwa Tatu Ntimizi, ni mwanamke anayekubalika, asiyetetereka kiutendaji, Rais hakukosea kumteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii, namwombea kwa Mungu amsaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitamsahau Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona, ameleta maendeleo na mabadiliko mengi tangu amefika kwenye Wizara hii. Watu sasa hawasumbuliwi tena kama zamani upatikanaji wa hatimiliki, ila namwomba mimi nazungushwa hati ya Alex Nyawazwa, Sinza *Plot.S594/B,* amepewa *Offer* tangu 1982 hadi leo hati haijapatikana, hili ni ombi maalum naomba Ofisi ya Ardhi Kinondoni watoe hati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bibi Salome Sijaona, naomba aendelee kuchapa kazi na sisi wanawake tuko pamoja naye, Mungu atamsaidia kwa kazi yake nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anifafannulie kwa nini *CDA* Dodoma inashindwa kutoa hati za wakazi wa maeneo ya Maili Mbili, *Oysterbay* na Chang'ombe haraka? Naomba nielezwe nani mhusika wa utoaji wa hati hizi; ni Wizara au *CDA?* Naomba mamlaka ya hati iwe chini ya Wizara na *CDA* wawapimie Wananchi viwanja ili wapate makazi mazuri, wanaondokane na MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa ratiba nzuri inayoendelea ya upimaji wa viwanja kwa wingi Dar es Salaam, naomba na Mikoani muendelee vivyo hivyo .

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja na Bunge liidhinishe fedha zote. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze watumishi wa Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mhesimiwa Tatu Ntimizi, Naibu Waziri na Mama Salome Sijaona, Katibu Mkuu, kwa jinsi walivyosimamia utendaji wa kazi na kupunguza kwa kiwango kikubwa, rushwa ndani ya Wizara. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Sumbawanga umekuwa Manispaa tangu tarehe 1 Julai, 2005. Kwa kuzingatia hilo, je, Wizara inasaidiaje Manispaa yetu katika kuiandaa *Master Plan* mpya ili mkao wa wakazi na wa ujenzi wa nyumba ulingane na heshima ya Mji wenyewe. Katika kutekeleza Sheria za Miji, je, maeneo kwa ajili ya *Green Belt* hutengwa kwa kutumia vigezo vipi, mbona Miji mingi haina *Green Belts?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu, mimi pamoja na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, tulifanya mkutano Afrika ya Kusini, Mjini Durban na moja ya mapendekezo ni kuwa na Miji isiyokuwa na *squatters.* Hivi mipango ipi inaandaliwa ili hata *squatters* wapangwe na wapewe hati za muda za maeneo yao? Hii itasaidia kuwapatia mikopo nafuu kwa kutumia vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzuia Miji yetu isiwe inapanuka sana kieneo kwa kujenga nyumba za kawaida badala ya kujenga maghorofa; je, kwa nini Shirika la Nyumba na Serikali isiweke sera kuanzia sasa ya kujenga maghorofa na hasa katikati ya Miji? Serikali imeendelea kufanya kosa hilo hilo kwa nyumba zake zinazojengwa sasa kuwa za *bungalow* badala ya maghorofa. Ikiwa Taasisi hizi zitaendelea na mtindo huo, je, watu binafsi watafikia wapi katika kujenga majengo ya juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya *Miji Proper* ni kigezo kipi kinatumika ili mwananchi aweze kumiliki eneo zaidi ya eka tatu za kulima au kuweka eneo la ufugaji. Je, ni kweli maeneo yaliyomo katika Miji, Manispaa na Jiji, hayawezi

kupewa hati za kumiliki mashamba zaidi ya eka tatu? Mwongozo kwa nchi nzima utolewe ili tusimwachie kila mmoja atekeleze aonavyo. Upimaji wa viwanja na gharama zake huzingatia nini, mbona katika Miji mingine gharama zake ni ndogo kuliko katika Miji mingine? Kwa nini wakati ufadhili wa kupima viwanja unatolewa na Mashirika ya Kimataifa lakini bado tunalipia gharama? Je, Mashirika ya Kimataifa hugharamia nini na mwananchi naye anagharamia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, *DAP* na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri za usimamizi wa kazi na majukumu yao. Hongera sana, nitawapatia medali ya neno ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumeshuhudia uwekaji wa mawe pembezoni mwa barabara. Haya mawe ni hatimiliki za barabara; nani anaweka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi au Wizara ya Ujenzi na ni nani mwenye mamlaka ya kuweka miliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu kama kuna tofauti ya gharama ya upimaji, umiliki na ada za vitu vifuatavyo vyenye eneo la ukubwa unaofanana, lakini matumizi tofauti mfano, kiwanja cha michezo, shamba, eneo la burudani au ufugaji na je ni kiasi gani kwa matumizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi za Vijiji mbona wanavijiji wenyewe bado hawajapata hata semina au angalau nakala ya sheria hiyo; Wizara ina mpango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi itahamia Dodoma? Bado mnang'ang'ania Dar es Salaam ndiyo maana nadhani Wizara yenu kazi zake ni kupima Gezaulole, Mwanabilam, Pinole, Mvuti na Kawe. Naomba kujua mpango wenu wa kuhamia Dodoma ukoje au hamtaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja vya kujenga Dar es Salaam na Dodoma, je, hivi kwa kuonesha mfano kama Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wa Idara na *DAP,* mna viwanja vingapi Dar es Salaam kila mmoja, kuna ushindani wowote Wizarani wa kuwahi viwanja au hamjachangamkia hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ramani ya nyumba za viongozi na nafasi, hapa ninazungumzia mtindo unaofanywa na huyu Mheshimiwa John Magufuli , kuleta mtindo wa kujenga nyumba za viongozi kama Kambi za Mkonge au *Barracks* za JWTZ, *Platoon, Sections;* kama Wizara naomba mtoe maelekezo, ujenzi wa aina ile siyo mzuri kwa hadhi ya viongozi. Hivi Wizara halioni hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inahusikaje kuhusu mipaka? Mfano wa kwanza, Lung'ala ilikuwa kijiji cha Rudewa baada ya Lung'ala kuwa kijiji. Mfano wa pili, Kisemo ilikuwa kitongoji cha kijiji cha Kidugallo baada ya Kisemo kuwa kijiji.

Mfano wa tatu, Kitongoji cha Bamba kilikuwa kitongoji cha Kiroka baada ya kuwa kijiji? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijibu kwa makini sana aina ya kodi zilizofutwa sekta ya ardhi, Halmashauri zinaendelea kuzikusanya. Tuambiwe leo aina ya kodi zilizofutwa ili Wananchi wasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tabia mbovu inaendelea miji kukua na kuhodhi vijiji kutangaza kuwa maeneo ya mji bila kushirikisha Halmashauri ya Wilaya husika. Baadhi ya vijiji humezwa kiholela, mfano, Dar es Salaam sasa iko kwenye Kibaha na Kibaha nayo inakuwa hadi Ruvu, Iringa inakuwa Morogoro, Tanga. Baada ya miaka 100 ijayo, Tanzania itakuwa mji mmoja tutalima wapi?

Naishauri Wizara ilete mwongozo wa kulinda vijiji vilivyomo kando kando ya Miji ili iviimarishe vijiji vilivyokuwepo kuwa vijiji na mji tofauti ulivyo, maana uji siyo ugali ulioyeyuka na ugali siyo uji ulioganda, ni maandalizi.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa na ngumu ambayo inafanyika siku hadi siku. Ningependa pia nitaje kwa majina viongozi wa Wizara ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Naibu Waziri, , Katibu Mkuu, Mama Salome Sijaona, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Sasa naomba nikumbushe machache ya utekelezaji na kama yametekelezwa basi nipatiwe majibu.

(a) Je, ni mashamba mangapi makubwa kwa ajili ya wawekezaji yaliyopimwa na kupata hatamiliki kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na kama matangazo kwa wawekezaji wakiwemo Watanzania? Je, ni katika Mikoa ipi na ni mashamba mangapi kati ya hayo yamekwisha milikiwa?

(b) Je, mtindo wa kupima mashamba makubwa kwa kilimo ni sawa na huu wa viwanja 20,000 vya Dar es Salaam, kwa maana ya mkopo maalum?

(c) Je, tumwone nani kama tutahitaji mashamba hayo mliyokwisha yapima?

(d) Shamba la Mwakinyumbi Hale Tanga lilitolewa kwa Wananchi wa eneo hilo muda mrefu zaidi ya miaka mitatu. Je, Wizara imechukua hatua gani ya kuwapimia Wananchi hao ili waweze kuzalisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa Wizarani kuanzia nidhamu hadi mapato. Je, ni kiasi gani cha makusanyo kwa kipindi cha miaka mitatu ya nyuma kwa mfano, mwaka 2002 hadi 2003, ongezeko hadi leo kwa asilimia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zinazojengwa zinauzwa ghali sana na tukiuliza tunaambiwa kwamba, gharama nyingine zimeingia kwenye miundombinu. Je, kwa nini miundombinu hiyo isifanywe na Wizara husika na kama hizo Wizara hazina fedha kwa sasa pindi wakipata fedha za miundombinu hiyo je, watarejesha kwa wateja hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kujua *time frame* na kiasi cha fedha kinachotumika kwa kurekebisha makazi ya Manzese na *study,* pamoja na michoro mipya kama ipo. Je, ni kiasi gani Wizara hii hushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula ili kuharakisha maendeleo Kitaifa? Ningeshauri kuwepo na ukaribu na Wizara hiyo ndipo tutakapoondoa umaskini nchini hasa kupima mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya bajeti na ninapendekeza kasma hii iongezwe zaidi kwani kuna nidhamu kubwa ya matumizi ya fedha za Serikali. Ahsante.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa ujumla sina ugomvi na mipango ya maendeleo ya Wizara hii, kazi yao ni nzuri na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkereketwa mkubwa wa kukuza uchumi wa nchi yangu. Tumefanya mengi ya kuvutia wawekezaji kuja ili kuinua uchumi wa nchi yetu, lakini bado kuna walakini katika kuwavutia wakulima wakubwa ili kuja kuanzisha mashamba mapya. Wengi au tuseme wote, wanaokuja ni kwa kufufua yale mashamba ya zamani, lakini hakuna walio radhi kuja kuanza mashamba mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwa kuwa hatutoi *free hold* tunag'ang'ania *lease hold.* Maendeleo waliyoyapata kwa haraka huko *Mozambique* na Kenya ni kwa kuwa wanatoa *free hold*. Nchi yetu ni kubwa sana, kwa nini hatugawi sehemu fulani ya nchi ambayo wawekezaji watapewa *free hold* na sehemu maalumu tufanye ni za *lease hold.* Mimi naamini kabisa mpango huu utafufua kilimo na utajiri utakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili linalonikera, ni juu ya uuzaji wa nyumba za Serikali. Hizi nyumba ni mali ya Watanzania wote, kama jana tulivyopinga kuhusu *Mafuta House* kupewa *NSSF,* kwani ni mali ya Watanzania wote. Kupitia magazeti, wengi waliouziwa hizo nyumba wameshindwa kuzilipia. Naomba kwa zile nyumba ambazo wameshindwa kuzilipia, zirudi Serikalini na zibakie kuwa ni za Serikali. Msemo kuwa kuzikarabati ni ghali, hili halina msingi, kwani sasa wanatumia mabilioni kujenga nyumba mpya kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali. Sasa hivi sera ya Serikali siyo kufanya biashara, sasa vipi Serikali inajenga nyumba na kuuza, hii siyo Sera ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nyumba za Serikali wasiuziwe wafanyakazi wa Serikali, ziwe ni makazi ya wafanyakazi wa Serikali na wakatwe pesa za pango ambazo zinatosha kabisa kuzi-*maintain* hizo nyumba. Leo hii tuna amani, huko mbele hatujui kuna nini, utata lazima utakuwepo. Sisi katika Chama chetu cha CHADEMA tunasema hata kama itachukua miaka 100 kuingia kwenye madaraka ya

kuendesha nchi, lazima hizi nyumba zirudishwe Serikalini na vyama vingine vya Upinzani vinasema hivyo hivyo. Kwa hiyo, siku yoyote ile ikitokea mabadiliko ya Serikali, hizi nyumba zitarudishwa. Hata Wana-CCM wengi hawaungi mkono kitendo cha uuzaji wa hizo nyumba.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua dira ya Wizara hii kuhusu ujenzi wa nyumba au makazi ili upanuzi wa miji usiambatane na kukua kwa umaskini, kuongezeka kwa gharama katika utoaji wa huduma muhimu (simu, maji, umeme na barabara) kutokana na miji kupanuka kwa kasi kubwa kutokana na ujenzi wa nyumba fupi badala ya nyumba za maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanuka kwa ujenzi wa miji na vijiji kunakula ardhi nzuri ya kilimo na kuongeza umaskini, vipi sera ya makazi isizuie ujenzi wa majumba katika maeneo yenye ardhi nzuri kwa kilimo au *urban farming?*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitano au kumi ijayo katika Wilaya ya Njombe vijiji vifuatavyo vitakuwa miji: Ilembula, Uwemba, Kifanya, Mtwango, Makega, Lupembe na kadhalika. Vipi vijiji visipangwe katika ngazi kadhaa kwa kuzingatia sifa au ukubwa wa kijiji ili uamuzi wa kijiji kuwa mji mdogo uamuliwe na Wizara badala ya kusubiri Wilaya ziombe. Wizara iunde Kamati kukagua vijiji na kutoa mapendekezo Wizarani ili kuzuia nchi isijae miji ya *squatters.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika kwa Wizara kuamua miji kujenga nyumba za maghorofa au kuzuia Tanzania isiwe nchi ya majengo kila mahali. *Either we do or we (will) perish, tomorrow is now.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika wa kuunda Tume za *Rural Development Commission* na *Urban Development Commission* na kwamba, zishirikiane kusimamia maendeleo ya makazi kwa ujumla.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Siha, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hutoba nzuri, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri.

Aidha, naomba niipongeze Wizara, kwa kupambana na urasimu usiokuwa na maana, ambao ulikuwa unachelewesha upatikanaji wa hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, suala la umilikaji wa ardhi ni suala ambalo linawahusu Watanzania wote. Hili ni suala ambalo ni lazima tuwe *very conservative and quite traditional* hasa katika kuwamilikisha ardhi Wananchi Wazalendo. Vinginevyo,

tusipokuwa waangalifu tutakuta tumemilikisha wageni toka nje. Hali hii itazua vurugu zisizo na maana na hali hiyo itahamisha amani na utulivu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi itolewe kwa Wananchi Wazalendo na watu kutoka nje watafute Wananchi Wazalendo waendeshe ubia au wakodishiwe hayo maeneo na siyo kumilikishwa ardhi. Ardhi ni mali ya umma chini ya dhamana ya Rais wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwa maandishi hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Namshukuru zaidi Mheshimiwa Spika, kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Kamati ambayo kupitia kwayo, nimejifunza mengi kwa kufanya kati kupitia vikao, ziara na machapisho mbalimbali ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Nawashukuru wote waliochangia kunipatia mafunzo na busara, pamoja na maarifa yanayohusu ardhi na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusikiliza hotuba ya Waziri na kupitia kwa kina hotuba nzima, pamoja na viambatisho vyote, nimeridhika na upeo na kina cha hotuba hiyo. Kwa sababu hiyo, nawapongeza sana, kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri na Maafisa wote wa Wizara, pamoja na wa Taasisi, waliochangia katika maandalizi bora sana ya hotuba hii ya bajeti. Naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani zangu na pongezi zangu za dhati, yapo maeneo ambayo naomba ufafanuzi kama ifuatavyo: Katika moja ya michango yangu humu Bungeni 2004/2005, nilipofanya rejea ya Sera ya Maafa ya Taifa kutambua wakimbizi kama mojawapo ya majanga na hivyo kutoa wito kwa Serikali itoe upendeleo katika upimaji wa mipaka ya vijiji vya Mkoa wa Kigoma ili kuvibainisha waziwazi kutokana na makambi yapatayo 12 yaliyotapakaa Mkoa mzima.

Nilifarijika na Wananchi Mkoani Kigoma hususan toka Jimboni kwangu, walifarijika na kupongeza majibu ya Serikali kufuatia maombi yangu kwamba, Wizara ilipanga kupima vijiji 750 nchi nzima na kwamba katika kufanya hivyo, Mkoa wa Kigoma ungepewa upendeleo.

Naomba kauli ya Wizara, itachangia kiasi gani cha bajeti yake ya mwaka huu 2005/2006, kama gharama za kupima vijiji 75 ambavyo Mkoa wa Kigoma umepanga kupima, ambavyo 17 kati ya hivyo viko katika Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana na kuishukuru Wizara, kwa kuanza utekelezaji kwa vitendo, kwa kupiga picha za anga za miji midogo ya Uvinza na Nguruka, ambayo inainukia kama vituo vya biashara.

Ombi langu katika hili ni kwa Wizara kuipatia Halmashauri ramani na maelekezo ya hatua zinazobidi kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria katika mabadiliko yatakayobidi toka hadhi ya awali ya kijiji kuwa miji midogo. Hatua hii iandamane na utekelezaji kwa vitendo kwa kutoa mafunzo juu ya uandaaji wa mipango miji *(Interim Land Use Plans),* kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 34 wa hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia Wizara kwa kutoa ahadi na kuzitekeleza kama ilivyodhihirishwa katika ukurasa wa 34 ambapo mwaka 2004/2005, Wizara iliahidi kukamilisha mipango ya uendelezaji upya maeneo ya kati ya miji ya Kigoma na Sumbawanga na sasa hilo limekamilika. Utekelezaji huu bora utaufanya Mji wa Kigoma ambao ni lango la kuingia toka Nchi za Maziwa Makuu utaweza kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na Serikali kwa kuwa na mtazamo mzuri na wenye sura ya kuleta uwiano wa maendeleo ya miji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kutokana na kazi nzuri ni matarajio yangu, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wana kila sababu ya kusimama mbele ya Wananchi, kuomba ridhaa waendelee kuijenga Tanzania kwa kuwawezesha Watanzania kufahamu na kutumia ardhi kama silaha ya uhakika katika vita ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na wote tuombeane kheri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao waliomba kuchangia, wote wameisha. Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka jioni wakati ambapo watoa hoja, wataanza kujibu.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.04 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ningeomba kabla sijaanza kuchangia na mimi niungane na Wabunge wenzangu, waliotoa rambirambi na pole nyingi kwa wenzetu waliotutoka katika kipindi cha miaka mitano hii. Walikuwa watano, wa mwisho akiwa ndugu yetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, kwa kweli akina mama tulijisikia vibaya sana, lakini Mwenyezi Mungu, ndiye mwenye hukumu hiyo na tunawaombea marehemu wote roho zao aziweke mahali pema peponi na *inshallah* kesho umri-kiama wakafufuke katika viwanja vya pepo. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi naomba niungane na Wabunge waliochangia hoja hii katika kuunga mkono na pia kuweza kuchambua machache ili kuwajibu Waheshimiwa Wabunge, hoja walizozitoa mbele yako katika kikao cha leo. Kwanza kabisa, naomba nizungumzie wakati walipokuwa wanachangia hoja ya bajeti, walizungumza wachache kuhusu rushwa kukithiri kwa Watendaji walioko Wilayani. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunaendelea kuwasiliana sana na Watendaji kwa ukaribu, kujaribu kukemea na kusaidiana na TAMISEMI ili waweze kutenda haki. Ni kweli malumbano yamekuwa mengi lakini kazi wamefanya na Waheshimiwa Wabunge mnafahamu katika majimbo yenu, binadamu hakosi kasoro, lakini bado na sisi tumezingatia kwa sababu sisi ndio wazalishaji wa hao wataalamu na wenzetu ndio ambao wako chini yao kiutendaji. Tunawahakikishia kwamba, tutaendelea kuwasiliana ili kuweza kukemea na kuzuia kabisa jambo hili ili Wananchi wasiwe na matatizo.

Katika hoja hiyo pia amezungumza kuhusu mashamba kutofautiana kati ya ulipaji wa kodi yaliyoko Dar es Salaam, Pwani na Mikoani. Kwamba, Dar es Salaam na Pwani wanalipa shilingi 3,000/= kodi ya ardhi lakini Mikoani shilingi 2,000/=. Haya yote yalijitokeza na tumejibu katika majibu ya hoja kwamba, sehemu hizi ni sehemu ambazo zimekuwa na wengi wa kuhitaji mashamba hayo na pia kiuchumi yana afadhali kuliko mikoa mingine, lakini naomba mwendelee kutushauri na tuone jinsi gani tunaweza tukarekebisha kama iko budi. Pia alizungumza katika Ofisi ya Waziri Mkuu, alipokuwa anatoa hoja yake kuhusu maeneo yasiyokuwa rasmi kwamba, mpaka leo hawajapata vyeti. Lakini mfahamu kwamba, kazi ambayo imeanza hivi karibuni na inafanyiwa kazi ni kwanza, kufanya utambuzi wa maeneo, kutafuta taarifa, kuandaa ramani na kuwa kwenye *register* baadaye kuhakiki maeneo yao Wananchi wenyewe. Baada ya hapo wanaarifiwa kuwasilisha maombi yao ili wapate leseni. Kwa hiyo, si kazi ndogo lakini jitihada ambayo Wizara imefanya kuweza kuwasaidia Wananchi namna gani waweze kutambua maeneo yao na wawe na haki ya kumiliki kisheria pindi lolote linapoweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kujibu angalau kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa hapa leo kwa maandishi na kwa mdomo kwa Wabunge kadhaa. Nikianzia na Mheshimiwa Ali Said Salim, ambaye ni Msemaji mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, amesema Serikali imeshindwa kabisa kukitangaza kitengo chake cha Mradi wa Utafiti wa Nyumba za Bei Nafuu, yaani *National Housing Building Agency* na matokeo yake ni kwamba, Wananchi walio wengi hawanufaiki na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa ambayo Serikali imeifanya ni pamoja na kukifanya kitengo hiki kuwa Wakala wa Serikali. Ni kweli kwamba, Wananchi wengi hawajanufaika vya kutosha na kuwepo kwa kitengo hiki. Kwa hiyo, Serikali imefanya jitihada za makusudi kabisa kwa kuhusisha Wakala huu na Halmashauri za Wilaya. Aidha, semina za uhamasishaji, zimekuwa zikifanyika katika Halmashauri kila mwaka toka 2001 na 2002 hadi hivi sasa. Vikundi mbalimbali vimeundwa na vinaendelea kuundwa katika Wilaya ambazo uhamasishaji umeshafanyika. Vikundi hivi vitakuwa ni Wakala Utafiti wa Nyumba za Gharama Nafuu na vitapewa mafunzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi vilivyotafitiwa na Wakala.

Mbinu za ujenzi na mbinu za upunguzaji wa gharama za ujenzi, Wakala wamekuwa wakishiriki katika maonesho mbalimbali ya Kitaifa kila mwaka ambao ni Sabasaba na Nanenane pia. Aidha, Wakala inajitangaza katika vyombo vya habari kama televisheni, magazetini, kusambaza vipeperushi na kadhalika. Kwa kutumia mbinu hizi, Serikali inaamini kuwa hatimaye shughuli za Wakala zitanufaisha Watanzania wengi kwa kujipatia nyumba bora za gharama nafuu. Lakini ni vema Halmashauri za Wilaya nchini zikashirikiana na Wakala huu ili Wananchi waweze kujijengea nyumba bora kwa gharama nafuu kama watafuata maelekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwenye Kambi ya Upinzani wameuliza licha ya kuwa na Chuo Kikuu kinachotoa wataalamu wanaoshughulikia masuala mbalimbali ya ardhi na kuwepo na Idara za Mipango Miji katika kila Halmashauri. Bado kuna upungufu wa viwanja vilivyopimwa na miji yetu kuwa na ujenzi holela, maeneo yenye msongamano na kukosekana maeneo ya huduma ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji sura ya 378 ya mwaka 1956, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1961, Wizara yangu ina dhamana kisheria kusimamia ustawi wa maendeleo ya miji yetu. Wajibu wake kiutendaji unahusu mipango ya muda mrefu na kuandaa sheria, sera, kanuni na miongozo. Pia kwa mujibu wa sheria hiyo, wajibu wa kusimamia na kudhibiti utekelezaji wa mipango yote ya uendelezaji na ukuzaji wa miji wako kwenye Mamlaka ya Wizara za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kutoka kwenye Mfuko wa *RHFL* utolewe kwa Wananchi wote. Wakati Mfuko huu ulipoundwa masharti yalilenga watumishi wa Serikali tu. Wabunge, wakulima, wafugaji pamoja na makundi mengine, watanufaika kwa mikopo kwa ajili ya ujenzi au ununuzi wa nyumba unaoendelea kutayarishwa na Serikali kama vile ambavyo tunatarajia kupata Benki Maalum ya kuweza kuwakopesha Wananchi kupata mkopo na kujenga nyumba zao. Ukosefu wa mikopo unasababisha ujenzi wa nyumba kukua kwa kasi ndogo sana. Ni kweli lakini Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi *(UN HABITAT),* imeandaa Taarifa ya Mpango wa Kuendeleza Nyumba, itakayosaidia kuwepo kwa mikopo kwa ajili ya kununua au kujenga nyumba ikiwa ni sehemu mojawapo ya utekelezaji Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi. Pia upo umuhimu wa kulinda maeneo ya wazi na burudani.

Wizara ibaini na kuyatangaza maeneo haya hivyo hulindwa kisheria, isipokuwa Wananchi ndio wanaovamia na kujenga maeneo ambayo yako wazi. Pia Kambi hiyo imesema ujenzi wa nyumba katika maeneo yaliyopangwa unatakiwa kufanywa ndani ya miaka mitatu, lakini bado kuna Wananchi wanaweka misingi tu bila ya kufanya maendelezo. Ni kweli Wizara imekwisha andaa Mpango wa Taifa ya Kuendeleza Nyumba, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa. Lakini basi kuna sheria ambayo mtu ukishapewa kiwanja unatakiwa ujenge kwa miaka mitatu. Lakini ni kweli watu wamekuwa na mbinu za kujenga uzio na kuacha, jambo ambalo

lazima Wizara itakaa tena ifikirie upya jinsi gani tunaweza tukawadhibiti watu hawa, kwa sababu ni kweli wakijenga uzio bado kunabaki pori na maeneo yale hayaendelezwi.

Pamoja na kwamba, hivi karibuni Serikali imebuni mradi wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam, bei za viwanja hivyo ni za juu mno kwa watu wa kawaida kuweza kuzimudu. Matokeo yake ni kwamba, vingi kati ya viwanja hivyo, vitaangukia katika mikono ya watu wachache, wenye uwezo na Wananchi wa kawaida, ambao ndio wengi wataendelea na ujenzi holela katika maeneo yasiyofaa. Bei za viwanja katika mradi wa kupima viwanja 20,000 Mjini Dar es Salaam ni asilimia 80 tu ya *roll* zilizotumika kuzalisha viwanja hivyo. Sehemu iliyobaki ambayo ni asilimia 20 ya gharama ilibebwa na mishahara na posho za watumishi waliotumika katika mchakato mzima wa kutekeleza mradi huo. Gharama hizo hazikuhusishwa makusudi ili kuleta nafuu ya bei ya kiwanja.

Gharama za kuzalisha viwanja hivyo inahusu yafuatayo: Kutambua maeneo ya kuweka mradi, kuandaa michoro ya viwanja hivyo, kufanya uthamini wa mashamba na mali zilizokutwa kwenye maeneo hayo, kulipa fidia ya mashamba na mali zilizokutwa kwenye maeneo hayo, kupima viwanja, kumilikisha viwanja, kuweka miundombinu ya barabara katika maeneo hayo na hata hivyo bado miundombinu mingine haijakamilika, kwa mfano, maji imezungumzwa hapa katika Wizara ya Nishati. Sehemu kubwa ya gharama katika shughuli zilizotajwa hapo juu ni kupata maeneo huru ya kuweka mradi wa kulipa fidia. Hadi sasa eneo hili limegharimu mradi wa kiasi cha shilingi bilioni 17.1 kati ya shilingi bilioni 21.9 gharama za mradi mzima. Kwa hiyo, mwone kwamba, lazima hela zirudishwe kwa sababu zilikuwa za mkopo.

Waheshimiwa Wabunge, lazima tukubali gharama za kiwanja ni ndogo ikizingatiwa maelezo yangu ya kina ambayo nimeyatoa hapo awali. Bei zikipangwa kuzingatia ukubwa wa kiwanja, mahali kilipo na matumizi yake mathalani eneo la Mwanagati katika Manispaa ya Temeke, kiwanja kidogo cha mita za mraba kati ya 400 hadi 600 kinagharimu Sh. 200,000/= hadi Sh. 300,000/= na kiwanja cha ukubwa wa namna hiyo Bunju katika Manispaa ya Kinondoni kinagharimu Sh. 500,000/= hadi Sh.700,000/=. Kutokana na thamani ya ardhi katika eneo husika, kwa viwango hivyo, ilikuwa fursa mwananchi kuchagua eneo mahali anakotaka kwa kuzingatia bei ya viwanja hivyo.

Kuna kifungu cha sheria katika Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 inayomtaka mmiliki wa kiwanja ajenge nyumba katika kipindi cha miezi 36 au miaka mitatu. Sheria hii inatumika kuwabana watakaonunua viwanja vingi, kwani ni gharama zaidi kujenga nyumba nyingi katika kipindi kifupi. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa mtu hutumia chumba kimoja katika usiku mmoja, ni dhahiri kwamba, nyingine zitatumiwa na Wananchi wengine kwa gharama nafuu hivyo kuwezesha walioshindwa kupata viwanja na kujenga kuweza kupanga nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walieleza dira ya Wizara kuhusu ulipaji wa kodi ya majengo ikusanywapo Wilayani, inaweza kuleta matatizo au inaleta matatizo kwani kodi kwa jengo inakadiriwa tu hakuna kigezo zaidi ya macho ya makusanyo kulingana na anavyoliona hilo jengo. Kambi ya Upinzani, inaiomba Wizara itoe mwongozo kuhusu

kodi za pango. Kambi ya Upinzani inawasilisha hoja inayohusu kodi hizo hasa *Property Tax* inakusanywa na Halmashauri si Wizara. Lakini kama ni dhahiri basi tutajaribu kuzungumza kwa sababu zote ni Serikali, tuone vipi wanaweza wasitoze kodi kubwa bila kutumia sheria au taratibu.

Kubadili hati za umilikaji ardhi wa miaka 33 zilizotolewa na wazawa na wamiliki uwe wa miaka 99 kama ilivyo kwa wageni. Utoaji wa muda wa milki unategemea mpango wa uendelezaji wa eneo usio kwa misingi ya matumizi na ukubwa wa viwanja sambamba na eneo katikati ya mji. Mpango wa uendelezaji unatenga maendeleo katika vipindi vya mwaka 33, 66 na 99. Mathalani milki ya miaka 99 hutolewa kwa ajili ya wawekezaji wa milki kwa ndani na nje viwanja vyenye ujazo wa chini ya makazi *(Low Density Plots),* pamoja na mashamba ya kilimo na ufugaji. Aidha, muda wa miaka 33 hutolewa na matumizi kwa makazi kwa viwanja vya ujazo wa juu *(High Density).* Viwanja vya katikati ya mji kwa tahadhari ya kuwezeshwa utekelezaji wa mpango mpya wa uendelezaji wa mji. Kwa msingi huu, utoaji wa muda wa milki hautegemei Wizara wala ugeni, bali masharti ya mpango wa uendelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Said Ali, ameuliza kuna uhusiano gani wa Mradi wa *HABITAT* kwa Mheshimiwa Anna Tibaijuka na Idara ya Mipango Miji. Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Shirika la *HABITAT,* imetambua mchango wa Mheshimiwa Anna Tibaijuka na kuona kwamba, wanawake wanapewa kipaumbele katika kuwapatia makazi. Kwa kuanzia, Wizara imetenga viwanja eneo la Kizota Mjini Dar es Salaam kwa ajili ya kukiwezesha kikundi cha wanawake kupata viwanja na hatimaye kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ameuliza je, ni kwa kiasi gani Wizara hii hushirikiana na Wizara ya Kilimo ili kuharakisha maendeleo Kitaifa. Ningeshauri kuwepo kwa ukaribu na ukaribu wa Wizara hiyo ndipo utakapoondoa umaskini nchini hasa kupima mashamba. Ni kweli Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Wizara ya Kilimo zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu tangu mwaka 1995 na 1997, zikishirikiana chini ya Mradi wa Kuendeleza Misitu ya *Forestry Resource Management Project,* kutambua mipaka ya Vijiji, pamoja na kupima Vijiji. Pia katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara hizi zilishirikiana katika zoezi la kutambua ardhi inayofaa kwa kilimo kuingizwa katika hazina ya ardhi *(Land Bank).* Wengine wamesema *Land Bank* pengine kuna mahali tumeweka fedha, hapana. *Land Bank* ni ardhi yenyewe ndiyo inafanywa kuwa ni Benki. Nilipata maswali hapa kuwa vipi tunagawa au tunawawezesha watu kutumia au kukopa kwenye *Land Bank.* Kwa hiyo, nasisitiza kwamba, *Land Bank* ni Benki yenyewe, ardhi ndiyo Benki yetu.

Wizara imefanikiwa kutayarisha mkakati wa utekelezaji wa Sheria ya Ardhi kupitia fedha za miradi iliyoko Wizara ya Kilimo. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 viongozi wa juu wa Wizara hizi wamefanya mazungumzo ili utekelezaji, mkakati wa upimaji Vijiji, kujenga masjala ya Vijiji na Wilaya. Sasa hivi wataalamu wa Wizara hizi wanafanyia kazi utaratibu wa kupanga fedha kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Paul Kimiti ameuliza katika maeneo ya mji *proper,* ni kigezo kipi kinatumika ili Wananchi waweze kumiliki eneo zaidi la eka tatu za kulima au kuweka eneo la ufugaji. Je, ni kweli maeneo yaliyomo katika Miji, Manispaa na Jiji, hayawezi kupewa hati ya kumiliki mashamba zaidi ya eka tatu? Mwongozo wa nchi nzima utolewe ili tusiwaachie kila mmoja atekeleze aonavyo. Ni kweli kufuatana na tangazo la Serikali Namba 1 la mwaka 2001, hairuhusiwi kutoa milki ya shamba chini ya eka tatu katika maeneo ya miji. Mwananchi anaruhusiwa kumilikishwa shamba zaidi ya eka tatu katika maeneo hayo. Wizara yangu itazikumbusha Halmashauri Kuu kuhusu uzingatiaji wa tangazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura ameulizia mipaka kati ya nchi iliyowekwa na Wakoloni haikuzingatia tabia halisi ya mito ambayo huhama na kubadisha mikondo yake. Mto Ruvuma una tabia ya kuhamahama na kubadilisha mkondo wake na hivyo kuathiri upande wa ardhi wa nchi moja au nyingine. Inashauriwa Wizara kwa kushirikiana na nchi jirani, kupima upya mipaka hiyo na kuweka *beacons* kwa kutumia vifaa vya kisasa kama *global position system.* Nafikiri labda alikuwa hajafahamu, kazi hii imeanza kufanywa muda mrefu. Mipaka ya enzi ya ukoloni haikuzingatia masuala mengi kwa sababu ya uelewa mdogo wa jiografia na hali halisi ya nchi zetu. Mara nyingi ugawaji na umegaji ulifanywa huko Ulaya kwa misingi ya taarifa na ufahamu mdogo uliokuwepo. Baada ya kupata uhuru, nchi zetu zilirithi mipaka kama ilivyokuwa wakati huo ili kudumisha amani na utulivu. Baadaye kinachofanyika ni maelewano kati ya nchi kwa nchi kurithi mipaka hiyo au kuijadili na kuirekebisha ipasavyo. Hili ndilo linalofanyika kati ya Tanzania na Malawi katika Mto Songwe, ambao uhamahama kwa kiwango kikubwa. Upembuzi yakinifu wa Mto Songwe ulibainisha kuwa ni vema nchi zenye tatizo la aina hii, kubuni na kutekeleza mipango ya maendeleo katika bonde kwa lengo la kudhibiti mto na kuleta maendeleo ya pamoja kwa wote. Hii ni dhana nzuri zaidi kuliko kuweka *beacons* na kisha kuachia mto ukaendelea kuhama na kuharibu mazingira. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, unazingatiwa kwa misingi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucas Selelii, ameuliza, Wizara ina mpango gani kwa miji midogo kama Ndala, Nata, Puge katika jimbo lake la Nzega linalokua haraka ili kulipatia ramani. Wizara ya Ardhi itasaidia kutoa ramani za awali kwenye maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ili ramani hizo zitumiwe na Halmashauri husika katika kutayarisha michoro ya mipango miji, ambayo hatimaye itawezesha wapimaji kutoka Halmashauri ya Wilaya husika kupima viwanja.

Ameuliza kama Wizara inaweza kuziwezesha Halmashauri za Wilaya Nzega kifedha, kivifaa na kitaalamu ili kununua viwanja katika miji midogo. Wizara ya Ardhi inasikitika kusema kwamba, haiwajibiki na suala la kuiwezesha Wilaya ya Nzega kifedha. Wataalamu na vifaa vya kupimia huo ni wajibu wa TAMISEMI. Kwa kuwa yeye ni mmoja wa Madiwani katika Halmashauri, ningeomba ashiriki katika vikao hivyo, kuwashauri na kuwashawishi kuweza kupata vifaa hivyo na wataalamu pia. Amezungumzia kuwa kuna upungufu wa wataalamu katika sekta ya ardhi. Ni wajibu wa TAMISEMI pia kuajiri wataalamu wanaohitajika katika kuendeleza Halmashauri za

Wilaya ambazo ziko chini ya TAMISEMI. Lakini namwomba tu aendelee kushiriki katika vikao ili awashauri na aone umuhimu wa kuwapata wataalamu hawa.

Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, amekumbushia ombi lake la wapima ardhi kwenda jimboni kupima eneo la majenzi mapya katika Mji mpya wa Namtumbo. Sio wajibu wa Wizara ya Ardhi kuwaruhusu wapimaji wa Halmashauri ya Namtumbo kwenda kupima eneo la majenzi mapya katika eneo la Mji mpya wa Namtumbo, bali ni wajibu wa Wizara ya Ardhi kutayarisha ramani za awali za maeneo mbalimbali nchini ili ziwawezeshe wataalamu wa ardhi walioko katika Ofisi ya Halmashauri kuchora michoro ya kubuni *(TV Drawings),* ambayo hatimaye hutumika katika upimaji wa viwanja vya eneo husika.

Mheshimiwa Halima Kimbau, amesema leseni za makazi zimetolewa lakini ardhi hiyo haiwezi kuwa mali bila hatimiliki hivyo, kushindwa kutolewa mikopo kwa sababu inayoelezwa kuwa ramani haijapitishwa. Jitihada za mikopo zifanywe ili Wizara ikope kutengeneza ramani. Leseni zilitolewa kwa maeneo yaliyorasimishwa, zinaweza kutumika kupata mikopo toka vyombo vya fedha, mkakati ambao Wizara imeuweka ili kuelimisha vyombo hivyo, kuitambua leseni hiyo kwa rehani ya mkopo. Aidha, kuna ramani za upimaji ambazo hazijakamilishwa kukaguliwa na hatimaye kuidhinishwa. Wizara imeweka mkakati wa kukamilisha kazi hiyo ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hoja ya *Mafuta House.* Lakini Waheshimiwa Wabunge nafikiri tunalirudia tu, ilielezwa vizuri sana na Serikali kuhusu *Mafuta House* na kwamba, Serikali ilizingatia hayo yote mliyoshauri na yaliyoanza kufanyika pia yalielezwa. Kwa hiyo, nina hakika sio upande wa Mafuta tu, yaani *TPDC,* lakini hata *National Housing Corporation,* nina hakika nayo imo ndani mle itashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu ambazo zitachambuliwa. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, hakuna dhuluma itakayofanyika, jengo lile litapata faida kwa wote walioanzisha na hata wale wanaoendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba sasa, niendelee kushukuru kwa kipindi cha miaka mitano ambacho nimefanya kazi nanyi Waheshimwa Wabunge ndani ya Bunge hili. Lakini nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema kwa kipindi chote cha miaka mitano niliyokuwa Bungeni na kuniwezesha kufanya kazi za Ubunge na za Wizara ya Ardhi bila ya kuwa na vikwazo. Nianze kuwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Igalula kwa jinsi walivyonienzi kunisaidia, kunishauri, kushiriki katika ujenzi wa huduma za jamii ndani ya maeneo yao. Kipindi chote nimekuwa na faraja na kunirahisishia kazi za jimbo. Pia nashukuru chama changu cha CCM ndani ya jimbo. Jinsi viongozi wapenzi walivyokieneza chama hicho katika jimbo langu na kupata Wana-CCM wengi kuliko miaka mitano iliyopita. Wengi waliokuwa sio wanachama wameingia katika chama na wale waliotupa kadi zao za Upinzani wakaingia CCM. Pia wamekuwa walinzi sana wa Ilani ya Uchaguzi na kukemea wazembe na wavivu wa maendeleo ndani ya jimbo langu. Kwa mshikamano huo, natumai nikirudi kuomba ridhaa yenu tena mtaniunga mkono kwani wengine wachache ambao hivi sasa wanahangaika huko majimboni, waungwana wanasema

kwamba, hakuna mvua isiyokuwa na mbu. Kwa hiyo, naona kwamba, hao ni mbu tu katika mvua nyingi lakini mwenyewe nipo. *(Makofi)*

Katika upande wa Wizara, kwa dhati kabisa, namshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Gideon Cheyo, ambaye nimemkuta akiwa mzoefu, amenisaidia sana katika kumsaidia kazi za Wizara hii, si kwenye usimamizi na utendaji tu. Amenivumilia wakati naonesha ukomandoo katika utekelezaji wa kazi zetu, lakini kwa kuwa ni muumini safi wa dini, amekuwa akinielekeza vyema na pia kuniunga mkono wakati namshauri vyema. Namtakia kila la kheri huko Ileje ili Wananchi wake wamuenzi tena ili arudi kwenye jengo jipya, akae atulie kwa umakini, kama kawaida yake na kutumiza wajibu wake kwa waliomchagua. *(Makofi)*

Niendelee kumshukuru mdogo wangu, Ndugu Salome Sijaona, akiwa mzoefu katika utumishi na utawala, amenisaidia sana katika maamuzi ya kikazi hapo Wizarani. Ni mtu makini, anapenda wafanyakazi na kuwawezesha kufanya kazi yao vizuri, mwenye ushirikiano na wenzake katika kazi bila kujali ngazi za utumishi, bila ya kuwasahau watendaji wote wa ngazi zote walionipa ushirikiano mzuri katika kazi. Wa mwisho lakini si kwa umuhimu, ni Shirika la Nyumba. Nimekuwa karibu sana kiutendaji tukivumiliana katika kazi, lakini nina hakika walielewa kazi gani nafanya kuanzia Bodi yake na Watendaji wote, nawashukuru sana kwa yote mliyonisaidia. Naendelea kumshukuru pia Mawaziri na hasa Wabunge, ambao mmenisaidia kuanzia Spika na Watendaji wake wote, kwa kweli kazi yangu nimeiona rahisi katika miaka yote niliyokuwa katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwape pole wote ambao tunajiandaa kwenye majimbo. Mwenyezi Mungu, atawajalia kwa sababu mtavuna mlichopanda. Naomba sana mrudi mkatetee vyama na wengi wawe wa CCM, Wapinzani wabakie wachache ili tuwaburuze katika Bunge jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naendelea kuunga hoja mkono ili Wizara hii ipite, kwa kweli kazi mmemaliza, naomba tu mfike hapa mkubali ili twende tufanye kazi kwa hela mtakazotupa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii tena niweze kuhitimisha hoja yangu.

Kama ilivyo ada, naomba awali ya yote, niwatambue waliochangia hoja yangu. Waliochangia kwa kauli humu ndani ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Edson Halinga na MheshimiwaTatu Ntimizi, ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Herbert James

Mntangi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Edward Ndeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu. Namshukuru kipekee, Naibu Waziri, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, kwa kunisaidia kujibu baadhi ya hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, natumaini majibu yaliyotolewa yametosheleza. Mimi nitajielekeza katika masuala machache yanayohitaji ufafanuzi na msisitizo, pamoja na majibu yetu hapa, kama ilivyo kawaida, michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, itajibiwa kwa maandishi na kuwasilishwa kwao kabla hatujamaliza Mkutano huu.

Aidha, napenda nitoe taarifa kwamba, tumekwisha toa majibu ya maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliohusika katika mijadala iliyopita, kuanzia kwenye Kamati ya Kilimo na Ardhi, Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali, hoja ya Bajeti ya Serikali, hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na TAMISEMI. Tumekwisha jibu na kuwagawia Waheshimiwa Wabunge wanaohusika na ukiangalia baadhi ya yale ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa leo, yamejirudia na tumekwisha yajibu tayari na kuwapelekea Waheshimiwa Wabunge wanaohusika.

Baada ya hapo, nitoe shukrani kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa taarifa yao na mapendekezo na maoni waliyotoa kwenye taarifa yao. Kwa ujumla tunaipokea taarifa hiyo na yote yaliyopendekezwa na kushauriwa tunayachukua na mengine kwa kweli tumekwishaanza kuyafanyia kazi na kwa hiyo, tunashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmefanya na tutaendelea kuyashughulikia. *(Makofi)*

Pia napenda kumshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa mawasilisho yake, pamoja na kwamba, tumegusia kidogo kumjibu lakini nimhakikishie tu kwamba, kama ilivyo kawaida, tutamjibu kwa maandishi. Baadhi ya hoja walizotoa zimejirudia za mwaka 2004, ambazo tulikwisha jibu, lakini kwa hiyo, tutazijibu tena ili kufafanua ziweze kueleweka na tunataka mambo yetu yawe kwenye kumbukumbu ili yaweze kueleweka vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie masuala machache maalum, kwanza, urasimishaji wa rasilimali mfu. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa MKURABITA, kwa maelezo yake fasaha, ambayo aliyatoa wakati wa kuchangia hoja hii. Wizara tumeanza kazi hii lakini uwezo wetu ni mdogo. Naamini wenzetu wa Wizara ya Fedha, wamekwisha sikia na kuona umuhimu wa zoezi linaloendelea hivi sasa na kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, Serikali ijayo itaendelea kuiwezesha Wizara yangu na Halmashauri zote kuendeleza zoezi hili muhimu, kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya yenye uhakika. *(Makofi)*

Napenda kutumia nafasi hii, kuvishukuru vyombo vya habari kwa kuhamasisha umma kushiriki kwa vitendo katika mipango hii ya kurasimisha mali mfu. Nina mifano michache ya maoni ya wahariri wa magazeti ya Uhuru, Nipashe, Mwananchi na Mtanzania ya mwezi Mei. Baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa Taifa mwezi wa nne, magazeti yametusaidia sana kuweza kufafanua na kuhamasisha Wananchi ili waelewe umuhimu wa ardhi, pamoja na nyumba kama rasilimali za msingi katika maendeleo yao.

Mhariri wa Uhuru anasema, Wananchi tuamke tuifanyie kazi ardhi ili itutoe katika umaskini, Nipashe wanasema, tuzinduke tutumie ardhi kujiendeleza na pia wanasema tuuchangamkie mpango huu wa leseni za nyumba, Mtanzania wanasema, makazi yasiyopangwa kupatiwa leseni, uwe ukombozi kwa Wananchi. Ujumbe huu tungependa uendelezwe tena na tena ili Wananchi waweze kuelewa umuhimu wa ardhi na makazi yao kwamba ni muhimu, yapewe thamani ambayo inajulikana iwasaidie katika maendeleo yao katika maeneo wanayoishi. Kwa hiyo, tunaomba changamoto hii iendelee.

Pili, suala la uendelezaji wa sekta ya nyumba, napenda nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, kwa mchango wake mzuri katika eneo hili. Ni kweli Mheshimiwa Dr. Milton Mhanga, amekuwa akichangia suala hili karibu kila mwaka na sisi tunatambua mchango wake muhimu na kwa kuwa amekuwa karibu sana na Wizara yetu, anajua nini kinachoendelea na kinachofanyika. Kwa hiyo, pamoja na zoezi linaloendelea ambalo linasimamiwa na Wizara ya Fedha, mapendekezo mbadala au yenye kuboresha yale ya awali kama Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga alivyopendekeza, tunadhani yana mantiki, ni vizuri yakazingatiwa ili katika awamu inayokuja, haya yote tuweze kuyaweka pamoja na tuone kama tunaweza kuanza kwa haraka iwezekanavyo kuwa na mfumo huu wa kutuwezesha kuwa na mahali pa kuweza kukopa kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba katika Taifa letu. Natumaini wadau wote wa ndani na nje ya nchi, wataendelea kushirikiana na Serikali ili kufanikisha zoezi hili mapema kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni uhusianao kati ya Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa, yaani Halmashauri. Suala hili limekuwa likijitokeza sana katika mijadala humu ndani, kuhoji au kuzungumzia mfumo tulionao hivi sasa wa madaraka kwenda kwa Wananchi Mikoani mpaka Wilayani. Uhusiano wa Wizara na Halmashauri umekuwa ukizungumziwa sana. Sasa mara kwa mara tumekuwa tukijibu kwamba, kuna mgawanyo wa madaraka, Wizara tuna mipaka yetu ya majukumu yetu na wenzetu katika Mikoa na Wilaya kwenye Halmashauri wana majukumu yao kupitia TAMISEMI.

Tumekuwa tukieleza hayo lakini inaelekea bado kuna dukuduku na wasiwasi. Kwa kuwa siwezi kutoa kauli hapa kuhusu suala hilo, niseme tu pengine haja ipo ya kutathmi mfumo mzima, tuone utekelezaji wake umekuwaje, matatizo yakoje ili kama ni lazima kuweza kuwa na marekebisho ya hapa na pale ili kuleta ufanisi katika utendaji katika ngazi zote kutoka Wizarani kwenda Mkoani mpaka kwenye Halmashauri zetu.

Lakini tunavyoelewa sisi, kwa mfano, katika sekta yetu ya ardhi, kila Halmashauri kuna Kamati ya kugawa ardhi na Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi wa Halmashauri husika na ile Kamati iko chini ya Halmashauri, inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya msingi ya Halmashauri yake kuhusu matumizi ya ardhi katika eneo lake. Kwa hiyo, sisi tunadhani kwamba, hiyo Kamati itafanya kazi kwa kuzingatia maelekezo ya jumla ya Halmashauri yao na kila kinachofanyika kwenye Halmashauri tunadhani ni lazima Mkuu wa Wilaya atafahamishwa na vivyo hivyo, Mkuu wa Mkoa, atajua nini kinatendeka katika Wilaya zake na Halmashauri zake.

Kwa hiyo, tulidhani kusingekuwa na tatizo la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kuelewa nini kinafanyika katika maeneo yao. Lakini kama kuna matatizo, kama nilivyosema, kuna haja ya kuiangalia na kutathmini ili tuwe na mfumo wenye uhakika zaidi wa kuleta ufanisi na uwajibikaji katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujumuisha haya yote yaliyofanyika na yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na mimi nimalizie kwa kutoa shukrani. Kwanza, lazima niendelee kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi walisema kwamba, Wizara hii ilikuwa inanuka kutokana na utendaji wake mbovu usioridhisha, sasa hivi tunashukuru kwa kauli zenu kwamba, mmeona yapo mabadiliko. Lakini hayo mabadiliko hayakuja hivi hivi tu, yamefanyiwa kazi na kwanza kabisa pongezi lazima tuzielekeze kwa Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Amekuwa karibu sana, ameelewa sana matatizo ya Wizara yetu, ametoa maelekezo na msukumo ili tuweze kufanya yale ambayo tulitakiwa tuyafanye katika kuleta hali hii ambayo tunaiona hivi sasa. Mambo mengine yalikuwa ni magumu sana kuyafanya na kama Waziri, pengine ilikuwa ni vigumu kuyafanya peke yangu na wasaidizi wangu. Tulihitaji msukumo na *support* ya uongozi wa juu. *Support* hiyo tuliipata kutoka kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ilitupa nguvu kuweza kufanya yale ambayo tuliyafanya, kuleta hali hii ambayo tunaiona hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Makamu wa Rais, naye amekuwa karibu na Wizara yetu, kutushauri na kutuelekeza ili tuweze kuleta ufanisi zaidi katika utendaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametusaidia sana, kama kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ametusaidia ndani ya Bunge na nje ya Bunge na kutukwamua pale ambapo tulikuwa tunakwama ili tuweze kusonga mbele, tutende yale ambayo tulipaswa kuyatenda kwa maslahi ya Taifa letu. Kwa hiyo, tunawashukuru sana viongozi wetu wote, kwa ushirikiano wao na msukumo wao na uongozi wao ambao umetuwezesha kuyafanya haya ambayo tunayashuhudia hivi sasa. *(Makofi)*

Kwa Watendaji wa Wizara yangu, pia nawashukuru. Walikuwa tayari, maana ilikuwa ni lazima tubadilike kiasi fulani katika utendaji wetu, lakini nashukuru kwamba, wengi wao walikuwa tayari kubadilika ili tutende yale yanayotupasa kutenda kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zote. Kwa hiyo, nawashukuru Watendaji wote, nikianzia awamu ya kwanza 1996 mpaka 2000, maana ndiyo ulikuwa msingi wa haya tunayoyaona hivi sasa. Tumeshirikiana vizuri alipokuwa Katibu Mkuu, Ndugu Mmari na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir. Tulishirikiana vizuri miaka mitano ile, kuweka misingi mizuri ya utendaji bora katika Wizara yetu. Katika kipindi hiki cha mwisho, uongozi uliopo hivi sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona na Watendaji wote, sasa tunashirikiana kuendeleza yale ambayo sasa hivi tunaona kwamba Wizara imetulia, imetengemaa. *(Makofi)*

Sasa wito kwa Awamu ya Nne ni kwamba, misingi mizuri iliyowekwa sasa hivi, bila shaka itaendelezwa ili rasilimali ardhi na nyumba ziweze kutumika kweli kwa kutuondolea umaskini Watanzania na kutuletea utajiri na tuweze kufanikiwa katika maendeleo yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru wote katika ujumla wenu, nawashukuru sana Kambi zote mbili, tumekuwa na ushirikiano mzuri. Nawashukuru kwa imani yenu na heshima yenu mliyotupa, tunawashukuru sana.

Pamoja na vyeo vya utani, majina ya utani niliyopewa, lakini kwangu imekuwa ni faraja maana pengine yamenisaidia kuniweka sawa na kuwafanya wale ambao walitaka kufanya mambo ya ajabu ajabu wakiniona tu basi wanakwepa. Kwa hiyo, nawashukuru sana, Mwenyezi Mungu, atujalie wote tuweze kuyapata yale tunayotarajia na tunaokwenda kugombea, basi Mwenyezi Mungu, atujalie tuweze kufanikiwa turudi tena tushirikiane katika Awamu ya Nne ijayo. *(Kicheko/Makofi)*)

Mwisho kabisa, napenda kuishukuru familia yangu na Wananchi wa Ileje, wamenielewa kipindi chote hiki na wamenisaidia wakati ambapo sikuwa pamoja nao, lakini walielewa kwamba, tuna majukumu ya Kitaifa lazima tuyafanye na nashukuru kwa uvumilivu wao na naomba niwahakikishie kwamba, hakuna kilichopotea, badala yake tumepata baraka nyingi na Mungu apewe sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote na naomba sasa niwaombe tupitishe haya tuliyoomba ili tukafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, watu walianza kujiuliza majina ya utani ni yepi? Jina la utani alilokuwa anaitwa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo ni Askofu. Kwa hiyo, watu wakimwona wanaona wasifanye dhambi mbele ya Askofu. *(Kicheko)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

| | |
|---|---|
| Kifungu 1001 - *Administration and General* | Sh.2,536,928,200/= |
| Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* | Sh.1,174,185,200/= |
| Kifungu 1003 - *Policy and Planning* | Sh. 463,964,900/= |
| Kifungu 1004 - *Management Information System* | Sh. 253,613,400/= |
| Kifungu 2001 - *Land Development* | Sh.1,330,468,000/= |
| Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping* | Sh.1,196,443,600/= |
| Kifungu 2003 - *Customary Land Tribunal* | Sh. 156,576,800/= |
| Kifungu 3001 - *Human Settlement Development* | Sh,3,317,596,200/= |
| Kifungu 3003 - *Housing Appeal Tribunal* | Sh.1,292,618,700/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

| | |
|---|---|
| Kifungu 1003 - *Policy and Planning* | Sh.100,000,000/= |
| Kifungu 1004 - *Management Information System* | Sh.285,000,000/= |
| Kifungu 2001 - *Land Development* | Sh.1,300,000,000/= |
| Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping* | Sh.415,000,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Taarifa ya Kamati sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Leo hatuna matangazo yoyote hapa na hatuna shughuli nyingine. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.54 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 15 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*